Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Sita - Tarehe 8 Februari, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji wa Soko la Bima Nchini kwa mwaka Ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003 *(The Annual Insurance Market Performance Report for the Year Ended 31st December, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

**Na. 57**

**Watumishi Wanaofua Nguo za Wagonjwa Hospitalini**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa, watumishi wa hospitalini wanaofua nguo za wagonjwa wako kwenye hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa Ukimwi na magonjwa mengine ya hatari na kwa kuwa, katika hospitali zetu nyingi hazina vifaa vya kutosha kujikinga na maambukizo kutokana na ufuaji wa nguo za wagonjwa pamoja na usafi wa malazi ya wagonjwa kwa ujumla:-

Je, ni lini Serikali inatanunua mashine za kufulia nguo za wagonjwa katika hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kutokana na maombi yao ya siku nyingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hatari inayoweza kuwapata watumishi wanaotoa huduma ya kufua nguo za wagonjwa katika hospitali mbalimbali hapa nchini. Kwa kutambua hali hiyo, watumishi wa hospitali wamekuwa wanapatiwa mafunzo juu ya kujikinga au kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali wakati wa kutoa huduma hiyo. Aidha, watumishi wote wakiwemo wale wanaofua nguo za wagonjwa hupatiwa na kutumia vifaa vya kujikinga na maambukizi *(protective gears)*, kama *gloves, gum boots, masks* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo za kinga, Serikali inaelewa umuhimu wa kuwa na mashine za kufulia nguo za wagonjwa katika hospitali zake zote za Wilaya na Mikoa ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Serikali inaendelea kutafuta njia za kupata fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine hizo. Kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga, umepanga kuomba fedha kupitia fungu la Mpango wa Miradi ya Maendeleo ya Mkoa kwa mwaka 2006/2007. Aidha, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge anavyojitahidi kwa shughuli nyingine, basi alipe suala hili kipaumbele kwa kujaribu vile vile kwa kutumia nafasi alizonazo kutafuta Wahisani ili waweze kuona kama ataweza kusaidia katika suala hili. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Hivi nguo za wagonjwa gani zinazofuliwa katika hospitali? Kwa sababu naona wagonjwa wanavaa nguo zao wenyewe wanapokuwa hospitalini! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, ngoja tulichukulie kwamba ni ushauri mzuri kutoka kwa Mheshimiwa Pawa na tutashirikiana na Wizara ya Afya tuone tunatanyaje.

**Na. 58**

**Ukarabati wa Shule za Msingi Chakavu**

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Siha wamefurahishwa sana na mpango wa Serikali wa kuimarisha Elimu ya Msingi kupitia mpango wa MMEM na kwa kuwa katika Jimbo la Siha kuna Shule za Msingi ambazo majengo yake yamechakaa kiasi cha kusikitisha kwa mfano, Shule za Msingi Suumu, Kitahemwa, Kyengia, Mae, Wanri - Kati, Lakitore, Ngaronyi, Nkyare, Nasai, Monico, Maarabo na kadhalika:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Shule hizo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia Shule za Msingi zilizopo katika Jimbo la Siha ili kuondokana na hali hiyo, kwani kuna hatari kwamba Walimu na wanafunzi wanaweza kuangukiwa na majengo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulibuniwa na Serikali ili kuboresha Elimu ya Msingi iliyokuwa imeanza kudorora. Fedha za mpango huu hupelekwa Shuleni na matumizi yake kusimamiwa na Kamati za Shule. Fedha hizi zinahusisha fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, vyoo, nyumba za Walimu, kununua madawati na ujenzi wa matanki ya kuvuna maji ya mvua. Fedha nyingine zinahusisha fedha za uendeshaji wa Shule ambapo asilimia 40 hutumika kununua vitabu, asilimia 20 kukarabati majengo, asilimia 20 nyingine kununua madaftari, chaki na kalamu; asilimia 10 kugharamia mitihani ya ndani na asilimia 10 ya mwisho kwa ajili ya shughuli za Utawala. Fedha zinazotolewa kwa ajili ya ukarabati huzingatia idadi ya wanafunzi wote waliopo Shule katika mwaka husika na husimamiwa na Kamati za Shule. Hivyo kila shule inastahili kupata fedha za ukarabati kila mwaka.

Lakini kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Halmashauri ilikaa na kuamua kuwa fedha za ukarabati ziende kwenye Shule zile zilizokubaliana kuwa zilikuwa katika hali mbaya zaidi badala ya kupeleka fedha kidogo kidogo katika kila Shule ambazo hazitaweza kuleta matokeo au *impact*. Hadi sasa Shule 50 kati ya Shule 152 zilizomo katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambazo zipo kwenye hali mbaya zaidi zimepata jumla ya Shilingi milioni 60.4 kwa ajili ya ukarabati.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya Shule 11 alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, Shule sita zilipata jumla ya Sh.10,1164,300/= kwa ajili ya ukarabati kati ya mwaka 2002 na 2004.

Shule ya Msingi ya Suumu ilipata Sh. 957,000/=; Shule ya Msingi Kyengia ilipata Sh.1,736,800/=; Shule ya Msingi ya Ngarony Sh. 2,000,000/=; Shule ya Msingi ya Nasai Sh. 3,500,000/=; Shule ya Msingi ya Kitahamwe Sh. 1,000,000/= na Shule ya Msingi ya Nkyare Sh.1,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Shule za Msingi na ukarabati wa Shule hizo na uendelezaji wake kimsingi ni jukumu la wananchi kupitia Serikali zao za Vijiji na Halmashauri zao. Hata hivyo, kwa kuzingatia kushuka kwa ubora wa Shule za Msingi

hapa nchini na uwezo mdogo wa fedha unaozikabili Serikali za Mitaa, Serikali ililazimika kubuni mpango huu wa Elimu ya Msingi ili kuzisaidia Serikali hizo za Mitaa kuweza kuboresha Elimu ya Msingi hapa nchini ikiwemo ile ya Halmashauri ya Hai. Naomba nitoe wito kwa wananchi wote nchini kwanza kuupokea Mpango huu vizuri na kutumia fursa hii kuboresha Elimu ya Msingi katika maeneo yao. Serikali kwa upande wake itaendelea kushirikiana na wananchi kadri uwezo wa fedha utakavyokuwa unapatikana kuendeleza Elimu ya Msingi.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa amekubali kwamba ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Hai imekubaliana kwamba ipeleke hela katika Shule Maalum kwa maana ya kwamba ukizitawanya hazitaleta *impact* inayotakiwa na kwa vile mimi natambua kwamba Shule hizi nilizozitaja hapa ziko katika hali mbaya sana; Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutoa maelekezo maalum kwa ajili ya hizo Shule ili ziweze kutengewa mafungu maalum kwa ajili ya kufanya kazi hiyo au Serikali Kuu iingilie kati kwa maana ya kulipa fungu litakalosaidia katika ukarabati wa hizi Shule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, haitakuwa jambo jema kwa Serikali kutoa maelekezo ya moja kwa moja kwenda kwenye Halmashauri ya Hai kwa sababu Halmashauri hii ni Serikali ambayo imetoa madaraka kamili na katika kuamua inavyoamua sisi kwa upande mwingine tunaheshimu sana maamuzi yake. Lakini kwa upande mwingine ni kwamba labda Serikali Kuu itazame ni nini inaweza ikafanya kwa ajili ya Shule hizi ambazo ziko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa si rahisi sana kutokana na ukweli uliopo kwamba hali ya kifedha sio nzuri na Mpango huu ndiyo hasa ulilenga kujaribu kupunguza hilo tatizo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mwanri kwamba tuendelee kwanza na mpango huu tuone utatufikisha wapi na baada ya hapo nina hakika Serikali itaona kiwango ambacho tumesaidia kuboresha elimu na baadaye kutazama ni mpango gani mwingine au juhudi gani nyingine ifanywe ili kuzidi kuboresha hali ya Elimu ya Msingi.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la uandikishaji wa watoto kutokana na utekelezaji mzuri wa mpango wa MMEM na hususan kuondoa ada ya Sh. 2,700 kwa mwaka na wananchi wameitikia kwa kujenga Shule mpya za Msingi ili watoto hao waweze kusoma; Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wananchi ambao wanajenga hizi Shule mpya na ili kuwapunguzia mzigo wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Mpango huu wa MMEM umesababisha kuwepo kwa ongezeko kubwa sana la watoto ambao wanaandikishwa hivi sasa, hasa baada ya kuondoa ada kama alivyosema. Lakini ni kweli vile vile kwamba imedhihirika wazi kabisa kwamba makisio yaliyokuwepo ambayo tulikuwa tunadhani

yangeweza kusaidia katika ujenzi wa madarasa sasa hivi inaonekana kwamba makisio yale yamepitwa kabisa kwa maana ya kwamba wananchi wengi wameamua kujitolea zaidi kuliko tulivyokuwa tumefikiria.

Sasa hii ni changamoto sio kwa Serikali tu, lakini kwetu sisi wote kwamba tunafanya nini katika mazingira haya. Tunaloweza kusema tu ni kwamba kama nilivyosema wakati najibu swali lingine juzi, pengine twende kidogo kwa uangalifu katika kujaribu kuwahimiza wananchi kujitahidi kutoa kila linalowezekana kusaidia kujenga Shule, wasije wakahimizwa tu wakatengeneza maboma mengi ambapo uwezo wa Serikali ni mdogo sana. Kwa hiyo, twende kwa mahesabu kwa sasa ili tuwe na uhakika kwamba nguvu zao hazipotei.

**Na. 59**

**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Karema**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tarafa ya Karema Wilayani Mpanda haina Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo hata mmoja hali ambayo ni kero kubwa kwa wananchi wa Tarafa hiyo kuwagharimia wahalifu kwa kuwasafirisha hadi Mpanda kusikiliza mashauri yao na kwa kuwa Wilaya ya Nkasi haina Hakimu wa Wilaya wala Mahakama ya Mwanzo hata mmoja:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, hali ya namna hiyo haiboreshi dhana ya Utawala Bora?

(b) Kwa kuwa, uhaba wa Mahakimu unaelekea uko katika Tarafa nyingi hapa nchini; Je, ni lini Serikali itaondoa kero hiyo kwa kupeleka Mahakimu katika maeneo niliyataja katika swali hili, na vile vile Serikali itakuwa tayari kupeleka angalau Hakimu mmoja mmoja wa Mahakama ya Mwanzo kwa kila Tarafa nchini?

(c) Je, hadi sasa kuna upungufu wa Mahakimu wangapi wa Mahakama hizo hapa nchini na ni hatua gani zinachukuliwa kukabiliana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mahakama kama mojawapo ya nguzo kuu ya dola ina wajibu mkubwa na muhimu katika kuboresha dhana ya utawala bora na kuhakikisha kuwa mashauri yanayopelekwa Mahakamani yanatolewa uamuzi wa haki na kwa wakati. Kwa kuzingatia kuwa suala la uhaba wa Mahakimu linaathiri utawala bora, jitihada kubwa

inafanywa na Serikali, kuimarisha Mahakama kwa kuongeza idadi ya Mahakimu wa ngazi mbalimbali hatua kwa hatua.

(b) Kwa sasa kuna Mahakama za Mwanzo 1,105 hapa nchini na kuna Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 662 tu. Kwa maana hiyo, kuna upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 443 nchini. Kati ya Mahakama ambazo hazina Mahakimu, Karema ni mojawapo. Kwa wakati huu Mahakama ya Karema inapata huduma kutoka Mahakama za Mwanzo zilizopo jirani. Hivyo, suala la upatikanaji wa Mahakimu kwa kila Tarafa zote hapa nchini ni vigumu kutabiri uwezekano wake.

Lakini litakapopatikana jengo la Mahakama ya Wilaya ya Nkasi tutahakikisha kwamba Hakimu wake anapatikana. Kwa wakati huu Mahakama itaendelea kutoa huduma hiyo kutoka Mkoani Rukwa.

(d) Kama nilivyosema hapo awali, tunao upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 443. Ili kukabiliana na upungufu huu, upo mpango endelevu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ambapo Chuo kitapanuliwa ili kiwe na uwezo wa kuchukua kila mwaka wanafunzi 500 badala ya 50 hivi sasa. Aidha, bado Mahakama inaendelea kutoa ajira kwa mkataba kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo waliostaafu na wenye sifa, maadili na utendaji mzuri, ili kupunguza kero hiyo.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

(a) Kufuatia majibu ya Mheshimiwa Waziri, kutokana na upungufu wa Mahakimu hao ameutaja; je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za makusudi kwa haraka za kuwaajiri wale wote ambao wana *Diploma* na Shahada za Sheria ambao wako tayari kufanya kazi hiyo kwa lengo la kupunguza tatizo la Mahakimu katika maeneo yetu?

(b) Lakini lingine ni kwamba, kwa kuwa Wazee wa Baraza ni muhimu sana kusaidia Mahakimu kufikia uamzi wa haki na kwa kuwa Wazee wa Baraza wa kule Karema wana kero ya kupunjwa malipo yao wanayostahili kwa maelezo kuwa upungufu huo unaojitokeza analipwa mtu wa katikati ambao wao hawamfahamu; Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatilia suala hili na kuchukua hatua dhidi ya wahusika?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, nikiri kwamba upo upungufu na jitihada zinafanywa na Serikali kuweza kuwapata Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wengi zaidi. Pili, ni kwamba upo utaratibu wa kuwachukua Mahakimu wastaafu kwa muda fulani kuweza kusaidia katika kuendesha mashauri ndani ya Mahakama zetu.

Lakini suala ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Margareth Bwana, nikiri kwamba mpaka sasa hivi kuna vijana ambao wamepata *Diploma* zao kutoka Lushoto, lakini Idara ya Mahakama au Mahakama haijaweza kuwaajiri na zipo sababu za kukubali.

Moja, ni kuweza kupata kibali kutoka Utumishi. Lakini la pili pia ni kwamba, hawa ambao wamekwenda Lushoto na kuchukua *Diploma,* siyo kwamba wanaajiriwa moja kwa moja, inabidi wafanyiwe *interview* na kuona kwamba kweli wanaweza kumudu shughuli zile hasa kwa upande wa maadili. Kwa hiyo, tunalo tatizo hilo lakini tunalifanyia kazi.

Kuhusu suala la pili, Wazee wa Baraza niseme tu kwa jumla kwamba wanatusaidia sana katika kuendesha mashauri katika Mahakama za Mwanzo. Lakini kwa hili ambalo amelizungumzia, kama kuna matatizo ya Mzee wa Baraza hajalipwa pesa ama kuna mtu katikati ambaye anachukua pesa za Wazee wa Baraza ,basi tupate jina la huyo ili tuweze kumshughulikia kiutaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, naomba kuongezea majibu ya ziada kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti na kwa kutambua kwamba Mahakama nyingi za Mwanzo na Kati hazina watumishi wanaotakiwa, Ofisi ya Rais, Utumishi imetoa kibali cha jumla kwa Mahakimu hao kuajiriwa ilimradi kuwe na ikama na Bajeti ya kulipa pale ambapo wataajiriwa. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda tu kupata maelezo kwamba wakati tunatunga sheria kuanzisha Chuo cha Lushoto ambacho kwa kweli kinafanya kazi nzuri sana, Wabunge walitoa hoja na kusisitiza kwamba Mahakama zile za Mwanzo zilizo karibu na eneo la Chuo ziimarishwe ziwe za mfano. Kwa mfano Mahakama ya Soni, Mahakama ya Vuga, Subiri katika jimbo la Lushoto na kwa kuwa hilo halijafanyika; Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba ili kuimarisha mafunzo ya vitendo ni vyema Mahakama hizo zikakarabatiwa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge moja kwa moja kwamba tuliahidi tutafanya hivyo na tumechelewa kufanya hivyo na kiutendaji kwa kweli inabidi tufanye hivyo ili kuweza kuwapa *exposure* nzuri zaidi hawa Mahakimu ambao wanasoma pale Lushoto. Pengine Chuo hiki kingekuwa kiko Dar es Salaam au mahali pengine wangelikuwa na mazingira mazuri zaidi. Kwa hiyo, umuhimu wa kuboresha Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Lushoto ni muhimu ili kuweza kuwa na Mahakimu ambao ni bora zaidi. Kwa hiyo, suala hilo la Mahakama tutalifuatilia.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kama Mheshimiwa Waziri alivyokiri mwenyewe kwamba kuna upungufu wa Mahakamu 443 na kwamba amekiri lile ambalo Kamati yangu iliripoti ilipotoka Lushoto kwamba wahitimu wa Chuo cha Lushoto hawaajiriwi wote, sasa atakapokuwa anafundisha wanafunzi 500 badala ya 50 wa sasa ataweza namna gani kuwaajiri hawa kwa sababu alizozitoa pamoja na urasimu ndani ya Serikali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu lipo. Tatizo la hawa ambao wamehitimu kama Mahakimu na wengi hawajapata ajira lipo, kinachogomba sasa hivi ni suala la bajeti. Kwa jinsi hali yetu ya kiuchumi inavyoendelea kuwa nzuri na kwa jinsi Sekta ya Sheria na hasa Mahakama inavyopewa nafasi katika Utawala Bora na kupunguza umaskini, nadhani baada ya muda si mrefu tatizo hili litakuwa limekwisha.

**Na. 60**

**Soko kwa Mazao yanayolimwa Singida**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Iramba Mashariki na Singa Kaskazini wanaongoza kwa kilimo cha alizeti, vitunguu maji, giligilani na dengu na kwa kuwa, mazao hayo yamekuwa yakiwavutia sana wanunuzi kutoka sehemu nyingine za nchi hii kama vile Mwanza, Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar na hata nchi za jirani za Kenya na Rwanda:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, itakuwa ni jambo la busara na la manufaa kwa mapato ya nchi hii kujenga soko la kisasa kwa ajili ya kuuzia mazao hayo pale Iguguno ambako barabara kuu inapita?

(b) Kwa kuwa, mazao niliyotaja hapo juu bado yananunuliwa kwa bei ndogo sana; Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia wananchi wa maeneo hayo wanunuzi wa uhakika na bei nzuri?

(c) Kwa kuwa, bado kuna upungufu mkubwa sana wa Maafisa Ushirika karibu kwenye Wilaya zote nchini hivyo kuwafanya wakulima kukosa elimu ya Ushirika; Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mazao ya alizeti, vitunguu maji, giligiliani na dengu yanayolimwa Mkoani Singida, hususan katika Majimbo ya Iramba Mashariki na Singida Kaskazini huuzwa kwa wanunuzi binafsi moja kwa moja kutoka kwa wakulima au kupitia Vituo vidogo vidogo vya biashara Vijijini (*Rural Trading Centres*) vilivyoko kwenye maeneo ya Vijiji vinavyozalisha mazao hayo. Kutokana na utaratibu huo unaotumika kuyauza mazao hayo ni dhahiri kuwa wakulima hao hawana mahali stahili pa kuuzia mazao yao na kwa hiyo wazo la Mheshimiwa Mbunge la kuwajengea soko la kisasa hapo Iguguno ni la msingi na Serikali inaliunga mkono.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendeleza juhudi za wakulima za kuzalisha mazao mbalimbali yakiwemo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza programu kadhaa za kuendeleza mifumo ya masoko nchini ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na Benki ya Dunia kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ili kuongeza uwezo wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo katika Wilaya zote nchini. Jitihada hizi za Serikali zina lengo la kuziwezesha Halmashauri za Wilaya nchini kupata fursa ya kuibua miradi ya kuendeleza miundombinu ya masoko katika maeneo yao likiwemo eneo la Iguguno ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Ni matumaini yangu kuwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wataupatia kipaumbele mradi wa ujenzi wa soko hilo ili uweze kuibuliwa kama mradi wa kuendeleza miundombinu ya masoko na Serikali itakuwa tayari kushirikiana nao.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza katika jibu la sehemu (a) ya swali hili, Serikali imekwishaandaa na kuanza kutekeleza programu za uendelezaji wa mifumo ya masoko zenye lengo la kuwapatia wakulima nchini kote Masoko ya uhakika na bei nzuri kwa mazao yao yakiwemo yale aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Sambamba na hatua hiyo, Serikali imeendelea kuzihimiza Halmashauri za Wilaya zote nchini kutenga na kuendeleza maeneo maalum au (magulio) kwa ajili ya kuuzia mazao ya wakulima ili kuwezesha ushindani wa wazi na wa haki kwa kuwakutanisha wakulima na wanunuzi wa mazao hayo katika eneo moja.

Aidha, Serikali imeendelea kuwahamasisha wakulima wadogo wadogo kujiunga katika vikundi au Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuyauza mazao yao kwa pamoja na hivyo kuwavutia wanunuzi wengi kutokana na urahisi wa kupata mazao mengi katika eneo moja. Serikali pia inawahimiza wakulima mmoja mmoja au kwa kupitia katika Vyama vyao vya Ushirika kila inapowezekana kusindika mazao kabla ya kuyauza ili kupata bei nzuri zaidi.

Vile vile Serikali imekwisha kamilisha mapitio ya mahitaji ya taarifa za masoko na hivi sasa utaratibu unafanyika ili taarifa hizo ziweze kuwa zinapatikana kupitia Redio za Mikoani Televisheni, simu za mikononi na *Agribusiness Directory* inayoandaliwa kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa za masoko kati ya wazalishaji, wauzaji na wanunuzi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi za Serikali zinalenga katika kuweka mazingira yatakayowezesha wakulima na wanunuzi kukutana au kuwasiliana na kuuziana mazao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu suala la upungufu mkubwa wa Maafisa Ushirika kwenye baadhi ya Wilaya hapa nchini. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, kila Mwajiri amepewa mamlaka ya kuajiri, kupandisha vyeo na kushughulikia nidhamu ya watumishi wote walio chini yake. Ni wajibu wa Mkuruenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuajiri Maafisa Ushirika wanaotakiwa ili kumaliza tatizo hilo. Wilaya nyingi

zimekwishatangaza na kujaza nafasi kulipokuwa na upungufu wa Maafisa Ushirika chini ya utaratibu huu.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri cha msingi hapa ni kwamba mkulima anahitaji apate bei nzuri ya mazao yake. Lakini Wizara ya Ushirika na Masoko ambayo tulitegemea ingemsaidia mkulima imekuwa haimtendei haki mkulima kama inavyotakiwa. Matokeo yake inakuwa inasema wanaandaa programu na mikakati. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambiaje kwamba wakulima ambao bei za mazao yao inazidi kudorora watasaidiwa namna gani badala ya programu ambazo zinazungumzwa kila leo?

Pili, Mheshimiwa Spika..

**SPIKA:** Hapana! Unaruhusiwa swali moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba Wizara ya Ushirika na Masoko haiwatendei haki au Serikali kwa ujumla haiwatendei haki wakulima, nimesema hapa kwamba katika jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei nzuri, nimeeleza mipango hapa ambayo sisemi kwamba inaandaliwa, nimesema imeshaanza kutekelezwa. Baadhi ya mipango ambayo imeshaanza kutekelezwa, kwa mfano, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Kongwa, Morogoro Vijijini, masoko yameshaandaliwa ili kuhakikisha kwamba wakulima hao wanakutana katika maeneo mamoja ili ushindani uwe wa haki na wa wazi. Kwa misingi hiyo hiyo ndiyo maana nimesisitiza hapa katika jibu la msingi kwamba kule Wilaya ya Iramba ambako tunategemea kwamba soko la Iguguno litaandaliwa, basi utaratibu huo unaweza kuwasaidia wakulima kuweza kuepukana na bei za chini. Lakini ninaongeza nikasema kwamba jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba tunatafuta njia ya kusindika mazao yetu ili kuyaongezea ubora na thamani ili bei iwe mzuri zaidi.

**Na. 61**

**Malipo ya Pension kwa Mashirika ya *PPF/NSSF***

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali haiwezi kuwahakikishia wala kuwapatia ajira wananchi wote nchini na kwamba inawahamasisha wananchi wake kujitegemea na kuwa wabunifu na kutumia maarifa ya kujiajiri wenyewe na kwa kuwa sheria zilizopo sasa za *PPF/NSSF* zinakataa na kumnyima mwananchi huyo kupewa pensheni yake kama bado hajatimiza umri wa kustaafu wa miaka 60 (kwa maana kwamba mwananchi huyo akiachishwa kazi kwa mfano akiwa na umri wa miaka 49 itabidi asubiri miaka 11 zaidi kama hakuajiriwa tena) ndipo apate pensheni yake hali ambayo inamnyima nafasi na haki yake ya kuitumia hiyo pensheni yake kujiendeleza au kujiajiri yeye mwenyewe katika kusomesha watoto wake au kufanya biashara na kadhalika:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba inajichanganya yenyewe kwanza kwa kumhamasisha huyu mwananchi kujiajiri na kujitegemea kwa kutumia (akiba) pensheni aliyojiwekea na halafu Serikali hiyo hiyo kwa Sheria za *PPF* na *NSSF* kumnyima haki ya kuzitumia fedha zake mpaka baada ya miaka 11 iliyobaki ili kufikia umri wa kustaafu na pili, Serikali inamkatisha tamaa huyo Mwananchi kwamba baada ya hiyo hamasa ya Serikali sasa hawezi kuzipata hizo fedha?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Bungeni Sheria hizo za *PPF* na *NSSF* zinazohusu suala hilo ili zifanyiwe marekebisho kwa lengo la kumwondolea mwananchi huyo adha au kero inayoambatana na kasoro zilizopo katika sheria hizo kama zilivyojitokeza?

(c) Kwa kuwa, *life expectancy* ya Mtanzania imeshuka kufikia miaka 47 jambo ambalo ni dhahiri kuwa mwananchi inawezekana asiweze kuishi kufikia miaka 60 na hivyo kukosa kufaidi pensheni yake, je, Serikali haioni busara kumpa Mwananchi huyo *option* ya kuchukua haki yake hapo anapoachishwa kazi kabla ya umri wa kustaafu?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, naomba nitoe maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* uliundwa kwa Sheria Na. 28 ya mwaka 1997 na Mfuko wa PPF uliundwa kwa Sheria Na. 14 ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 9 ya mwaka 2000.

Madhumuni ya kuanzishwa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na ule wa *LAPF*, ni kuwapatia wanachama kipato kilichotokana na majanga ya uzee, ulemavu, kifo, ugonjwa na kadhalika. Kwa hiyo mifuko hii inalenga kuwasaidia wanachama kutokana na malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Peter Kabisa, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwemo ya *NSSF* na *PPF* inaendeshwa kwa kufuata misingi ya Bima ya Jamii. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali haijichanganyi, bali inachofanya ni kutekeleza Sera zake sahihi zilizobuniwa na kukubaliwa na wadau wa Sekta hii. Aidha, Serikali inatambua tatizo la kutoeleweka vizuri kwa dhana ya Hifadhi ya Jamii. Kwa kutambua hilo Serikali inaandaa utaratibu na kutekeleza yafuatayo:-

- Kuitangaza Sera ya Hifadhi ya Jamii na kuielimisha jamii juu ya dhana nzima ya Hifadhi ya Jamii.

- Serikali inaangalia uwezekano na kuingiza dhana hii katika muhtasari wa elimu katika ngazi mbalimbali.

Kwa kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipo kwa ajili ya kutoa kinga kutokana na majanga niliyoyaeleza (kustaafu, ugonjwa, ulemavu na kadhalika) zipo Taasisi nyingine kama Mabenki ambayo pia yanaweza sambamba na mifuko hiyo kutoa mikopo mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika kujiletea maendeleo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Hifadhi ya Jamii, Serikali imekwishaanza kuandaa Sheria mama ya Hifadhi ya Jamii. Sheria hii itajumuisha marekebisho ya Sheria za Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwemo *NSSF* na *PPF*.

(c) *Life Expectancy* ni takwimu iliyoandaliwa kwa kuzingatia makundi yote ya kijamii katika Tanzania kutoka katika mazingira tofauti tofauti kwa mfano watoto wanaozaliwa katika mazingira magumu na kadhalika. Lakini *Life Expectancy* kwa watu waliofikia umri wa kustaafu ni tofauti na wastani wa nchi nzima. Aidha, pia napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge ya kuwa sio wafanyakazi wote wataugua magonjwa haya ya kisasa na hivyo kuishi umri mfupi. *(Kicheko)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri majibu yake mazuri. Lakini naona bado sijapata maelezo sahihi kuhusu mwananchi ambaye anakuwa hana nafasi ya kupata kazi nyingine na anaachishwa kazi na akiachishwa kazi ule Mfuko wake unakuwa unawekwa mahali ambapo hawezi kufikia mpaka afike umri wa kustaafu: Je, Serikali inaweza kurekebisha Sheria hii ili imruhusu mwananchi huyu ili aweze kupata fedha zake mapema afanye vitu vyake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Kabisa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa naeleza wakati najibu swali la msingi, kwamba madhumuni ya Mifuko ya Jamii vigezo vyake vikuu ni viwili. Moja, ni muda wa uchangiaji katika Mfuko huo. Lakini kigezo cha pili, ni umri wa kufikia kupata hiyo pensheni. Sasa tukileta marekebisho hayo hapa kama anavyopendekeza Mheshimiwa Peter Kabisa, mambo mawili yanaweza yakajitokeza. Moja, mtu huyu anaweza akanufaika kwa kiasi kidogo sana kwa sababu atakuwa amechangia kwa muda mfupi. Tukichukulia umri ambao Mtanzania anamaliza Elimu ya Juu, kuna hatari mtu huyu akafanya kazi labda kwa miaka kumi akataka apate pensheni kwa miaka ishirini na tisa jambo ambalo haliwezekani.

Pili, madhumuni ya Mfuko huu ni tofauti na madhumuni ya mikopo kama ya Benki. Mfuko huu unalenga kusaidia umri na hii ndivyo ilivyo kwa dunia nzima siyo Tanzania tu. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni Bima ya Kijamii. Kwa hiyo, lengo lake ni kumsaidia mtu anapokuwa mzee kupata majanga kama vile ya kifo, ugonjwa na kadhalika. Ndio maana mtu akiumwa hata kama bado yuko kazini bado Mfuko huu wa *NSSF* unaweza ukamsaidia matibabu na hata mama anayekwenda kujifungua bado anapata msaada huu. Lakini kwa mikopo ya kujengea nyumba, kusomeshea watoto

nafikiri tungetumia Benki. Kwa maana hiyo, Serikali haifikirii kuleta marekebisho ya Sheria kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. *(Kicheko)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mifuko hii ya *PPF* na *NSSF* wanafanya biashara kama vile ya majumba; Je, kuna gawiwo lolote ambalo wanapewa wateja wa Mfuko huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Ni kweli kwamba Mashirika haya yanafanya biashara ili kuzifanya zile fedha ziweze kuwa na maana. Maana fedha inayokaa tu bila kutumika athari yake ni kubwa sana sote tunaifahamu. Lakini hawa wanachama wananufaika zaidi ingawa siyo moja kwa moja, mtu anatoa asilimia kumi anachangiwa na mwajiri wake asilimia kumi. Kwa Sheria ya *PPF* kwa mfano anapofikia umri wa kustaafu anapata asilimia ishirini na tano ya mkupuo halafu anaendelea kulipwa kila mwezi mpaka mwisho wa uhai wake. Ina maana analipwa zaidi kuliko vile alivyopata. Kama sikufanyia biashara pesa hizi zisingepatikana fedha za kumlipa mtu kwa umri wake wote. Kwa hivyo wananufaika siyo moja kwa moja lakini kwa kupitia mafao wanayoyapata.

**Na. 62**

**Usajili wa Wachezaji katika Timu za Mpira wa Miguu**

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA (k.n.y MHE. FRANK G. MAGHOBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni kumekuwepo na malumbano ya usajili wa wachezaji wa mpira wa miguu kati ya timu za kiraia na timu za Magereza, ambapo timu ya Magereza ikitaka kusajili mchezaji yeyote kutoka kwenye timu za kiraia inakuwa rahisi kumsajili, lakini timu za kiraia zinapotaka kumsajili mchezaji toka timu ya Magereza huwazuia wachezaji wake kwa kutumia Sheria ya Magereza yaani *Prison Act* ya mwaka 1970 wakidai kuwa wao ni Askari hivyo hawaruhisiwi na timu za kiraia na hivyo kuwafungulia mashtaka Mahakamani:-

(a) Je, timu ya Magereza inaposajili mchezaji toka timu ya kiraia huwa inatumia Sheria iliyoanzisha Idara ya Magereza *(Prison Act. 1970)*?

(b) Je, ni Sheria gani inayosimamia masuala ya usajili wa wachezaji na panapotokea mgogoro wa Sheria ni ipi itakayo *prevail*?

(c) Je, Sheria ya Magereza inacho kipengele kinachoeleza kuwa mpira wa miguu utakuwa sehemu ya kazi ya Idara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Frank Maghoba, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tusichanganye Sheria na ajira za Askari na Kanuni za Usajili wa Wachezaji. Askari anaajiriwa katika Utumishi kama Askari kwa kazi ya uaskari na kwa masharti ya uaskari kwa mujibu wa Sheria ya Bunge iliyoidhinisha kuundwa kwa Jeshi husika. Katika suala hili, Sheria ya Magereza yaani *Prison Act* ya mwaka 1970 ndiyo inayomwajiri kazi Askari wa Magereza. Kwa hiyo, Askari yeyote wa Magereza ni lazima atii Mkataba wake wa Ajira. Hata kama ni mchezaji wa mpira wa miguu anapaswa kujua kuwa ana Mkataba wa Ajira. Usajili wa kujiunga na Klabu ya Mpira wa Miguu hauwezi na wala haupaswi kusimamia badala ya Sheria ya Ajira iliyoidhinishwa na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuwasaidie vijana hawa kufuata Sheria tulizozitunga ili wawe raia bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kujibu swali la Mheshimwa Maghoba, kama ifuatavyo:-

(a) Tume ya Magereza inapomsajili mchezaji kutoka timu ya kiraia inatumia Sheria iliyoanzisha Jeshi la Magereza kwa sababu kabla mchezaji hajasajiliwa kwenye timu ya *Tanzania Prisons Sports Club* ni lazima kwanza awe ni Askari Magereza. Askari Magereza hufanya kazi kwa Mkataba wa miaka mitatu mitatu na hauruhusiwi kuvunja Mkataba huo bila idhini ya mwajiri wake. Kwa hiyo Askari Magereza ambaye pia ni mchezaji wa *Tanzania Prisons Sports Club* haruhusiwi kuhamia timu nyingine kabla hajamaliza Mkataba wake wa Uaskari.

(b) Hakuna Sheria inayosimamia usajili wa wachezaji wa mpira wa miguu bali kuna Kanuni za *TFF* za usajili wa wachezaji wa mpira wa miguu Tanzania. Kwa hiyo haiwezekani kuwa na mgongano kati ya Sheria iliyopitishwa na Bunge kuhusu ajira ya Askari Magereza na Kanuni za *TFF* kuhusu usajili wa wachezaji. Tatizo linatokea wakati mchezaji ambaye pia ni Askari anapoamua kuhamia Klabu ya uraiani bila kujali Mkataba wake wa ajira uliundwa na Sheria iliyoanzisha Jeshi. Hapa siyo mgongano bali ni uhalifu wa Askari ambaye pia ni mchezaji wa mpira wa miguu aliyekiuka Sheria halali za Jamhuri ya Muungano kwa kutoroka kazini.

(c) Ukakamavu ni hitaji la msingi la uaskari. Njia pekee ya kuleta ukakamavu ni mazoezi ya viungo na michezo, mpira wa miguu ukiwa miongoni mwa michezo hiyo. Hakuna hata Mtanzania mmoja tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge anayetaka hata kufikiria licha ya kuona Jeshi letu likiwa legelege. Kwa hiyo, Askari wote lazima wafanye mazoezi ya viungo na michezo na ili ujue ubavu wako ni lazima ushindane. Kwa mujibu wa Kanuni za *TFF*, ili uweze kushindana ni lazima usajiliwe. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, katika maelezo yake ameeleza kuwa msingi wa

matatizo haya yanayojitokeza ya uaskari kwenda katika timu za mitaani yanavunja miiko ya kazi yao; Je, haoni wakati umefika wa kufanya marekebisho ya hiyo Sheria ili hawa walinzi wakapata fursa ya kukuza vipaji vyao kwa kujiunga na timu kubwa ili waliendeleze Taifa letu?

Pili; Askari hawa wanapokuwa katika shughuli ili timu yao iende vizuri wanakuwa wakichangia kwa hiari au kwa namna yoyote ambayo imeandaliwa na Jeshi. Siyo hawa tu, lakini kwa kweli ni walinzi wa vikosi vingi wanapaswa kuchangia timu zao; Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anayo habari kuwa kuna manung'uniko juu ya suala hili? Kama anayo, watafanya nini ili kuondoa usumbufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kama kuna sababu ya kubadilisha Sheria za Ajira za Askari Magereza eti tu mchezaji wa Magereza au wa Polisi, Jeshi aweze kwenda kuchezea timu ya kiraia kwa matarajio kwamba anakwenda kukuza kipaji. Kujiunga na timu yoyote ni suala la hiari. Kwa hiyo mtu anapoamua kuhiari mwenyewe kwenda kujiunga na timu ya Jeshi anafahamu mwenyewe kabisa kwamba ana hiari na kutii Sheria za ajira ya Jeshi husika. Kwa hiyo ni suala la yeye kuchagua tu aende kwenye timu ya kiraia ambapo anaweza kutoka muda wowote akijisikia au kwenda Jeshini ambako anakutana na Mkataba wa Ajira. Ningeomba vijana wawe makini katika hili kwa sababu *TFF* ya sasa haitavumilia vurumai za aina hii.

La pili, ni kweli Askari huchangia timu zao. Kama kuna manung'niko, najua tabia ya manung'niko ni mambo ya chinichini hayasikiki ndio maana ya kunung'unika. Unatakiwa uwe na sikio lenye nguvu kweli kweli kusikia manung'uniko. Lakini unapochangia chako hata kama kutoa kunauma nafikiri unatimiza wajibu wako. Ndio maana hata sisi Wabunge humu ndani huchangia Vyama vyetu vya Siasa. Sasa inawezekana unatoa kwa shingo upande lakini ni wajibu wako. Maana chako ni chako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, swali hili linailenga moja kwa moja timu yangu ya T*he Tanzania Prisons*, ningependa nijue hawa wachezaji wangu Nsajigwa na Ivo Mapunda waliotoroka kwenda *Moro United* kwa Sheria hii; Je, Serikali inanisaidiaje kuwarudisha ili waimarishe timu ya *Prison*? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hatuwashitaki kwa kwenda *Moro United,* lakini tunawashitaki kwa kutoroka Jeshi na leo wanafikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

**Na. 63**

**Watuhumiwa Kujeruhiwa Wakiwa Mikononi mwa Polisi**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na matukio kadhaa ya baadhi ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali kupoteza maisha au kupata ulemavu wakati wakishikiliwa na Polisi kituoni:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wamekufa au kupata ulemavu wakati wakishikiliwa na Polisi katika Vituo mbalimbali vya Polisi nchini kuanzia mwaka 1990 hadi sasa?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na matukio kadhaa ya baadhi ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali kupoteza maisha au kupata ulemavu wakati wameshikiliwa na Polisi Vituoni. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1990 hadi sasa jumla ya wananchi 36 wamefariki na sita wamepata ulemavu wakati wakishikiliwa na Polisi katika Vituo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, vifo na ulemavu huo umewapata watuhumiwa hao wakiwa katika Vituo vya Polisi kutokana na ama maradhi au kwa kutohudumiwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria. Ili kuweza kuhakikisha kuwa hali hiyo inadhibitiwa, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kutoa elimu kwa Askari na kuwakumbusha Askari katika Mabaraza juu ya wajibu wao wa kufanya kazi kwa kuzingatia Kanuni za Jeshi la Polisi hasa (*PGO*)No.353 inayomtaka kila Askari kuzingatia haya yafuatayo anaposhughulikia watuhumiwa;

* Kuweka kumbukumbu sahihi za watuhumiwa na kukagua mahabusu kila baada ya saa moja na kusikiliza shida zao mbalimbali pamoja na za kiafya na kushughulikia kwa haraka kabla shida hizo hazijaleta madhara makubwa kwa watuhumiwa.

* Kuwaweka mahabusu wa kike peke yao na wa kiume peke yao.

* Vile vile wanatakiwa kutotumia nguvu kupita kiasi wakati wa kuwakamata wahalifu.

(ii) Kuhakikisha kuwa Askari wazembe na uzembe wao kusababisha vifo au ulemavu kwa mahabusu wanachukuliwa hatua ya kushtakiwa kijeshi na kufukuzwa kazi

wakipatikana na hatia kwa kosa la kinidamu na hatimaye wanafikishwa Mahakamani kujibu mashitaka ya kosa la jinai.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; Je, utakubaliana na mimi kwamba kutokana na majibu yako...

**SPIKA:** Hapana! Mimi sijakujibu, siyo majibu yangu. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN C. KIGWELILO:** Serikali inakiuka Haki za Binadamu; Je, imetolewa fidia kwa wote walioathirika au kwa ndugu wa Marehemu kutokana na matukio mbalimbali aliyokuwa ameyataja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali wawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba baadhi ya vifo vinavyotokea katika Vituo vya Polisi vinasababishwa na maradhi. Watu wanaingia mle wana maradhi mbalimbali kisukari, *pressure* na kadhalika. Katika hali hiyo, nikiunganisha swali lake la pili, katika vifo kama hivyo hakuna fidia kwa sababu ni kifo tu kama kinavyotokea kama angekuwa nyumbani kwake. Lakini wakati mwingine Askari anayeshikilia mahabusu anaweza akawa mzembe na akasababisha mahabusu akapata madhara. Sasa ikithibitika hali kama hiyo, Askari kama hawa ndiyo niliosema kwamba kwanza wanashitakiwa Kijeshi, wanahukumiwa kwa kosa la kinidamu ya Kijeshi, lakini vile vile wanapelekwa Mahakamani. Sasa Mahakama ikimtia hatiani katika hukumu hiyo, Mahakama ikiona inafaa inaweza ikaweka na kipengele cha fidia. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kuwa, uko ushahidi wa kuonyesha kwamba katika kurahisisha kazi yao ya uchunguzi, Askari wanawatesa baadhi ya mahabusu wakiwa katika uchunguzi kwa kuwapiga, kuwafanya wakae muda mrefu bila ya kulala wala kula chakula na kwa kuwa, pia uko ushahidi kwamba, mahabusu za Polisi mara nyingi zimejaa sana na hivyo kusababisha upungufu wa hewa na matatizo mengine:-

Je, Serikali iko tayari sasa kuamua kutunga Sheria rasmi juu ya fidia ya watu au mahabusu wanaokufa wakiwa katika uchunguzi wa Polisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Askari kuwatesa watuhumiwa, wanapowafanyia *interrogation*, hili kwanza halipo katika utaratibu na sasa hivi katika mitaala ya ya masomo ya Askari Polisi tumeingiza vile vile na somo la Haki za Binadamu. Kwa hiyo kuanzia kwenye mafunzo yao tunawafundisha habari ya haki za binadamu. Habari ya kufanya uchunguzi kwa mateso ni mambo ya historia, sasa hivi haitakiwi. Tukipata ushahidi ni hawa ndio ambao

sasa tunawashtaki kijeshi na baadaye tunawapeleka Mahakamani kwa sababu wamevunja maadili ya kazi aliyofundishwa.

Kuhusu kutunga Sheria ya Fidia kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, hata sasa hivi Askari kama huyu akipelekwa Mahakamani Hakimu akimtia hatiani katika hukumu, Hakimu akiona inafaa anaweza akaweka suala la fidia. Sasa kama Waheshimiwa Wabunge mtaona hilo halitoshi, mnataka Sheria rasmi, basi nyinyi ndiyo watunga Sheria mnaweza mkaleta mapendekezo na yakafikiriwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY J. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa amekubaliana kwamba maradhi ni sababu mojawapo inayowafanya wafungwa kufariki katika mahabusu; Je, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba katika mahabusu zetu hamna vyoo na wafungwa wanatumia madebe au ndoo ambazo mara nyingi zinafurika na zinapofurika, basi ndivyo wanavyoambukizana maradhi ya kuambukizana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna maradhi mbalimbali yanayowapata watuhumiwa katika Vituo vya Polisi. Kuhusu suala la mazingira ya mahabusu ili yawe na vyoo, kwa kweli ndio utaratibu sasa hivi kila Kituo cha Polisi ambacho kinajengwa, moja ya matarajio muhimu ni lazima kuwa na vyoo.

Hata baadhi ya Vituo baadhi ya Wabunge wanalalamika kwamba Kituo kimekamilika hatujapeleka Polisi. Moja ya sababu ambayo tunasita kufungua Vituo ni kama bado Kituo hakina choo, hatuwezi kuruhusu kikafunguliwa. Kwa hiyo hitaji la choo kwa sasa hivi ni muhimu kabisa katika Kituo chochote cha Polisi. Pale ambapo Vituo vya zamani havina vyoo sasa hivi tumetoa kipaumbele kwamba kila Kituo cha Polisi, mahabusu iwe na vyoo ili tupunguze maradhi haya kwa wenzetu ambao wanakumbwa na matatizo ya kukaa katika mahabusu ya Polisi. *(Makofi)*

**Na. 64**

**Adhabu kwa Wanaosimama Ndani ya Gari**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na matukio ya ajali za mara kwa mara ambazo husababishwa na uzembe na kujaza abiria kupita uwezo wa gari na pindi ajali zinapotokea mazingira hayo husababisha vifo na ulemavu mkubwa unaoleta umaskini zaidi kwa Taifa hili na wale wote waliozidi huwa wa kwanza kufa au kuvunjika baadhi ya vioungo na kwa kuwa hivi karibuni Serikali imepiga marufuku watu kusimama kwenye mabasi ya abiria kama vile daladala na mabasi ya safari ndefu mikoani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kutoa adhabu kali kama vile faini ya papo kwa hapo au kwenda jela pindi Askari wa Usalama barabarani anapolisimamisha gari?

(b) Je, kuna Sheria yoyote inayoruhusu wanafunzi kusimama ndani ya gari au kwa wale waendao mnadani kukaa juu ya mizigo yao wanayopeleka mnadani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usafirishaji Na. 1/1973 katika Vifungu Na. (10) na (28) inatamka wazi kuwa kila msafirishaji anatakiwa kuzingatia masharti ya leseni yake na kwamba mabasi ya abiria yanatakiwa kuzingatia ujazo wa gari (viti vilivyopo). Sheria hiyo inakataza abiria kuzidi na kusimama ndani ya mabasi kwa vile wao ndiyo huathirika zaidi ajali inapotokea. Ili kuwabana wamiliki wa magari na madereva, Serikali mara kwa mara huongeza viwango vya adhabu kwa anayekiuka Sheria za Usalama Barabarani. Adhabu zinazotolewa ni pamoja na faini ya papo kwa papo inayotozwa na Polisi na adhabu ya kifungo inayotolewa na Mahakama kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo Sheria ya Usafirishaji Na. 1/1973 na ile ya Usalama Barabarani Na. 30/1973, hakuna Sheria yoyote inayoruhusu wanafunzi kusimama ndani ya mabasi ya daladala au wananchi waendao Minadani kupanda malori na kukaa juu ya mizigo. Huu ni ukiukwaji wa Sheria za Usalama Barabarani.

Serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali pamoja na Sekta Binafsi kuboresha usafiri Mijini, hasa Dar es Salaam kwa lengo la kuondoa usumbufu wa wanafunzi na hata watu wazima kujazana mno kwenye daladala. Hatua kama hizi pia zitachukuliwa kuboresha usafiri Vijijini ili waendao minadani wasilazimike kuvunja Sheria kwa kukaa juu ya mizigo. Wakati hatua hizo zikiandaliwa, Madereva wa mabasi la malori wanatakiwa wakati wote wazingatie Sheria zilizopo na zinazotawala leseni zao.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hali halisi ya Tanzania Sheria ya Usalama Barabarani huvunjwa kila siku kwa abiria kujaza kupita kiasi kwenye mabasi, malori na daladala na Serikali inafahamu hali hii;

(a) Je, hii ina maana kwamba Serikali inaruhusu hali hii iendelee kutokea?

(b) Je, Serikali ina mipango gani mahususi ya kukabiliana na hali hii kabla ya yeye kuandaa mipango halisi ya kuzuia ajali hizo zisitokee? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la watu kujazana katika mabasi hasa kule Dar es Salaam na hata wanaopanda malori kwenda Minadani, Serikali haituruhusu. Lakini mazingira na hali ilivyo huku leo tukisema sasa tunapiga marufuku usafiri wa malori wakati hali halisi huko Vijijini tunajua mabasi hayapo, wananchi hawatatuelewa. Au pale Dar es Salaam kwa hali *population* ya Dar es Salaam iliyopo ya mabasi na vile vidaladala vilivyopo ukifanya vinginevyo utaleta vurugu.

Kwa hiyo tunasema kwamba kwa Dar es Salaam kwa mfano, kuna mpango ambao juzi ameutaja hapa Waziri wa Mawasiliano wa mabasi makubwa *BRT* ambao wakati wowote mwaka huu utaanza. Yale mabasi makubwa yanachukua zaidi ya watu 160 basi moja, yatatengenezewa *line* yake maalum na yanakwenda kwa haraka. Kwa hiyo watu watakaa vizuri huu mpango ukikamilika wakati wowote mwaka huu, kwa Dar es Salaam tatizo litakuwa limekwisha.

Kwa Vijijini Serikali na nyinyi mashahidi tutafanya juhudi kubwa kuboresha barabara za Vijijini. Jinsi barabara vinavyoboreka Vijijini wenye mabasi watapeleka Vijijini, kwa hiyo mtu hataacha basi apande kwenye lori apate vumbi, anyeshewe na mvua. Nyinyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi katika Majimbo yetu kuna sehemu ambazo zamani magari yalikuwa hayapiti kwa sababu barabara zilikuwa mbovu, sasa zimetengenezwa mabasi yanapita. Programu ya barabara ikikamilika, mabasi yatakuwa mengi Vijijini na habari ya kupanda kwenye malori nayo itakwisha. **MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwa kuwa mabasi ya daladala yanachangia kwa kiasi kikubwa sana ajali na kwa kuwa ni sheria kwa kila mwenye basi la daladala awe na Bima ya *Comprehensive* itakayomwezesha kulifanyia matengenezo gari analoligonga; kwa vile utekelezaji wa hiki kitu haufanyiki; Je, Serikali ipo kumbana Mwaibula ili ahakikishe kwamba mabasi yote ya daladala yawe na Bima ya *Comprehensive* kwa ajili ya kutengeneza magari wanayogonga?

**NAIBU WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Sheria inamtaka kila mwenye basi kuwa na Bima kubwa yaani *comprehensive*. Sasa ile Bima kubwa inamwezesha kwanza kulipa fidia wale wanaoumia kama yeye akisababisha hiyo ajali, vile vile Bima kubwa maana yake inamwezesha atengeneze kwa Bima yake gari alililoligonga, ikithibitika kwamba yeye ndio aliyegonga na huo ndio utaratibu. Kama sasa Mheshimiwa Mbunge anasema utaratibu haufuatwi, basi tutawasiliana na Mamlaka za Leseni ile la Kitaifa na zile za Mikoa kuhakikisha kwamba Sheria inasimamiwa kila mwenye basi la abiria awe na Bima ambayo ni Bima kubwa yaani *comprehensive insurance.*

**Na. 65**

**Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetamka mara kwa mara kwamba upo mpango mkubwa wa Kitaifa wa kuanzisha kilimo cha kisasa cha umwagiliaji nchini badala ya kilimo cha kutegemea mvua na kwa kuwa Wilaya ya Kyela ina mbuga nzuri ambazo zinafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya mito yote, Songwe, Kiwira, Mbaka na Lufiyo:-

(a) Je, Wilaya ya Kyela itaanza lini kufaidika na mpango huo wa Kitaifa wa Kilimo cha Umwagialiji?

(b) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa juu ya Kilimo cha Umwagiliaji katika Wilaya ya Kyela? Kama upo, ni nini matokeo ya utafiti huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) ningependa kutoa maelezo mafupi ya utangulizi yafuatayo:-

Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na *JICA*, ilikamilisha maandalizi ya Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani katika mwaka wa 2004. Mpango huo haukusudiwi kuwa badala ya kilimo cha kutegemea mvua bali unategemea kusaidiana na kilimo kinachotegemea mvua ili kuboresha na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula nchini. Bila mvua hata kilimo cha umwagiliaji hakiwezekani.

Baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakipesile, kama ifuatavyo:-

(a) Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani ulibaini kuwa Wilaya ya Kyela ina eneo la hekta 9,970 zinazofaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maji ikiwemo mito ya Songwe, Kiwira na Lufiyo.

Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Umwagiliaji Maji Mashambani katika Wilaya ya Kyela, ulianza mwaka wa 2003/2004 ambapo *scheme* ya Ngana yenye ukubwa wa hekta 600 ilitekelezwa kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (*DADPs*) na *scheme* ya Ikumbilo yenye hekta 500 ilitekelezwa kwa kutumia fedha za *TASAF*. Aidha, *scheme* ya Kabanga yenye hekta 3,000 imefanyiwa upembuzi kwa msaada wa *Nordic Development Fund* na utekelezaji utaanza mara tu fedha za uendelezaji Mto Songwe zitakapopatikana.

(b) Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilifanya utafiti katika Wilaya ya Kyela uliohusu Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Utafiti huo ulizingatia kiasi na ubora wa maji yaliyopo, ardhi na matumizi yake, masuala ya kijamii na uchumi, mazingira, idadi ya watu na mawasiliano na uchukuzi. Utafiti huo umeonyesha kuwapo kwa jumla ya hekta 12,970 zinazofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Ikama hekta 1,000, Ikumbilo hekta 500, Kanga hekta 220, Songwe hekta 300, Lusanjo hekta 550, Ngana hekta 600, Nsesi hekta 6,000, Tenende hekta 500 na Kabanga hekta 3,000.

Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha ujenzi miradi ambayo imeanza kutekelezwa na kujenga miradi mipya.

**Na. 66**

**Upungufu wa Mabwana Shamba**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, muda wote kilimo kimekuwa Sekta Kiongozi kwa uchumi wa nchi yetu na kwa kuwa katika miaka ya 1990 - 2000 Serikali ilisitisha kufundisha wataalamu wa Kilimo (Mabwana Shamba) katika Vyuo vyake vya Kilimo:-

(a) Je, kwa sasa kuna upungufu wa Mabwana Shamba wangapi katika Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Nzega?

(b) Kwa kuwa sasa hatufundishi wataalam wa aina hiyo; Je, hao waliopo wakistaafu wakulima watahudumiwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, napenda kutoa maelezo machache ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Serikali haijawahi kusitisha kufundisha wataalam wa kilimo kwenye Vyuo vyake, bali imeendelea kuvitumia Vyuo hivyo kutoa mafunzo kwa Watumishi walioko kazini *(In-service trainees),* wanafunzi watalajali *(Pre-service trainees)* waliogharamiwa na Serikali na waliojigharamia wenyewe na wakulima. Kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2004 jumla ya wataalam 5,279 walihitimu mafunzo katika Vyuo mbalimbali vya Kilimo. Kati yao 1,901 walihitimu mafunzo ya Stashahada kwa ufadhili wa Sekta Binafsi. Wataalam 3,378 walihitimu mafunzo ya Stashahada za Kilimo kwa ufadhili wa Serikali. Aidha, wataalam 1,602 walihitimu mafunzo ya shahada katika fani mbali mbali za kilimo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Lengo la Serikali ni kuwa na Afisa Ugani mmoja kwa kila Kata. Mkoa wa Tabora una jumla ya Kata 138 na una Maafisa Ugani wapatao 257. Idadi hii kimkoa ni

kubwa ikilinganishwa na mahitaji halisi ya wataalam hao. Hivyo Mkoa wa Tabora una ziada ya Afisa Ugani 119. Maafisa Ugani walioko katika Mkoa wa Tabora wanatosheleza kuwahudumia wakulima 774,772 Mkoani humo.

Wilaya ya Nzega yenye jumla ya Kata 37 ina jumla ya Maafisa Ugani 66. Ukiainisha huduma ya Afisa Ugani mmoja kwa kila Kata, Wilaya ya Nzega ina ziada ya Maafisa Ugani 29. Mahitaji ya Maafisa Ugani katika Wilaya ya Nzega ni 37 ambao wanatosheleza kuwahudumia wakulima 183,704 kwa Wilaya hiyo.

Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kwamba Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Nzega hazina upungufu wa Maafisa Ugani na Wizara ya Kilimo na Chakula inashauri Mikoa na Halmashauri za Wilaya kufuata utaratibu wa mgawanyo wa Maafisa Ugani kwa kuzingatia kila Kata kuwa na Afisa Ugani mmoja.

(b) Endapo wataalam wastaafu hapatakuwa na upungufu wowote kwa kuwa Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya kilimo. Hivyo, Halmashauri za Wilaya zinashauriwa kutenga fedha kwa kuajiri wataalam wapya watakaoziba nafasi zitakazoachwa wazi na wastaafu. Mbali na kustaafu, upungufu wa wataalam utakaojitokeza aidha kwa kufariki, kuacha au kuachishwa kazi utaendelea kuzibwa kwa kufuata taratibu na Kanuni za ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri ambazo ziliomba na kukubaliwa kuajiri Maafisa Ugani kwa mwaka 2002/2003. Baadhi ya Halmashauri hizo ni Handeni watano, Ulanga wawili, Biharamulo mmoja, Kibondo mmoja, Nkasi mmoja, Sumbawanga wanne, Songea Vijijini mmoja, Mkuranga mmoja, Makete watatu Moshi Vijijini watatu na Manispaa ya Ilala mmoja.

**MHE. LUCAS L. SELEII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nina maswali madogo sana mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wizara ya Kilimo kama alivyoeleza pale mwanzo ni Sekta Kiongozi na kwa kuwa kinaajiri watu wengi nchini na mafunzo yaliyopo sasa hivi kwenye Vyuo wanafunzi wanajilipia;Je, Serikali haioni ikafanya makusudi kama ilivyofanya kwa wanafunzi wanaosomea elimu ikawasomesha kwa pesa ya Serikali?

La pili, kwa takwimu hizi alizoonyesha Waziri wa Kilimo imeonyesha ukweli kuna Mabwana Shamba wengi sana hasa hata katika Wilaya ya Nzega, lakini mimi nimeuliza kuwa hawaoni kwa sababu kule shambani hawafikii; Je, Serikali ipo tayari kuweka mtaala wa kueleza kwamba Ofisi ya Bwana Shamba ni shambani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NACHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kilimo ni Sekta kiongozi lakini si Sekta peke yake inayotumia wataalam Vijijini, kwa hiyo hatuwezi kuongeza idadi yao bila kufikiria kwanza uwezo wa Serikali ya kuwahudumia hao waliopo na katika Sekta nyingine mbali mbali. Hii ndio maana ikawekewa *formula* au utaratibu wa kuwa mtumishi mmoja kwa Kata moja na kama

hatasimamiwa vizuri. Hiyo inawezekana, kwingineko imewezekana na naamini hata huko Nzega itawezekana.

Kuhusu Mabwana Shamba hawaonekani na kwa hiyo tuweke kwenye mtaala kuwa Ofisi yake ni shambani ni kweli nasema wanaweza kuonekana kama wakipangia utaratibu wa kusimamiwa. Hao Mafiasa Kilimo wa Ugani waliopo katika Wilaya wameajiriwa na Halmashauri na mkubwa wao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Tunaomba kutoa ushauri kuwa kupitia Halmashauri hao watumishi wahakikishe wana mipango ya kazi na ratiba za kazi ambazo nakala zake ziko maofisini katika Halmashauri kusudi mamlaka zote husika iwe Mkurugenzi mwenyewe, Mtendaji au sisi Waheshimiwa Madiwani tuweze kuwasimamia. Kwa kufanya hivyo hatuna haja ya kusisitiza madarasani kuwa mahala anapostahili Bwana Afisa Kilimo awepo Kijijini, itakuwa ni suala lisiloulizwa. Bwana shamba mahala pa kufanyia kazi ni Vijijini na sio Maofisini.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Wilaya nyingine zina Mabwana Shamba wa ziada wakati Wilaya nyingine hazina kwa sababu ya mazingira magumu mfano ikiwa ni Wilaya ya Makete; Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwapa motisha Maafisa wa Kilimo ili waweze kufanya kazi kwenye Wilaya za mazingira magumu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mazingira yote ya Vijijini kwa kawaida ni magumu. Sijawahi kuona Kijijini ambako hakuna tatizo kabisa. Mambo ni ya raha tupu, hakuna. Aidha, kwa kuzingatia hilo, niliomba Halmashauri zenyewe ziainishe ugumu huo na kupanga maslahi manono kusudi wabakie huko huko. *(Kicheko)*

**Na. 67**

**Tatizo la Kukatiwa kwa Mawasiliano ya Simu - Lindi**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO (k. n. y MHE. MOHAMED ABDULAZIZ)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na tatizo la mara kwa mara la kukatika kwa mawasiliano ya simu katika Mji wa Lindi:-

(a) Je, ni nini sababu za tatizo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali itashughulikia tatizo hilo na kuliondoa kabisa ili kuwaondolea kero wananchi wa Lindi na kwa Wilaya karibu zote za Mkoa wa Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge la Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lilikuwepo tatizo la kukatika kwa mawasiliano ya simu Mjini Lindi. Sababu kubwa ya tatizo hilo ni umeme usio madhubuti ambao kwa nyakati tofauti umesababisha kuharibika kwa mtambo wa simu wa *GX* 5000 uliopo Mjini Lindi.

Pia, kulikuwepo na tatizo la sehemu ya mitambo ya *VSAT* ya Mjini Mtwara kutofanya kazi inavyotakiwa. Mitambo ya *VSAT* huwezesha kupatikana simu nje ya Mikoa ya Mtwara na Lindi kupitia Kituo cha Satelaiti cha Mwenge.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matatizo haya, Kampuni ya Simu Tanzania itaendelea kuwasiliana na kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unapatikana huko Lindi jinsi inavyowezekana.

Matengenezo ya *VSAT* yalifanywa na vipuri vya ziada vimetumwa Mtwara. Mtambo mpya wa *digital microwave radio link* kati ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara unawekwa na mradi huu unategemewa ukamiliaka ifikapo mwezi wa Mei mwaka huu 2005. Mtambo wa *VSAT* utaondolewa mara baada ya kukamilika mtambo huo wa *digital microwave radio link*" kati ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kero kubwa ipo kwenye Kiwanja cha Ndege cha Lindi ambako hakuna mawasiliano kabisa pamoja na Ukanda unaozalisha korosho hasa kuanzia Mnazi Mmoja, Nyengedi, Mtama na Nyangawo; lini hasa Mheshimiwa Waziri atawahakikishia wananchi hawa kupata mawasiliano ya simu ili waweze kujumuika na wenzao duniani katika mtandao?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, mara tu tutakapomaliza *digital microwave link* ambayo hivi sasa inajengwa na itamaliza Mei, Masuala mengi ya simu tu kwa ukanda ule ikiwemo Ikwiriri, Utete na sehemu nyingine alizotaja Mheshimiwa Mbunge, zitapata mawasiliano.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona leo.

**SPIKA:** Alaa! *(Hapa Wabunge walipiga makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa katika jibu lake amesema mitambo iliyokuwa imewekwa ya *VSAT* ilikuwa inaharibika kutokana na tatizo la umeme na kwa kuwa sasa anaweka mitambo mingine; Je, hii mitambo haitaathirika na tatizo la umeme wa Lindi tatizo ambalo bado lipo na kama litaathirika, wana mpango gani Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha kwamba Mji wa Lindi na Mkoa wa Lindi unapata huduma sahihi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Maria Watondoha kwamba, katika Vituo vyetu vya simu tuna *backup system ya generators* ambazo zinafanya kazi. Lakini naelewa kwamba Wizara ya Nishati na Madini wanao mradi wa umeme wa Mnazi Bay ambao nina hakika hivi karibuni utaanza kufanya shughuli zake. Lakini mimi nasema tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Nishati na Madini kuhakikisha shughuli hizi zinafanikiwa ipasavyo.

**Na. 68**

**Mbia Katika Kampuni ya Simu *TTCL***

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2001 Serikali iliahidi Bungeni kwamba kupitia Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* itapeleka vibanda vya simu katika Miji na Vijiji vyenye wakazi zaidi ya 3000 kama vile Kakongwa, Segese, Bugarama, Kakola na vinginevyo nchini kote na kwamba, Serikali kwa kauli yake ya tarehe 2/11/2004 ikijibu swali la Mheshimiwa Janguo, Mbunge wa Kisarawe ilikiri kwamba, *TTCL* imeshindwa kufanya hivyo kutokana na matatizo ya kifedha na kwa kuwa Serikali ilitafuta mbia - *Strategic Investor* kwa madhumuni ya kuiboresha kampuni hiyo kiteknolojia na kifedha:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, mbia huyo alileta *financial proposal* za uongo kwa nia ya kushinda tenda hiyo hali akijua hana uwezo?

(b) Kama hakudanganya; Je ni vigezo gani vilitumika kumruhusu kuingia ubia huo au Serikali haikuzingatia kigezo muhimu cha uwezo wa kifedha wa mbia huyo?

(c) Kwa kuwa mipango yote ya *TTCL* kabla ya ubia huo ilisitishwa ili kutekeleza mpango mpya ulioletwa na mbia, zikiwemo mbwembwe za kupeleka simu katika Miji na Vijiji kama mlivyoeleza hapo juu na kwa kuwa mpango wake huo haukutekelezeka; Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya mbia huyo kwa kuwachelewesha Watanzania kupata huduma muhimu ya mawasiliano kwa miaka mimne sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, mpango wa awali wa Kampuni ya Simu Tanzania ulikuwa ni kupeleka simu Mijini na Vijiji vyenye wakazi zaidi ya 3,000 na pia kama tuliyomjibu Mheshimiwa Janguo, Mbunge wa Kisarawe hapo tarehe 2/11/2004, kwamba azma hiyo au mpango huo ulishindwa kutekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo tunategemea baada ya kupitisha mpango wa kuanzisha Mfuko maalum ujulikanao kama *Universal communication Fund*, tatizo hilo litapungua au litapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, tokea *TTCL* kubinafsishwa hadi leo mambo mengi tu yameshughulikiwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwenye *backbone* tumeweza kueneza mtandao wa *backbone* yenye *channel* 1900 na kubadilisha/kupanua *links* zifuatazo:-

- Dar es Salaam/Lugoba/Mnyusi
- Dar es Salaam/Lindi/Mtwara
- Mwanza/Nyama Nyama
- Dodoma/Singida/Tabora/Shinyanga/Mwanza na tunatarajia kazi hizi nyingi zitakuwa zimefikia upeo ifikapo Mei, 2005.

(b) Kwenye *transmission link* tumeweza kubadilisha *channels* 480.

(c) Kwenye *switches* waliweza kubadilisha zile *analogue* na kuweka *digital* kwenye Miji na maeneo mbalimbali nchini na *TTCL* imeweza kujenga vibanda vya simu 4,438 maeneo mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya mawasiliano imebadilika sana tangu mwaka 2001. Hivi sasa duniani simu za mkononi zinachukua nafasi kubwa katika masuala ya mawasiliano ulimwenguni na kufanya simu za kawaida kutumika kwa kiwango kidogo sana.

Mheshimiwaa Spika, hapa Tanzania sasa wateja wa simu za mkononi ni 2,100,000 wakiwepo wale wa *Celtel* 500,000; ukilinganisha na wateja 463,000 hapo awali. Wateja wa simu za kawaida walikuwa 88,000 tu mwaka 1995 na hivi sasa wako 150,000. Mtaona kwamba ongezeko sio kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Mawasiliano ya Simu, napenda nikiri kuwa Wizara imetekeleza vyema kwa kadri ilivyoweza, kupitia Kampuni na Makampuni ya Simu mbalimbali, ilani ya uchaguzi na naamini Waheshimiwa Wabunge, wengi ni mashahidi wa hilo. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Kipole na wananchi wake wote wa Msalala kwani Jimbo lake ni moja ya Majimbo ambayo tayari huduma hizo zimewafikia.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na maswali mawili ya nyongeza. Swali langu lilihusu vibanda katika Vijiji nilivyovitaja vya Kagongwa,

Segese, Bugarama na Kakola ambavyo viliahidiwa tangu mwaka 2001 kama nilivyosema na wananchi bado wanaendelea kusubiri. Sasa pengine Mheshimiwa Waziri atanipa kauli leo kwamba wananchi hao waendelee kusubiri mpaka lini haswa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, tunafahamu kwamba katika biashara yoyote mwenye hisa chache huwa na sauti ndogo lakini inavyoonekana kwenye Kampuni ya Simu mwenye hisa ndogo ndiyo mwenye sauti kubwa, kwa sababu mipango ya mwekezaji ndiyo inayosikilizwa kuliko ya mwenye *share* kubwa. Je, ni kwa nini huyu mwekezaji amepewa kipaumbele namna hiyo kuamua mambo yote kwenye *TTCL*. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulitoa ahadi ya kupeleka simu vibandani katika Vijiji vyenye watu 3,000 na ninakubaliana naye kwamba sehemu nyingine nyingi tu za Jimboni kwake bado hatujamfikia. Lakini napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania ni kubwa na kazi nyingi imefanyika na tunakwenda kwa awamu na nina hakika kama tumeweza kufikisha mawasiliano ya simu ya *Celtel* Jimboni kwake na mawasiliano mengine yatafika.

Mheshimiwa Spika, pili makubaliano ni makubaliano na kama tulikubaliana na masuala ya kibiashara kwamba huyu awe na kauli zaidi, huyu asiwe na kauli zaidi; lakini nataka nimwambie kauli zaidi pia ipo kwa wenye hisa ya Serikali na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mawasiliano ya simu ya *Celtel* yamefika maeneo mengi nchini. *Celtel* ni Kampuni tanzu ya *TTCL*.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua kwamba, kwa kuwa Serikali imesema wajenge Shule za Sekondari kila Kata na Mheshimiwa Waziri anaelewa kwamba ili kupeleka *Computer* pale, lazima kuwe na sehemu angalau za *landline* kwa Tanzania. Je, kitendo chao cha kukimbilia kupeleka hela kwenye *Celtel* na kuacha kupeleka hizo simu za *Landline* hajui kwamba kinatuhujumu zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, hata wenzetu wamesema Rome haikujenga kwa siku moja. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge tulipotoka na tulipo sasa kwenye masuala ya mawasiliano ya simu, yeye ni shahidi. Ilikuwa ukitaka simu kwa siku moja unakaa siku tatu unakorogewa hujapewa *line* ya kwenda, lakini leo Mheshimiwa Mutungirehi unaweza kuzungumza na wateja wako na Wapigakura wako ukiwa hapa Dodoma au ukiwa popote nje ya nchi. Kwa hivyo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mutungirehi kwamba na sisi tutafika huko ambako tunahitaji kufika katika mawasiliano. *(Makofi)*

**Na. 69**

**Elimu na Zana za Kisasa kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA (k.n.y. MHE. DR. AARON CHIDUO)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika uchimbaji wa madini, wachimbaji wadogo hawana zana za kisasa na elimu ya kutosha juu ya kazi hiyo na kwa kuwa, hakuna mfano ulio wazi wa soko la madini humu nchini na vile vile uhusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo sio wa kuridhisha:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata zana za kisasa na kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri kati ya hao wachimbaji wakubwa na wadogo, kwa lengo la kuwafanya wachimbaji wakubwa wawasaidie wachimbaji wadogo katika kupata zana za kisasa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani maalum za kuwawezesha wananchi kupata elimu ya kisasa juu ya madini na uchimbaji wake na hasa kuwaelekeza kwenye sehemu zenye madini na kuwapa elimu juu ya soko la ndani kwa madini hayo?

(c) Je, kuna ukweli gani kwamba katika Tarafa ya Nongwe kwenye milima ya Ukaguru Wilaya ya Kilosa kuna utajiri wa vito vya thamani ambavyo wananchi wa maeneo hayo hawajafaidika na utajiri huo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b), na kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kutathimini kuwepo kwa wachimbaji wadogo wa madini nchini. Wizara yangu imekuwa ikihakikisha kuwa wachimbaji hao wanaondokana na tatizo la kutumia zana duni za uchimbaji madini. Wizara pia imekuwa ikishirikiana na Shirika la viwanda nchini *(SIDO)* pamoja na Shirika la Madini nchini *(STAMICO)* katika kuwasaidia wachimbaji wadogo ili waweze kuboresha shughuli zao za uchimbaji. Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kutumia Taasisi yake ya *IPI* kimekuwa kikishirikiana na Wizara yangu kufanya utafiti wa vifaa mbalimbali vikiwemo vya uchimbaji kwa lengo la kuunda baadhi ya vifaa na mitambo ya uchimbaji hii ya wachimbaji wadogo wavipate kwa urahisi hapa hapa nchini na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa kupitia Wizara yangu imekuwa ikikaribisha Makampuni, Mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)*, watu binafsi na hata Taasisi mbali mbali za kifedha zinazoweza kusaidia kupatikana kwa vifaa vya uchimbaji madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Serikali pia imekuwa ikiwataka wachimbaji wakubwa na wadogo kuwa na uhusiano mzuri wakati wa kuendesha shughuli zao za uchimbaji. Uhusiano huo mzuri ndiyo unaowezesha wachimbaji hao kushirikiana na wachimbaji wakubwa ili kupata vifaa bora vya uchimbaji na utafutaji wa madini. Kwa mfano, kumekuwa na ushirikiano ambapo Makampuni makubwa yamekuwa yakifanya utafiti wa madini kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo kwa ushirikiano. Hali hii imewafanya wachimbaji

wadogo walioweza kushirikiana na Makampuni makubwa kupata mitaji ya kuweza kununua vifaa bora vya kuchimbia na pia kuweza kuazima vifaa vya uchimbaji mkubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi zake zilizopo Mikoani, imekuwa ikichukua hatua madhubuti ya kuwaelimisha wananchi kuhusu shughuli za madini. Juhudi hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara ya madini juu ya upatikanaji wa aina mbalimbali za madini na uchimbaji wake kwa kuendesha Semina na mafunzo mbalimbali ili kuwawezesha wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa madini kuendesha uchimbaji na biashara ya madini kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za madini katika hali iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mafunzo hayo, wachimbaji wamefundishwa Sheria ya Madini na Kanuni zake, taratibu na namna bora ya kutafuta na kuchimba madini, biashara ya madini, namna bora ya kuchimba madini, matumizi salama ya baruti na uhifadhi wa mazingira. Wizara yangu imeshatoa mafunzo hayo katika maeneo ya wachimbaji wadogo huko Londoni Mkoani Singida, Matundasi Mkoani Mbeya, Mererani Mkoani Arusha na katika Miji ya Morogoro na Tanga kwa ajili ya wachimbaji wa Mikoa hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika Tarafa ya Nongwe kwenye milima ya Ukaguru Wilaya Kilosa kuna utajiri wa madini ya vito. Kwa sasa madini ya vito yanayofahamika kuwepo katika eneo hilo ni pamoja na *rhodolite, amethyst, yellow scopolite, regamet, moonstone* na *purple scapolite.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imekwishatoa leseni nne za utafiti mkubwa wa madini ya vito katika maeneo hayo kwa Makampuni mawili ya Kitanzania ambayo ni *M/S Warthog Resources (T) Limited* yenye leseni tatu katika eneo hilo na *M/S Hydro-Geos Consulting Group (T) Limited* yenye leseni moja. Aidha, Wizara yangu imetoa leseni kumi za wachimbaji wadogo wa madini ya vito katika maeneo hayo ambazo zinamilikiwa na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi yake ya Mjini Morogoro imetembelea maeneo hayo mara kwa mara kwa lengo la kuelimisha wananchi kuhusu taratibu za kisheria za kumiliki na kuendesha utafiti na uchimbaji wa madini pamoja na kuhamasisha utafiti zaidi wa madini hayo ili hatimaye uchimbaji mkubwa na wa kisasa uweze kuanza kama ilivyo kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo mengi yanapogunduliwa madini wanaondolewa; Je, isingekuwa vizuri badala ya kuondolewa wawezeshwe kuyamiliki maeneo hayo ili wawekezaji wanapokuja waweze kushirikiana na wao?

(b) Kwa kuwa Sera yetu ya uwezeshaji wa nchi inatamka kwamba pale madini yatakapogundulika wananchi wataondolewa, isingekuwa vizuri ili iwe sera ya uwezeshaji kweli ikabadilishwa na ikasomeka pale madini yatakapogunduliwa wananchi watamilikishwa maeneo hayo ili wawe tayari kushirikiana na wale watakaokuja kuwekeza?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wachimbaji wadogo wadogo mara nyingi wakishagundua mahali ambapo pana madini wanakuja kwa wingi na wanachimba kiholela. Tungeweza kusema kiholela kwa sababu hapajapimwa, kunakuwa na kitu wanachoita *Gold rush* kama kule Muheza mwaka jana. Tunachofanya ni kwamba mara ikitokea hilo tunatuma wataalam wetu wanadhibiti uchimbaji huo ili kulinda mazingira na afya za wale ambao wanachimba pale.

Mheshimiwa Spika, tunaunda Kamati katika Wilaya ile, kama tunaona kwamba kuna madini ambayo ni endelevu, tunaunda Kamati na inawapa maeneo yale kwa sehemu ndogo ndogo ili waweze kuchimba kwa ufanisi zaidi na kwa kutambulika. Kwa hiyo tukiona kwa mfano Muheza sasa hivi hakuna madini tena yaliyobaki, basi tunafunga sehemu ile ili mazingira yasizidi kuharibiwa na vyanzo vya maji au misitu kuharibiwa kwa sababu wakuja kwa wingi sana.

Suala la pili, kuhusu sera yetu ni kwamba kukigunduliwa kwamba kuna madini mahali fulani, waliopo pale wanakuja kuomba leseni na anayeomba leseni kubwa ni lazima atambue wale wananchi waliopo sehemu ile, kama ni Kijiji au ni mtu binafsi kama wanachimba mmoja mmoja ni lazima watambuliwe na haki yao inalindwa kisheria. Hawaondolewi bila kupewa fidia kama wanataka kuondoka, kama wanataka kuendeleza kazi ya kuchimba, basi nao wanapewa leseni zao ili waweze kufanya kazi kwa kushirikiana. Mara nyingi wanaondolewa baada ya kulipwa *compensation* na baada ya kuwasiliana na wale wachimbaji wakubwa ambao wana ufanisi zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Beatus Magayane.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wa Kiti ili niweze kufahamu ni kitu gani kitatokea kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye kwenye Mkutano wa hadhara anatamka bayana kwamba yanayotendeka katika Bunge yanatia kichefuchefu. Au anapokuwa anahojiwa na Vyombo vya Habari anatamka kwamba katika kupitisha sheria kilichofanyika ni uhuni. Naomba mwongozo wako ni nini kifanyike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Beatus Magayane. Mwongozo upo. Mwongozo wa nini kifanyike kwa hakika hilo, uko wazi. Tunayo Kamati ya Bunge ambayo kazi

yake ni kuangalia maadili ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini nieleze vile vile kwamba hiyo Kamati ya maadili inafanya kazi sawa sawa na zinavyofanya Mahakama, kwamba Mahakama haiendi yenyewe kutafuta makosa ili ije iyasikilize. Mahakama lazima zipokee malalamiko kutoka kwa mlalamikaji au mshtaki yeyote na Kamati yetu inayosimamia maadili ya Wabunge halikadhalika inapokea malalamiko halafu inayafanyia kazi. Sasa wewe haukumtaja huyo Mbunge lakini ukipeleka malalamiko yako uliyoyatoa hapa Bungeni kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Wabunge yatashughulikiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya Vikao vya Kamati kwa leo, Kamati nne zimepangiwa kukutana. Kamati ya kwanza ni Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mwenyekiti, anaomba Wajumbe wake wakutane saa 7.30 mchana katika Ukumbi namba 227 ili kukutana na ujumbe wa Kampuni ambayo imeomba kukutana na Kamati hiyo.

Kamati ya pili ni ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wake anaomba Kamati hiyo ikutane saa 5.00 asubuhi hii kwenye Chumba cha Kamati Na.428 ghorofa ya nne. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(Public Accounts Committee)* Makamu Mwenyekiti wake Prof. David Mwakyusa anawaomba Wabunge wa Kamati hiyo wakutane katika Chumba Na. 219 kuanzia saa 5.00 asubuhi hii. Kamati ya mwisho ni ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC*, Mheshimiwa Mgana Msindai Mwenyekiti wake anaomba Wajumbe wa Kamati hii wakutane saa 5.00 asubuhi hii Chumba Na. 428. Hivyo ni Vikao vya Kamati za Bunge.

Sasa kuna Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wa CCM kuwa Kikao chao kilichokuwa kifanyike leo sasa kimeahirishwa mpaka kesho tarehe 9, saa 7.00 mchana Chumba Na. 231.

Mwisho nimeombwa na Mheshimiwa Athumani Janguo niwatambulishe wageni wake walioko kwenye *gallery* ambao wamekuja kuona jinsi Bunge linavyoendesha shughuli zake. Ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ambao wako hapa wote. *(Makofi)*

*(Hapa Wageni waliotajwa walisimama na kuonekana)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria inayoainisha Masuala ya Kiutawala na Kinidhamu ya Majaji Wasajili na Utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu ya Mahakama wa Mwaka 2005 *(The Judicial Service Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuifuta na kuiandika upya Sheria ya

Utumishi wa Mahakama *(The Judicial Service Act)* ya mwaka 2004 kama ilivyobadilishwa kwa mujibu wa orodha ya mabadiliko iliyoambatanishwa kwenye orodha ya shughuli za leo sasa isomwe kwa mara ya pili.

Awali ya yote napenda nitoe shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge hili ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kazi kubwa na nzuri waliyofanya ya kuuchambua Muswada huu. Muswada umeboreka kutokana na mchango waliotupa, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa, tangu miaka ya 1980 nchi yetu imekuwa ikiufanyia marekebishao mfumo wa uchumi wetu ili kuimarisha na kuondoa vikwazo vinavyozuia au kuchelewesha ukiukaji wake. Sekta ya Sheria ni moja ya Sekta muhimu katika jitihada hizo. Hata hivyo, ndani ya Sekta hususan katika Mahakama, yapo maeneo ambayo yamekuwa au yanaweza kuwa kikwazo kwa juhudi hizo.

Aidha, utendaji wa Mahakama umekuwa ukilalamikiwa sana katika jamii. Kwa sababu hizo zimekuwa zikiundwa Tume na Kamati mbalimbali kuyapitia matatizo hayo na kutoa mapendekezo.

Baadhi ya Tume na Kamati hizo ni Kamati ya Msekwa ya mwaka 1977, Tume ya Nyalali, Kamati ya Jaji Bomani, Tume ya Jaji Warioba iliyokuwa ikiangali suala la rushwa na Tume ya Jaji Kisanga. Aidha, ipo Kamati ya Jaji Mroso iliyoundwa na Jaji Mkuu. Mapendekezo katika Muswada ulio mbele yetu ni matokeo ya kazi za Tume na Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Majaji, tunalo tatizo la kutokuwepo chombo au utaratibu mzuri wa kushughulikia nidhamu na utendaji wa Majaji. Utaratibu pekee ni ule ulioainishwa katika Ibara ya 110 ya Katiba unaoelezea uwezekano wa Jaji kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi yake, ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya Jaji au Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 110(6) ya Katiba inaainisha kuwa iwapo Rais anaona kuwa suala la kumwondoa Jaji kazini linahitajika kuchunguzwa, basi ataunda Tume ambayo Mwenyekiti wake na angalau nusu ya Wajumbe watakuwa ni Majaji kutoka nchi nyingine za Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge hili tarehe 02 Februari, 2005 wakati nikiwasilisha Mapendekezo ya Mabadiliko ya 14 ya Katiba, utaratibu huu tutauendeleza. Hata hivyo utaratibu huo huanzishwa pale tu panapokuwa na tatizo au tuhuma inayoweza kusababisha kumwondoa Jaji kazini. Isitoshe haupo utaratibu maalum wa kupokea malalamiko yanayohusu Majaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika utaratibu wa sasa, Jaji Mkuu hana nguvu ya kutosha kisheria kusimamia utendaji kazi wa Majaji na kudhibiti kikamilifu nidhamu ya Majaji hao. Hali hii imekuwa chanzo cha matatizo na malalamiko ambayo Sheria inayopendekezwa inakusudia kuyarekebisha. Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeamua kufanya kuyafuatayo:-

(a) Kuainisha majukumu na wajibu wa Majaji.

(b) Kuiongezea majukumu Tume ya Utumishi wa Mahakama ili pia iweze kushauri kuhusu uteuzi na nidhamu ya Majaji.

(c) Kuainisha utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu Majaji ambao haupo kwa hivi sasa.

(d) Kuainisha utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu Majaji ambayo hayalengi kumvua madaraka Jaji mhusika. Kwa sasa haupo utaratibu wa namna hiyo. Madhumuni ya Muswada huu ni kumpa Jaji Mkuu uwezo Kisheria wa kumwonya Jaji yeyote atakayetenda vitendo vinavyokiuka maadili.

(e) Kuweka muda ambao baada ya kesi kusikilizwa hukumu itatakiwa kutolewa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo tunayotoa yana lengo la kuweka misingi ya kuimarisha asasi hii ya Mahakama ili ifanye kazi zake kwa ufanisi na kuwajibika kwa Taifa, wananchi na wateja wake.

Maudhui yaliyomo katika Sheria yatawapunguzia Majaji uhuru wa kujifanyia watakacho na hivyo kuwabana kiutendaji. Hata hivyo, hatua hizi hazitaingilia kwa namna yoyote uhuru wa Majaji kutoa maamuzi katika mashauri mbalimbali. Kuhusu suala muhimu la maslahi kama Katiba inavyoelekeza na kama ilivyo katika nchi nyingine tunakusudia kulitungia Sheria yake peke yake.

Mheshimiwa Spika, hayo tuliyoyakusudia yangeweza kufanyika ama kwa kuandika Sheria mpya au kuyajumuisha katika Sheria iliyopo. Serikali imeamua kuyajumuisha katika Sheria iliyokuwepo ikishughulikia ajira, nidhamu na mambo mengineyo kuwahusu Mahakimu. Kwa kuwa mambo yanayoongezewa ni mengi na pia baadhi ya yale ambayo yapo katika Sheria hiyo yatahitaji kufanyiwa marekebisho, imeamuliwa kuwa Sheria hiyo ifutwe na kuandikwa upya.

Mheshimiwa Spika, Muswada una sehemu nne. Sehemu ya kwanza inajumuisha kifungu cha kwanza hadi cha tatu, kinahusu mambo ya kiutangulizi kama vile jina la Sheria, kutumika kwake na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria. Sehemu ya pili inajumuisha vifungu vya nne hadi sita, inaziainisha zaidi kazi za Jaji Mkuu na kumpatia meno akiwa Mkuu wa Mahakama. Jaji Mkuu sasa anaweza kuwataka Majaji kumpatia taarifa ya kesi walizoziendesha, kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu ucheleweshaji wa kesi na kuchukua hatua yeyote ili kudhibiti matatizo atakayoona.

Kwa malalamiko mazito zaidi, Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kuelekeza yashughulikiwe na Tume ya Utumishi ya Mahakama. Sehemu ya tatu inajuisha vifungu vya saba hadi 18, inahusu Tume yenyewe ya Utumishi wa Mahakama ikiainisha muundo, *management* na uendeshaji wa Vikao vya Tume. Tume itakuwa na Katibu atakayeteuliwa na Rais atakayesimamia utekelezaji wa maamuzi ya Tume. Sheria inawalinda Wajumbe wa Tume wasiwajibike binafsi kwa mambo waliofanya katika utekelezaji wa majukumu yao.

Sehemu ya nne yenye vifungu 19, 20 na 21 inahusu mamlaka mbalimbali ya Rais kuhusiana na shughuli za Tume. Sehemu hii yote imechukuliwa kutoka katika Sheria ya Utumishi wa Mahakama iliyofutwa.

Sehemu ya tano inajumuisha vifungu vya 22, 23 na 24 na inahusu utendaji kazi wa Tume na kuongeza masuala yafuatayo:-

(a) Kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji, Msajili wa Mahakama ya Rufani na yule wa Mahakama Kuu.

(b) Kumshauri Rais kuhusu Jaji kushindwa kutekeleza majukumu yake.

(c) Kumshauri Rais kuhusu ukiukaji wa maadili unaoweza kufanywa na Majaji.

(d) Kuchambua malalamiko yanayohusu Majaji.

(e) Kuchukua hatua za kiutawala dhidi ya Majaji ambazo hazihusu kumwondoa kazi katika madaraka yake.

Sehemu ya sita ambayo ndio ndefu kuliko sehemu nyingine zote, inahusisha vifungu vya 25 hadi 41. Inahusu Kamati mbalimbali ambazo zitasadia Tume katika kufanya uchunguzi wa tuhuma. Kwa utaratibu tulionao hadi sasa zilikuwepo Kamati mbili, moja *District Judicial Board* ikishughulikia Mahakimu wa Mahakama za mwanzo na nyingine *Regional Judicial Board* ikishughulikia Mahakimu wa Kazi na wa Wilaya. Badiliko la kwanza lililofanyika ni kubadilika kwa majina, sasa zitaitwa *Committees* badala ya *Board*.

Badiliko la pili kubwa katika eneo hili ni kuongeza Kamati mbili ambapo moja itashughulikia kupokea malalamiko kuchunguza tuhuma kuwahusu Majaji na nyingine kuwahusu Wasajili. Kamati za Wilaya na Mkoa zitabakia na majukumu ya kushughulikia Mahakimu wa Mahakama za mwanzo na Mahakimu Wakazi na wa Wilaya.

Sehemu hii inaainisha Wajumbe wa kila Kamati, Wajumbe katika Kamati za Wilaya na Mkoa watakuwa ni wale wale ambao hadi sasa walikuwa Wajumbe wa *District and Regional Judicial Board.* Kamati ya kushughulikia masuala ya Majaji itahusisha Majaji pamoja na Msajili wa Mahakama ya Rufaa atakayekuwa Katibu.

Kamati ya Wasajili itakuwa na Jaji Kiongozi kama Mwenyekiti, Majaji wengine wawili na Msajili wa Mahakama Kuu kama Katibu. Sehemu hii pia itaainisha jinsi Kamati hizi zitakavyopokea na kushughulikia malalamiko na kutaka kila mmoja inapokamilisha jukumu lililokabiliwa, kupeleka taarifa ya uchunguzi kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa uamuzi.

Sehemu ya saba inajumuisha vifungu vya 42 hadi 44 inahusu maeneo ya jumla kama uwezo wa Jaji Mkuu kutoa kanuni kuhusu uendeshaji wa Mahakama Tanzania ikiwa ni pamoja na kuanisha adhabu zinazoweza kutolewa na Tume.

Sehemu hii pia inaifuta Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya mwaka 1962. Sehemu ya nane inajumuisha vifungu vya 45 na 46, inahusu marekebisho katika Sheria ya mwenendo wa Mashauri ya Madai na Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ili kuwataka Majaji na Mahakimu kutoa hukumu haraka baada ya kusikiliza kesi na kwa vyovyote vile iwe ndani ya siku 90 tangu kumaliza kusikiliza ushauri husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru wewe mwenyewe binafsi na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wachambue na kuyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Serikali katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa niseme kwamba sijapata ombi lolote la kuchangia Muswada huu kwa hiyo endapo utamalizika mapema kwa kuwa tunayo Miswada mingine iko kwenye foleni, mchana

tutatoa *Order Paper* ya nyongeza ya ziada ili tuweze kuendelea na Mkutano wetu. Sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Spika anipokee Kiti.

*Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Juma J. Akukweti) Alikalia kiti*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipatia fursa hii adimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Juu wa Muswada wa Sheria inayoainisha masuala ya kiutawala na kinidhamu ya Majaji, Wasajili na Utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu ya Mahakama wa mwaka 2005 *(Judicial Service Bill 2005).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada ya Vikao vya Kamati za Bunge, Kamati yangu ilipata fursa ya kujadili Muswada huu katika Kikao kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 26 Januari, 2005. Katika Kikao hicho Kamati yangu ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu nia na madhumuni ya kuleta mapendekezo yake kama ilivyowasilishwa na Mtoa Mada muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jumla Kamati yangu inauunga mkono Muswada huu, hasa kwa kuzingatia mahudhui ya jumla ya Muswada huu yalenga kuifanya Mahakama kiwe chombo madhubuti kitakachowahudumia watanzania katika suala zima la utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Kamati yangu iliupitia Muswada huu kifungu kwa kifungu na kutoa maoni na ushauri wa Serikali katika maeneo kadhaa.

Aidha, pale ambapo Kamati yangu haikuelewa vyema ilitaka ufafanuzi, Serikali ilitoa maelezo ya ufasaha ambayo yalitosheleza Kamati. Kwa sababu hiyo basi, sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni Na. 70 (2) Kanuni za Bunge Toleo la 2004 katika maeneo kadhaa ambayo Kamati yangu ilijielekeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya Bunge lako Tukufu, kutokana na umuhimu wa muhimili wa dola, Kamati yangu ilitaka ipewe taarifa za Tume za Mheshimiwa Jaji Warioba, Mheshimiwa Jaji Mroso na kadhalika ambazo Serikali ilidokeza katika maelezo yake kuwa Tume hizo za Majaji ziliwahi kuundwa kwa lengo la kuboresha Mahakama na kwamba baadhi ya mapendekezo ya Muswada huu yanatokana na Tume hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, chombo hiki ndio chombo pekee Kikatiba cha kuisimamia Serikali kutunga sheria na kadhalika kwa niaba ya wananchi. Kwa sababu hiyo, Kamati yangu iliomba ipewe taarifa hizo ili ipate kuangalia kwa undani maudhui yake na kutoa ushauri wa kina kwa Serikali kwa nia ya kuboresha muhimili huu wa dola. Serikali iliahidi kutupatia taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika suala la kuboresha maslahi ya Mahakama, Serikali imeithibitishia Kamati yangu kuwa iko mbioni kuandaa sheria kuhusu maslahi ya Majaji. Hapa napenda nisisitize kuwa Kamati ilipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na kuiasa Serikali kuwa juhudi hizo zisiwe za maneno tu bali ziwe za vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 8 cha Muswada kinachohusu uteuzi wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati ilikuwa na Majadiliano marefu kuhusu Katibu huyu kuteuliwa na Rais. Upande mmoja wa Kamati ulidai kuwa kwa kuwa Muswada huu unaimarisha dhana ya uhuru wa Mahakama na mgawanyo wa madaraka basi ingekuwa vema Katibu huyu ateuliwe na Tume yenyewe.

Kwa kufanya hivyo kutampunguzia Rais mzigo na kwamba Ofisi ya Rais, *Management* ya Utumishi wa Umma iangalie uwezekano siku za usoni kuvipa mamlaka vyombo vingine viteue watendaji wakuu. Upande mwingine uliona kuwa ateuliwe na Rais kama ambavyo watendaji wakuu wa Serikali wanavyoteuliwa katika vyombo mbalimbali. Upande huu uliona kuwa kuteuliwa kwake na Rais hakutaathiri dhana nzima ya uhuru wa Mahakama kwani akishateuliwa atalindwa na Katiba na sheria kama wanavyolindwa viongozi wengine. Zaidi ya hayo, Kamati ilitaka sifa za Katibu wa Tume ziwekwe bayana katika sheria. Baadhi ya wajumbe walipendekeza Katibu wa Tume awe Mwanasheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano makali, Serikali ilitoa ufafanuzi juu ya uzoefu uliopatikana wa Katibu wa Tume aliyekuwepo jinsi alivyomudu kazi yake vizuri licha ya kutokuwa Mwanasheria. Juu ya hayo, ilitoa maelezo ya kina juu ya uzoefu wa watendaji wakuu kuteuliwa na Rais. Baada ya ufafanuzi huo, Kamati yangu iliafikiana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu hicho hicho cha 8(1), Kamati yangu ilishauri kuwa hakukuwa na haja kwa wajumbe wengine wa Tume kuteuliwa baada ya kudhinishwa na Rais. Kamati iliona kuwa maneno *with the approval of the president* hayakuwa na maana yaondolewe. Kwa bahati nzuri, ushauri huu umezingatiwa na Serikali kama ilivyo katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 14,15,17 cha Muswada, Kamati yangu iliona kuwa adhabu zilizoanishwa kwenye vifungu hivyo ni vya aina moja yaani kifungo. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa vifungu hivyo vifanyiwe marekebisho ama vionyeshe kifungo na faini au vyote kwa pamoja. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilichukua ushauri wetu na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 26 kinazungumzia kuundwa kwa Kamati ya Maadili ya Majaji. Katika Kifungu cha 26(2)(c), Muswada unapendekeza Jaji Mkuu ateue Majaji watatu wa Mahakama Kuu kwa misingi ya kijiografia na kanda za Mahakama. Kamati yangu haikubaliani na uteuzi kwa misingi hiyo. Hivyo inashauri maneno hayo yafutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vifungu vya 39 na 40 vya Muswada, Kamati yangu ilieleza wasiwasi wake juu ya wajumbe watatu watakaoteuliwa na Kamati ya Mahakama ya Mkoa mmoja wao akiwa anateuliwa na Mkuu wa Mkoa hii ni Kifungu cha 39(d) hali kadhalika wajumbe wa namna hiyo katika Kamati ya Mahakama ya Wilaya mmoja akiwa ameteuliwa na Mkuu wa Wilaya hii ni Kifungu cha 40(d). Kwa kuruhusu wakuu hawa katika Kamati hizi, Kamati inadhani utatokea wakati haki haitaweza kutendeka. Hivyo inashauri kuwa kuwe na udhibiti wa namna fulani kwa wale watakaoteuliwa ama na Mkuu wa Mkoa au na Mkuu wa Wilaya. Kamati inapendekeza kuwa kwa Mkuu wa Mkoa uteuzi uidhinishwe na Waziri na kwa Mkuu wa Wilaya uidhinishwe na Mkuu wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri pia fungu la kuhudumia Kamati hizi litoke Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba moja kwa moja ziwasiliane na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vifungu vya 45 na 46 vinavyotoa ukomo wa siku 60 kwa Mahakimu na Majaji kutoa hukumu katika kesi za madai na jinai, Kamati ilikuwa na maoni ya pande mbili. Upande mmoja uliona kwamba muda wa siku 90 kulingana na pendekezo lililotolewa baadaye na Serikali ni mzuri kwa Jaji au Hakimu yeyote kwa sababu bila kuwawekea kikomo kuna hatari kuwa watajifanyia kazi wawezavyo na hivyo kuchelewesha haki. Upande mwingine uliona kuwa Mahakimu na Majaji wana kazi kubwa na wakifungwa kisheria kukamilisha kazi zao katika muda huo kuna hatari wasiendelee tena na hukumu hata kama hawajamaliza kwa kuwa sheria inawazuia. Hivyo upande huu unapendekeza liwekwe sharti *'proviso'* kumwezesha Jaji Mkuu amruhusu Hakimu au Jaji kuendelea na hukumu endapo ataridhika na sababu zilizotolewa. Kutokana na mvutano huo, Kamati yangu inaishauri Serikali ikiangalie tena Kifungu hicho na kuona jinsi itakavyokiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla haya ndio maeneo ambayo Kamati yangu inashauri na kuyatolea maoni. Kama yapo ambayo nimeyasahau au sikuelezea kwa ufasaha, natumaini baadhi ya wajumbe wa Kamati yangu watajazia pindi watakapopata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nikushukuru kwa mara nyingine kwa kunipatia nafasi hii. Pia nimshukuru Mheshimiwa Harith Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu na wataalam wao kwa kuwasilisha vema maelezo ya Serikali mbele ya Kamati yangu na kufanya kazi ya kuufikiria Muswada huu iwe nyepesi.

Aidha nawashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa michango mizuri iliyozidi kuuboresha Muswada huu. Napenda niwatambue kama ifuatavyo. Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngomba-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali na Mheshimiwa Ramadhani Khalifani.

Wengine ni Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira; Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba; Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

Mwisho kabisa nisingependa kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, ndugu Ernest Zulu, Charles Mloka na Aggrey Nzowa kwa kufanya kila jitihada ili kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Spika anaondoka hapa kwenye Kiti alisema kwamba alikuwa hajapata orodha ya wachangiaji. Sasa kwa maana ya wachangiaji hao wajiandae orodha hiyo sasa imefika hapa na ningependa niwataje kabla sijamtaja Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nao ni Mheshimiwa Dr. Kamala, Mheshimiwa Dr. Kabourou, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Nimewataja ili muweze kujiandaa. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5)(b) na 81(1) kuhusu Muswada wa Judicial Service Act, 2005 yaani Muswada wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada huu kama Mheshimiwa Waziri na hata Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala walivyosema ni kufanya Mahakama zetu kuwa chombo madhubuti na kimbilio la wananchi katika suala la utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana kabisa na dhana na lengo hilo. Vipengele mbalimbali vya Muswada vimejengwa kwa nia na lengo la kutoa na kuimarisha dhana ya uhuru wa Mahakama; vinaainisha masuala mbalimbali ya kiutawala yanayotegemewa kuimarisha dhana hii ya uhuru wa Mahakama na kwa sehemu kubwa Muswada umejikita katika masuala ya nidhamu ya Majaji, Wasajili na Mahakimu ikiwa ni pamoja na utaratibu wa ajira zao, misingi ya utumishi wao na nidhamu yao. Aidha, Muswada huu pia kmsingi unashughulikia masuala yote yanayohusu mkono mmoja wa dola katika mikono mitatu ya dola yaani Serikali, Bunge na Mahakama.

Kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake katika maeneo machache kutokana na umuhimu wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni ya Kambi ya Upinzani katika sehemu ya tafsiri Kifungu cha 2 inatakiwa iongezwe kuwa 'sheria hii inahusu pia Tume ya Huduma ya Mahakama *(The Judicial Service Commission)'* kama chombo kipya kinachoundwa na sheria hii kusimamia masuala yote ya ajira na nidhamu ya watumishi wa Mahakama. Katika sheria hii, shughuli za Tume hiyo zinafafanuliwa kwa kina na kuiacha katika Kifungu hicho cha tafsiri kwa maoni ya Kambi ya Upinzani itakuwa na athari kubwa sana. Ni imani yetu kuwa Waziri atalitafakari hilo na kulifanyia kazi kabla ya majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imetafakari kwa kina kuhusu Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama inavyofafanuliwa katika Sehemu ya 7 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na hasa Ibara ya 125 na 126. Pamoja na ufafanuzi huo mzuri, Kambi ya Upinzani inapendekeza ifuatavyo:-

Kwa kuwa Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano sasa umekomaa na umepanuka sana, kama desturi mtu yeyote anavyopanuka ndivyo pia mawazo yake yanapanuka na mambo mengi yanaanza kuhojiwa, kwa vile Katiba yetu inaunda Mahakama ya Katiba kwa makusudi ya kusikiliza shauri lililoletwa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyonukuliwa katika Ibara ya 126.

Hivyo ni wazi Mahakama hii inatoa tafsiri kwa masuala yanayowasilishwa mbele yake au na Serikali ya Jamhuri au na Serikali ya Zanzibar. Kwa maoni yetu Muungano wetu umekua na watu wengi pamoja na kwamba wanaweza kutumia njia ya kawaida ya kwenda Mahakama za kawaida lakini Mahakama ya Katiba ndio ingekuwa chombo sahihi na pekee cha kutafsiri masuala yote yanayohusu Tafsiri ya Katiba aidha yanayowasilishwa na Serikali au na mtu, kundi la watu au taasisi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya sasa ni tofauti sana na mwaka 1977 wakati Katiba yetu ilipotungwa na hivyo si dhambi tena kuhoji juu ya utekelezaji wa jambo fulani la Muungano kama ilivyokuwa huko nyuma na wala hakuna unyeti wowote katika masuala ya Kikatiba kwani yanagusa maisha ya Watanzania wote katika ujumla wao na hivyo wana haki ya kuhoji jambo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano ni mali ya Watanzania na Katiba ni mali ya Watanzania hivyo kuna haja kubwa kabisa leo wa kuwa na utaratibu wa wazi wa kupata tafsiri sahihi ya Ibara mbalimbali za Katiba na kwa sasa hakuna chombo chochote cha kisheria ukiacha njia za kawaida za Mahakama za kawaida ambao ndio wanatoa tafsiri hiyo. Kambi ya Upinzani inadhani tumeanza kuingia kwenye mitego mibaya kwa mfano suala la kuwa Zanzibar inastahili kuwa na bendera yake imepewa tafsiri na Serikali. Si jambo la kawaida na si vema kwa mtu kuwa hakimu katika shauri lako mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *Hansard* kuna maswali mengi yameulizwa kuhusu Muungano lakini Serikali ndio inayojitosa kutoa tafsiri jambo ambalo sio halali hata kidogo. Kungekuwa na chombo kama Mahakama ya Katiba, watu binafsi, vikundi

vya watu na Taasisi mbalimbali vingetumia fursa hiyo kupata ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali kuhusu Muungano na kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ni kwa jinsi gani orodha ya mambo ya Muungano yameongezeka hadi kufikia zaidi ya 22 kutoka kwenye orodha ya mambo 11 yaliyokuwepo katika Hati za Muungano *(Articles of Union)* ni masuala yanayohitaji majibu ya kina na sio haki kwa Serikali kutoa tafsiri hiyo. Sasa hivi kuna mijadala mingi inavyojitokeza kwenye vyombo vya habari kila kukicha na tafsiri ya migogoro hiyo haina mahali muafaka pa kupata tafsiri sahihi.

Tanzania kwa muda mrefu tumejaribu kuendesha mambo ya nchi kwa kinachoitwa muafaka. Hatuna tatizo kuwa na muafaka kwani ni vizuri jamii ikimaliza migogoro yake kwa muafaka *(consensus)* lakini muafaka hauna misingi ya kisheria japo baadaye unaweza kujengewa nguvu ya sheria. Si kila kitu tutaweza kufikia muafaka. Kadri tunavyoenda mbele mambo magumu yanazidi kujitokeza na ni lazima tuweke *safeguards* yaani njia sahihi za kisheria za kuzuia au kumaliza migogoro inayoweza kutokea huko mbele. Anayeogopa kuweka misingi ya kisheria haitakii jamii hiyo mema kwani siku litakapolipuka jambo si ajabu yeye hayuko tena. Utawala mzuri ni ule unaoacha misingi imara ya kisheria. Tunaitaka Serikali isiendeshe Muungano kama kampuni ya mtu binafsi ambayo hata hiyo ina misingi fulani ya sheria ambayo inaifuata. *(Makofi)*

Isitoshe hata hiyo Mahakama Maalum ya Katiba nayo inafanya misingi ya uuluhishi tu na wala hakuna haki ya kukataa rufaa popote. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa chombo kimoja kusikiliza na uamuzi wake unakuwa wa mwisho bila rufaa ya aina yoyote *administratively* au *judicially* ni kunyonga demokrasia. Misingi hii huenda ilikubalika chini ya mfumo wa Chama kimoja lakini kwa dhahiri kabisa hauwezi kukubalika chini ya Mfumo wa Vyama Vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, tangu Katiba hii imetungwa Mahakama hii Maalum haijakaa hata mara moja pamoja na maswali mengi yaliyohitaji tafsiri ya Kimahakama kuwepo. Kambi ya Upinzani inadhani wakati sasa umefika wa kufikiria dhana sahihi ya Mahakama hii na kuianzisha Mahakama kamili ya Katiba itakayoshughulikia masuala yote yanayohusu tafsiri ya Katiba isiwe kwa masuala yanayowasilishwa na Serikali tu. Mahakama iwe wazi kwa Serikali, Taasisi, watu na makundi ya watu wanaofikiri wanahitaji huduma ya Mahakama hii. Kuona jinsi ambavyo Serikali haikuwa na nia ya kuifanya Mahakama hiyo ifanye kazi, maelekezo yote yaliyo katika Ibara ya 128(4) hayakutekelezwa hata moja kwa karibu miaka 30. Hakuna maelezo mengine labda Waziri alieleze Bunge hili lakini ni dhahiri Kifungu hiki kimewekwa kwa kutimiza tu malengo fulani maalum ya kisiasa kwa wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina tatizo la msingi pia na Kifungu cha 7(1). Hapo mwanzo tumeeleza lengo kuu la Muswada huo kuwa ni kuimarisha uhuru wa Mahakama lakini inaelekea nia hizi tunazitamka bila kuwa na dhamira ya dhati katika kuitekeleza. Katika Kifungu hiki wajumbe wa Tume ya Huduma ya Mahakama ambao ndio chombo au alama ya uhuru wa Mahakama kati ya wajumbe sita watatu wanateuliwa

na Rais, wawili wanaingia kwa nyadhifa zao mathalani Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Kiongozi wajumbe waliobaki yaani Jaji wa Mahakama ya Rufani na wajumbe wengine wawili wanateuliwa tena na Rais. Kifungu hiki hakionyeshi kabisa dhamira tunayoitaja ya kuunda Tume hii kufanywa Mahakama kuwa mkono huru wa dola.

Kwa upande wa Bunge angalau sehemu fulani ya uhuru umejionyesha kwa wajumbe wa Tume ya Huduma ya Bunge kuchaguliwa na Wabunge wenyewe, Spika anachaguliwa na Wabunge. Haiingii akilini kwa mtu yeyote sehemu nzito kama Mahakama yenye watu wazito kabisa, ndio wanaomwapisha Rais wa Jamhuri ya Muungano, ndio pekee katika nchi wamepewa mamlaka ya Kikatiba kutoa uhai wa mwanadamu katika mazingira maalum ya kisheria, ni kweli kuwa watu hawa hawawezi kujichagulia Tume ya kulinda maslahi yao na kujiendesha kama sehemu huru muhimu katika mihimili mitatu ya dola? Kambi ya Upinzani inadhani Serikali inazungumzia kwa mdomo tu suala la *separation of powers* lakini haitaki kuachia kabisa madaraka kwa vyombo hivyo ili vijiendeshe kwa misingi ya mamlaka waliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi inapendekeza Rais ateue Mjumbe mmoja tu wa kulinda maslahi ya mhimili Serikali na Rais mwenyewe lakini Jaji Mkuu kupitia utaratibu utakaondaliwa rasmi na kwa kutumia vyombo vilivyopo chini yake wateue wajumbe wanaotakiwa kuwa katika Tume hiyo na Jaji Mkuu kama alivyo Spika awe Mwenyekiti wa Tume hiyo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itafakari pendekezo hili kama kweli tuna dhamira ya kuwa na mhimili Mahakama aliye huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haiamini kabisa katika kumrundikia Mheshimiwa Rais madaraka mengi ambayo kimsingi peke yake hawezi kuyatekeleza. Tume hiyo ina uwezo kabisa wa kusimamia masuala yote ya nidhamu na ajira itakuwa kama ilivyo kwa Tume nyingine zote zinazoajiri katika Taasisi za Serikali. Isitoshe Kambi ya Upinzani inadhani kama walivyouliza Wabunge wengi kila mara na hapa nanukuu, sheria zilizotungwa na Bunge zinatafsiriwa na Mahakama na wanaendelea kuuliza Mahakama zinasimamiwa na nani? Kambi ya Upinzani inadhani wakati sasa umefika wa *performance* yaani taarifa ya utendaji kazi sio ya utoaji haki ya Mahakama kuripotiwa na kujadiliwa Bungeni. Kwa namna hiyo udhaifu mwingi ulioko Mahakamani utatoweka yaani rushwa, ucheleweshaji kesi usio na msingi, kutojali wajibu wa Majaji, kesi nyingi kwa mfano zinaahirishwa bila sababu za msingi na hata Jaji akiamua tu kupumzika hana wa kumuuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kujadili taarifa ya utendaji kazi wa *Chief Justice,* nchi nyingi zinafanya hivyo na hiyo sio kuingilia majukumu ya Mahakama. Tunapenda Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina katika hili wakati wa kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha uwazi na ukweli, kwa dhati kabisa Kambi ya Upinzani inaamini Kifungu cha 13 na hapa ninaomba nikiri kwamba kama ilivyotokea juzi na *Schedule of Amendment* tumeletewa tena hapa hapa. Kwa hiyo, sijaona ndani humu kuna nini na isingewezekana vile vile kusoma *schedule* hii, kumsikiliza Waziri na wakati huo huo kufanya *amendment.* Kwa hiyo, tumeomba na

tunaomba kwamba hii tabia labda ikome kwa sababu hatutendewi haki kwa kuletewa amendment wakati tayari tuko Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haiamini ni kwa nini iwapo Mjumbe wa *Commission* amewasiliana kuhusu haki fulani mtu aliyeko chini ya Tume yake na vyombo vingine mathalani Tume ya Polisi, Tume ya Huduma za Umma, Tume ya Magereza na mathalani wameingia kwenye hujuma juu ya haki za mtumishi huyo na ameweza kugundua maandishi yanayohusu haki yake ni kwa nini watu hao wasilazimishwe kutoa ushahidi huo ili haki ya mtu huo ilindwe? Naona Ibara ya 13 hapa imetoka kwa kweli kama ilivyokuwa huko nyuma inazaniwa imefanyiwa marekebisho sijagundua ni kitu gani lakini sehemu ambayo naisoma inafanana kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki hakifai katika kipindi hiki ambacho tunakazia uwazi, *client charter* na hatari ya kifungu hiki ni kulinda *syndicate* inayoweza kufanyika kati ya vyombo hivyo vya dola kwa lengo la kuminya haki ya mtu binafsi. Katika nchi yetu hivi sasa watu wengi wanazungushwa haki zao kwa kukosa uwazi wa aina hiyo kwa upande mmoja na *syndication* ya aina hiyo kwa upande mwingine kati ya vyombo vya dola.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanyia marekebisho kifungu hicho ili watumishi pia wafahamu kuwa wakifanya uzembe watawajibika binafsi bila kuihusisha Serikali. Hali hiyo itajenga uwajibikaji mkubwa kati ya Taasisi zinazoshughulikia haki za watu na haingii akilini kuwa unahitaji kuomba *consent* ya Mwenyekiti wakati mtu wake amehusika inahitaji *integrity* ya hali ya juu sana kwa Mwenyekiti huyo kutoa kibali hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati za Mikoa na Wilaya, Kifungu cha 39 na 40, Kambi ya Upinzani inaona mashaka makubwa sana na maeneo yafuatayo:-

(a) Mkuu wa Mkoa na Wilaya kuwa Wenyeviti wa Kamati za Mkoa na Wilaya. Sheria yetu imetamka wazi kuwa viongozi wa kisiasa wasiwe kwenye Tume hii ili kuondoa uwezekano wa mwingiliano wa kisiasa na utoaji wa haki. Kwa bahati mbaya katika nchi yetu japo Wakuu wa Mikoa na Wilaya rasmi wanajulikana kama watumishi wa umma *(public officers)* na hivyo kimsingi hawatakiwi kuwa wanasiasa au mashabiki wa kisiasa au hata kuwa na nafasi ya uongozi katika siasa, hali halisi ni tofauti sana. Wengi wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, wengine ni wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, wengine ni wajumbe wa Kamati za Siasa za Wilaya zao.

Watu hao wala hawafanyi kazi kwa siri na hasa nyakati za uchaguzi husimama rasmi majukwaani kunadi sera za CCM. Tumetoa taarifa kote kunakohusika na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Kumbe dhana ya kuondoa viongozi wa siasa inawahusu Wapinzani tu! Huu sio utawala bora hata kidogo na Kambi ya Upinzani inapinga kwa nguvu zote Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa Wenyeviti wa Kamati hizi.

Iwapo Serikali haitakubali kuleta mabadiliko, Kambi ya Upinzani italeta mabadiliko katika maeneo haya wakati Kamati ya Bunge Zima. Tutaendelea kupiga kelele kuwa kwa makusudi Serikali haitaki kutengeneza uwanja unaolingana. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, bado inasikitisha kuona kuwa wajumbe wote wa Kamati za Mkoa na Wilaya kimsingi ukiacha Hakimu Mkazi au Hakimu wa Wilaya na mteule wa Jaji Mfawidhi wengine wote au wanateuliwa na Mkuu wa Mkoa na Wilaya au ni watu walio chini yao na hivyo wanapokea amri kutoka kwao. Huu si mtindo hata kidogo wa kutengeneza Mahakama ziwe madhubuti na ziachane na rushwa na ziwe mahali pa kukimbilia wananchi wanyonge kama lengo la Muswada lilivyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza Kifungu hicho kiandikwe upya na wajumbe wengi walio huru na angalau wanaweza kuonekana kutenda haki wateuliwe.

(c) Dhana ya kuwaweka Wakuu wa Mikoa na Wilaya inakinzana na dhana ya kutenga Mahakama na Serikali. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa ili kuachana na Mkuu wa Wilaya basi Wenyeviti wa Mabaraza hayo wawe Wakurugenzi wa Halmashauri ambao kimsingi ni watumishi wa umma na hawako kwenye chombo chochote cha Chama cha Siasa. Kwa msingi huo, tutakuwa tumejenga dhana imara, tumetenganisha mamlaka na madaraka na tumweka mtu mwenye mamlaka kusimamia jambo hilo kubwa katika kujenga imani ya wananchi wa eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na dhana ya kuweka muda maalum wa Mheshimiwa Jaji kusoma hukumu yake na kwa vyovyote isizidi siku 60. Naona kwenye *schedule* imebadilishwa sasa inakuwa siku 90. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inadhani haitoshi kukomea hapo kwani ucheleweshaji mwingi zaidi unatokea kwa ma-*Prosecutor* na mara nyingi files zinakuwa kwa ma-*DPP* au kwa Polisi ambao hawajamaliza upelelezi. Kambi ya Upinzani inadhani haitoshi kushughulika na matawi ya tatizo kama mizizi yenyewe haijashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza sheria zote zinazohusu jinai na mwenendo wake zinahitaji mapitio makubwa yaani *overhaul* ili kuhakikisha kuwa haki za msingi za wananchi haziminywi katika ngazi ya kukamatwa na ngazi ya upelelezi. Ni kweli kuwa kwa sehemu kubwa sheria zetu kwa kiasi kikubwa ni nzuri lakini zinakosa watekelezaji wazuri.

Lakini sheria ikiwa wazi haiachi nafasi ya kutumika vibaya na Maafisa wachache itaondoa uwezekano wa sheria pia kutumia vibaya. Hivyo ili haki ionekane kweli inatendeka hatua ya kwanza kabisa iwe ni kurekebisha sheria zote husika. Ndani ya sheria hizo pia yawekwe masharti maalum na adhabu zitolewe kwa mfano kwa Polisi wanaoendelea kusema upelelezi haujakamilika lakini hawafanyi chochote kuukamilisha na au wana sababu zao nyingine za kutokamilisha upelelezi.

Bila kufanya hivyo tutakuwa tunawaonea Waheshimiwa Majaji ambao kwanza wako wachache pili wanastahili vifaa vya kisasa kutekeleza majukumu yao kama taarifa mbalimbali zilivyoonyesha kama ya Jaji Bomani na tatu hawana hata Ofisi ya kukaa kwa utulivu kuandika hukumu na bado tunataka hukumu itolewe ndani ya siku 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutozingatia mahitaji muhimu ya Majaji inasababisha ucheleweshaji mkubwa wa kutolewa kwa hukumu. Kamati yetu imeshuhudia na kuambiwa jinsi Jaji anavyopaswa kumpisha mwenzake ofisini ili huyu mwenzake aweze kusikiliza kesi pale kwenye *chamber*. Ni kutaka miujiza katika mazingira ya aina hiyo kutoka kwa Majaji wetu kuwatakia watoe hukumu katika siku 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ni imani yetu kuwa Serikali itafanyia kazi mambo hayo na mapendekezo hayo na Mheshimiwa Waziri atatoa majibu ya kina kwa manufaa ya kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na timu yao yote kwa kazi walivyofanya kutuandalia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani na nawashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kama nilivyosema tayari tunao wachangiaji hapa, kwenye orodha wako sita kwa hiyo nitawasoma wote ili waweze kujiandaa. Nao ni Mheshimiwa Dr. Kamala, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Khamis Nguli na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai. Sasa natawaita kama nilivyowataja, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu ambao mimi nadhani utachangia vile vile katika kudumisha amani tuliyonayo katika nchi hii kwa sababu unagusa nguzo muhimu ya uongozi wa nchi hii nikiwa namaanisha Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla ya kufanya hivyo, nitoe pole kwa Mheshimiwa Ntagazwa kwa kufiwa na mke wake. Vile vile natoa pole kwa Mheshimiwa Benedicto Malangalila kwa kufiwa na mke wake. Natoa pole kwa Mheshimiwa Hoogan kwa kufiwa na mzazi na natoa pole kwa wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kufiwa na Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwanza ili amani ya nchi hii iweze kuendelea ni vizuri basi nguzo tatu muhimu nikiwa namaanisha Serikali, Mahakama

pamoja na Bunge hili hizi nguzo tatu kila nguzo iwe na uhuru wake na isiwepo nguzo ambayo kwa kutumia nguvu zake za kiutawala ama za kisiasa kuingilia nguzo nyingine. Ikitokea Mahakama ikaacha kuliamini Bunge au Bunge likaacha kuamini Mahakama au Serikali ikaacha kuamini Bunge au Bunge likaacha kuamini Serikali au Mahakama basi itakuwa ni mwanzo wa amani ya nchi hii kuvurugika. Ili amani isivurugike basi lazima kila nguzo ipewe uhuru wake na iheshimike na ifanye kazi kwa kufuata sheria na taratibu na huo ndiyo utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nina wasiwasi kidogo na Muswada huu kwamba huenda ikawa chanzo cha kupunguza uhuru wa Mahakama. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba uhuru wa Mahakama utazingatiwa, mimi binafsi kama mtunga sheria ninaona kwamba sheria hii ikishapitishwa hapa huenda isisaidie kuongeza uhuru wa Mahakama lakini itasaidia kupunguza uhuru wa Mahakama na vilevile huenda ikadhalilisha Mahakama.

Naomba nitoe *interest* kwamba kwa bahati nzuri mimi sitarajii hata siku moja kuwa *advocate* wala sitarajii kuwa Jaji wala Hakimu, mimi tayari nimeingia kwenye mlengo kuwa mwanasiasa lakini kwa sababu sina nia ya kuingia katika Mahakama si sababu ya kuondoa uhuru wa Mahakama sasa ninapenda hilo lieleweke.

La kwanza, kwa nini nina wasiwasi? Wasiwasi wa kwanza ukienda *section 7* kifungu cha 7(e) kinaeleza kwamba kuwa kuna Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kwa ajili ya kuingia kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama. Lakini hapa hakielezi sifa za hao Wajumbe zitakuwa zipi, katika baadhi ya miswada tumekuwa tukitaja hata katika huu kwamba labda fulani akiteuliwa awe na sifa zinazomuwezesha labda kuwa Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Rufaa au Jaji wa Mahakama kuu, sasa unapoiacha hivyo kwamba Mheshimiwa Rais atateua Wajumbe wawili tu kuingia kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama sasa hapa unaweza siku moja ukakuta Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake anawateua wanasiasa tu kuingia kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama na ukifanya hivyo itakuwa chanzo cha kupanda mbegu ya kuvuruga mwenendo wa shughuli za Mahakama.

Sasa ingekuwa vizuri basi tukataja walau sifa kwamba Mheshimiwa Rais atateua watu wenye sifa fulani fulani zinazoendana na duru za kimahakama ili walau wakiwa mle basi asifanye kazi kwa kuzingatia matakwa ya yule aliyemteua bali afanye kazi kwa kuzingatia umuhimu wa kuendeleza uhuru wa Mahakama. Hilo la kwanza.

La pili, ukichunguza Wajumbe wataokuwa kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama nusu yao wote unakuta kwamba wanateuliwa na Rais sasa ukiiacha hivyo madhara yake yanayoweza kutokea baadaye ni kwamba kwa taratibu unazidi kuongeza nguvu za *executive branch* ya State maana yake unazidi kupunguza nguvu za Mahakama kwa kuwa na watu wengi zaidi wanaoteuliwa moja kwa moja na kiongozi mkuu wa *branch* nyingine. Kwa hiyo, hata ukisema unaongeza uhuru wa Mahakama maana yake hapa unakuwa unapunguza uhuru wa Mahakama.

Mimi ningependekeza labda *Law Reform Commissioner* inaweza ikawa na mtu ambaye anaingia kwenye hiyo Tume ya Utumishi wa Mahakama lakini tuna chama cha wanasheria kinaweza kikawa na mtu ambaye anaingia kwenye Tume ya Huduma za Mahakama, lakini vile tunao wataalam wengine ambao wanajulikana kwamba wanahusika moja kwa moja na masuala ya Sheria na Mahakama. Watu wa namna hiyo wanaweza wakaenda kwenye Tume hiyo na wakafanya kazi ikawa nzuri nzuri zaidi na Mahakama wakajisikia kwamba uhuru wao upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 kinaelezea kwamba Mheshimiwa Rais atatunga taratibu mbalimbali ambazo zinaweza zikatoa miongozo ya Tume ya Mahakama ifanye kazi namna gani. Sasa unapoiacha hivyo kwamba Mheshimiwa Rais anaweza akatunga kanuni zozote basi usishangae siku moja Rais akatunga kanuni kwamba Tume ya Mahakama isifanye jambo lolote kama yeye hajatoa kibali cha kufanya hivyo. Sasa tukifikia hapo uhuru wa Mahakama tunaoungelea utakuwa haupo, sikatai Rais kutunga taratibu za kusaidia kuongoza Tume hiyo lakini lazima tujue ni kwa mambo yapi Mheshimiwa Rais anaweza akatunga taratibu na ni kwa mambo yapi Mheshimiwa hawezi kutunga taratibu.

Kwa mfano, tunatamka katika Katiba yetu kwamba Mahakama ndicho chombo cha juu kabisa ambacho kina uwezo wa kutoa haki na kwa sababu hiyo hatutarajii tena awepo mtu mwingine kikatiba au kwa kutumia sheria ndogo ya Bunge ambaye anaweza akatunga taratibu ambazo zinaweza zikaendelea kugusa uhuru wa Mahakama kutoa haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiachana na eneo hilo tunaenda kifungu cha 19 ambacho kinaeleza kwamba Mheshimiwa Rais anaweza kuanzisha au kufuta ofisi yoyote ya Mahakama lakini tukumbuke kwamba Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zipo ofisi zinazoanzishwa rasmi na Katiba ya nchi, sasa ukishakuwa na ofisi za Mahakama zinazoanzishwa na Katiba ya nchi lakini baadaye ukawa na sheria ya Bunge ambayo inasema Rais anaweza kufuta ofisi yoyote ya Mahakama maana yake sheria hiyo itakuwa batili kwa sababu itakuwa inapingana na Katiba lakini Mahakama hiyo inaweka nafasi kwa Rais ambaye hatakuwa na busara kuweza kufuta hata Mahakama zote kama ataamka kutoka usingizini akaona Mahakama zinaingilia kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wasiwasi wangu kwamba ni vizuri tukadumisha uhuru wa Mahakama ningependa itajwe ni ofisi zipi ambazo Rais akiamua anaweza akafuta lakini tuelewe kabisa kwamba ziko ofisi zinazoanzishwa kikatiba na hizo Mheshimiwa Rais akae akijua kwa vyovyote vile hawezi kuzifuta labda kama sheria imeletwa ndani ya Bunge hili na Bunge hili likaamua kufuata mabadiliko katika katiba ndipo ofisi hizo zinaweza zikafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye kifungu namba 39 kinaelezea Wajumbe mbalimbali watakaoingia kwenye Kamati za Utumishi wa Mahakama ngazi ya Wilaya, lakini nilipozipitia nimekuwa na wasiwasi nikaona sasa Mahakimu wa Wilaya na *Resident Magistrates* sasa watafanya kazi zao kwa wasiwasi na hiki kitu tunasema uhuru wa Mahakama kitakuwa hakipo.

Haiwezekani ukawa na Hakimu Mkazi ambaye unasema ni wa Mkoa lakini ambaye anatazamwa kwa karibu utendaji wako wa kati na Kamati inayoongozwa na Mkuu wa Mkoa, Kamati ambayo ina baadhi Wajumbe wanaoteuliwa na Mkuu wa Mkoa ambaye vilevile *Regional Administrative Secretary* yumo kwenye Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinaondoa tu uhuru wa Mahakama na si kweli kwamba kinaongeza uhuru wa Mahakama, nakubaliana na dhana ya kuwa na Kamati kama hii lakini nashauri iwe na Wajumbe wanaotokana na duru za kimahakama na wala si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kifungu cha 40 kinaelezea Kamati kama hizo za wilaya na tatizo ni hilohilo ambalo nimeeleza, unapunguza uhuru wa Mahakama. Ukienda kwenye *section* ya 47 *proviso to section 43 page 23 of the Bill ina-refer* kifungu ambacho hakipo nitaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kifungu kipi ana-*refer* hapo kwa kutokupoteza muda.

Ukienda kifungu cha 45 kinaelezea kwamba kinaweka utaratibu wa jinsi ambavyo Hakimu au Jaji atalazimika kutoa hukumu kwenye siku 90 lakini ni kwa bahati mbaya kimesahau kutaja *decree* ni uamuzi wa kukaza hukumu wanasema wataalam.

Sasa ukienda kwenye *section 28* labda niwaambie wataalam wetu waje waangalie kwa haraka ukienda kwenye *section 28* ya *Civil procedure court ina-provide for both judgment and decree* lakini humu tunasema tu kwamba *judgment* ikiisha tolewa basi kwenye siku 90 iwe imepatikana lakini tumesahau *decree* ambayo wakati mwingine inaweza ikawa na umuhimu mkubwa zaidi kuliko hata hukumu yenyewe. Kwa hiyo, ningeomba pale neno *decree* liongezwe kwamba *judgment* na *decree* nadhani itakuwa imesahaulika kwa bahati mbaya si vizuri ku-*assume* kwamba *judgment* siku zote itakuwa ni *decree.*

Mheshimwa Spika, la mwisho ambalo niliseme ni kwamba Muswada huu ni mzuri kama tutaboresha na tukajaribu kuhakikisha uhuru wa Mahakama unaheshimika lakini matatizo mengi yanayotokea kwenye Mahakama si kwa sababu Mahakimu wetu wanashindwa kufanya kazi nzuri na si kwa sababu majaji wetu wanashindwa kufanya kazi, si kweli. Tatizo kubwa ni fedha tunazotenga kwa ajili ya Mahakama ni ndogo, Mahakimu tulionao ni wachache na matokeo yake sasa kuna vurugu kubwa kwenye Mahakama. Kwa hiyo, hata kama ungekuwa na Muswada mzuri namna gani na kamati nyingi za kudhibiti Mahakimu na Majaji na wengineo kama hatujawa na mkakati wa makusudi wa kuziwezesha Mahakama nakuhakikishia Muswada huu utakuwa kazi bure.

Iko mifano ambayo ningetaka kuitoa lakini kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi mambo mengine si vizuri kuyaongea Bungeni maana unaweza ukaongea jambo kwa nia nzuri tu lakini wenzako wenye akili ndogo wakalipotosha na kwa sababu hiyo niongee tu kwa ufupi kwamba ni vizuri tukaiwezesha Mahakama kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. Dr. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi kidogo nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono moja kwa moja na hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu suala la Mahakama ya Katiba, nadhani imesahauliwa na niseme vilevile labda hapa tuna tatizo la kutoelewa demokrasia, tunadhani hii mihimili mitatu ni vitu vinatajwa halafu basi mnasahau. Kuna mifano mingi tu, mimi naona ajabu kwa mfano hata hili neno Tume, Tume ya Kazi ni jambo tu linatumika Tume ya Magereza, Tume ya Polisi, Tume ya Bunge ni lazima kuwe na utaratibu wa kutumia kitu ambacho kina- signify kitu kikubwa sasa kuna Tume ya Polisi, Tume ya Magereza. Nazungumzia mihilimi ni mitatu tu Tanzania nzima hatujaweka vyombo vya habari *of course* hiyo ni forth state lakini kwa sasa tunajua iko mitatu lakini sasa hata hilo neno tu Tume lenyewe linasikitisha. Kila kitu ni Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu jambo jingine linalonisikitisha ni kwamba ghafla Tume ya Utumishi wa mhilimili mmoja wa Demokrasia nchini mwetu inateuliwa na kiongozi wa mhimili mwingine. Peke yake inatisha, ndiyo hawa wanapitia hapa kifungu namba 7, 11 tumeshaona athari za vitu vya namna hii, unaposema Rais anaweza kufanya hivi sasa si Rais hivyo hivyo alisema kwamba *PCB* inaweza ikafanya upelelezi au isifanye upelelezi kama hakuelekeza. Rais.

Sasa tunajua kwamba miswada inaletwa na Serikali na lazima ipitie kwenye Baraza la Mawaziri na Rais yupo pale sasa labda kwa uoga watu wanamlimbikizia madaraka sisi tunataka *the congestion of powers* za Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengi hapa Afrika kwetu ni hivyo mtu anakuwa na nguvu nyingi tumesikia Togo tu jana hapa mtoto wa Rais kashakuwa rais, kinyume kabisa cha utaratibu ana nguvu nyingi sana na ndilo tatizo na sasa tunazungumzia mihimili mitatu. Idara ya Mahakama tumeondoa juzi tu hapa kwenye Muswada uliopita tukasema Idara bwana inadhalilisha kidogo iitwe Mahakama kuu, lakini sasa Mahakama yenyewe inawekwa chini ya Serikali kwenye ngazi zote, ngazi ya juu kabisa Rais anateua watu hawa, anamteua yule anamweka yule Jaji mkuu mwenyewe kateuliwa na huyo huyo, yule kateuliwa na huyu basi watu wote walioko mle ni watu walioteuliwa na Rais. Sasa kwa nini hawa wasipewe nafasi kama Tume ya Bunge ilivyopewa nafasi ya kujipanga, tuanze kukubali kwamba Rais siyo kila kitu, tuanze kukubali hilo kwamba ana kazi zake na ni nyingi tu sasa tusimuongezee kazi anafuta na Mahakama, atafuta na hiki, sasa sisi tutakuwa ni Serikali gani hiyo ambayo muhimili mmoja saa yoyote unaweza ukaingilia kazi za mhimili mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hilo limenitisha sana, sasa baada ya kusema hayo mimi naamini siungi mkono Muswada huu kwa jinsi ulivyo kwa sababu tumetoa sababu za kutosha *DC* ni mkuu wa Mahakama, *DC* ni mkuu wa Mahakama na *DC* ni mjumbe wa Kamati ya siasa ya chama fulani Mkuu wa Mkoa hivyo hivyo sasa najiuliza hivi huko kwenye Mahakama hakuna watu wanaotosheleza kufanya kazi kwa niaba ya Mahakama? Hivi kwa nini *DC* awepo? Kwa nini tunampa *DC* kazi ya utendaji, kama tunataka ku - replicate kama nia ni *replicate* mfumo kwa vile huku juu

tumeshasema Rais atamteua Jaji Mkuu, atamteua na huyu, atamteua na huyu, wateuliwa wote ni Rais kwenye hiyo Tume ya Mahakama. Lakini hatumwoni Rais kama ni Mwenyekiti wa Tume ya Mahakama, tunamwona pale? Sasa mdogo wake Mkuu wa Mkoa yeye anapewa kabisa na uenyekiti kwenye Tume ya Mahakama katika ngazi ya Mkoa au Wilaya, sasa mna-*replicate* nini? Basi na Rais mumfanye Mwenyekiti wa Tume ya Mahakama juu awe anakaa pale Jaji Mkuu naye anamsikiliza kwa sababu Mkuu wa Mkoa akikaa *magistrate* anamsikiliza yeye. *(Makofi)*

Unaweza ukamwambia bwana unajua hawa wapinzani wanatukanatukana lazima afungwe mmoja na kweli haya mambo yakatokea kwa sababu yule anaona uoga asitungiwe hoja nasema hivi kama mnataka huyo *DC* na Mkuu wa Mkoa waendelee kuwa Wenyeviti wa hizo Tume za Mahakama huko mikoani na Rais tumfanye Mwenyekiti wa Tume ya Mahakama. Si wadogo zake wale? si ndiyo wanakopata madaraka yao, basi tumpe na yeye tunaogopa nini tumpe bwana Mheshimiwa Rais awe anaingia kwenye vikao vyote anamaliza mambo pale. Mimi sitaki niseme hayo kwa sababu sasa hivi yamesemwa sitaki kurudia nadhani Mheshimiwa Dr. Slaa ameyaweka vizuri sana na kwa kweli tunatakiwa tuliangalie hilo. Mimi nasema kwa utaratibu ulivyo ni kwamba Serikali yetu inapoamua jambo lake wanakuja wanalipitisha hapa kura ni nyingi tu za CCM hakuna matatizo kwa hiyo kuna uwezekano Muswada ukapita pamoja na mawazo yetu haya ambayo tunayasema kwa nia njema tu sasa kama utapita naomba Jaji Mkuu kwa sababu yeye amepewa sasa Mamlaka ya kusimamia utendaji wa Mahakama imesemekana zamani alikuwa hana lakini sasa anayo. Jaji Mkuu apewe pesa ili isiwe tu hata ugawaji wa mihimili hii mitatu basi tu ni *balance* sijui Bunge, Serikali na Mahakama hapana na wananchi na wenyewe wananufaika nini na huu ugawaji wa madaraka. Wananufanika vipi? Mimi nastaajabu na tumesema hapa mara nyingi tukiambiwa hapa kuboresha shughuli za Mahakama tunachofikiria ni kwamba na Jaji awe na Shangingi kama Waziri na anapewa na nyumba *Oyster Bay* na nini, na nini lakini tunasema hivi kweli kwa nini Jaji asiwe na vinasa sauti na vipaza sauti kama tulivyonavyo hapa Bungeni ili awe anaandika taarifa ya yale yaliyosemwa na watu na isiwe ni mawazo yake tafsiri zake.

Tuna Mahakama ngapi? tuna majaji wangapi 50, 30 sijui 40 kweli kamashine kamoja kama haka katatushinda kwa kila jaji? Ili tuwe na uhakika na tunapozungumzia Mahakama na kutoa uhuru na kadhalika hivi tunajua ni mateso mangapi wanayopata watu kila mahali Tanzania? Mwenyewe mimi nimewahi kuwekwa jela na dhamana yangu ikawa inangoja jaji inamngoja jaji tumekaa mwezi na nusu na akaja akafuta tu mashitaka kama ilivyo Serikali yetu haimlipi mtu kwa sababu Kigoma hakuna jaji. Tumesema hapa kwa nini wasiwepo majaji kila mkoa? kwa nini watu walundikane Dar es Salaam? Kila mkoa uwe na Jaji, tuongeze majaji. *(Makofi)*

Kuna watu walikuwa wanazungumza hapa kwamba tuwe na majaji 60 au 70 miminakubaliana na hilo lakini wapelekwe kila kila mkoa, kuna mtu ameshakwenda pale amekiri mahakamani kwamba nimeua lakini anangoja miaka miwili rumande kungoja hukumu yako kwa sababu jaji hajaja kwa sababu jaji hana pesa,sasa huyu mwananchi ananufaika nini na hii mihimili ndicho tunachotaka kujua sisi. Kwa nini asiwepo jaji kila mkoa akatoa maamuzi wakati muafaka ili wananchi wapate haki yao hata kama ni haki

ya kunyongwa apewe anyongwe kuliko kukaa gerezani miaka mitano anangoja jaji ambaye anasemekana atakuja na ambaye haji kwa sababu hakuna pesa. Sasa tungeomba Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa sababu unapewa kazi hii uhakikishe kwamba hao majaji wanatawanywa wa wananchi wanapata huduma ya Mahakama popote walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa nimwulize Jaji Mkuu atakapokuwa anatengeneza utaratibu wake hivi ni kitu gani kinachozuia hata kwenye kesi za uchaguzi ambao unakuja na zitakuwepo, Jaji asiwe na jury ni kitu gani? Hapa anahukumiwa Mbunge kuna mtu alisema alitoa khanga na mwingine akasema yule nilimwona anampiga fulani. Watu waliotengenezwa kuja kuweka taswira fulani pale mahakamani amekuja Jaji Kigwalilo kutoka Musoma hajui utaratibu wa watu wa Kigoma linasemwa neno ambalo kwa mtu yeyote wa Kigoma angeambiwa asingeamini lakini yeye kwa sababu ni jaji anafuata *principle* tu hana mtu wa kumsaidia. Kwenye kesi ya uchaguzi watu wa wamekwisha chagua, wamepiga kura 30 anakuja kutenguliwa na mtu mmoja aliyekaa peke yake pale na tena anaandika anavyotaka yeye wala hakuna ushahidi kwamba ukienda kesho ukasema mimi nilisema ukuta huu ni rangi ya bluu yeye anaandika alisema ukuta huu ni kama manjano.

Mheshimiwa Spika, ukisema hapana anapinga huyu na nini sijui utapitia utaratibu huu utakwenda huku tunasema sisi kama raia tunapata nini kwenye hii mihimili na uboreshaji huu? *Why not?* Leo kwenye utaratibu tulio nao mimi sijui tumeutoa wapi maana yake kila mahali tunajaribu kugoma kwamba ooh! bwana sisi ni Westminster, hakuna. Leo na tumeshapata malalamiko hapa mara nyingi na Waziri wa Sheria ni shahidi kwamba wazee wa Mahakama hawajalipwa posho zao, wazee wa Mahakama sijui nini *jury* ya Tanzania imekuwa ni kazi wakati hata *definition* ya *jury* haisemi kwamba ni kazi. Wenzetu wanakaa tu wanapitia *roster* ya walipa kodi wale au wapiga kura wote halafu wanachaguliwa tu watu kila miezi mitatu wanakuja wanaisaidia Mahakama lakini hapa imekuwa ni kazi. *Why?* Hii ni *module* ya wapi? na kama kuna ma-jury *permanent* pale kwenye Mahakama za mwanzo kwa nini tusiwenao kwenye Mahakama kuu? Hasa kwenye kesi kubwa ambazo zina-*involve public interest* masuala ya siasa, mimi nasema jaji mkuu hili tungependa kwa kweli liangaliwe. Vilevile wamelalamika watu wengi hapa kuhusu taratibu na misongamano ya watu magerezani, hukumu kutotolewa kwa muda na kadhalika hilo limesemwa vizuri na mimi nimeunga mkono kabisa kwamba siku 90, siku 60 mimi sijali ni ngapi lakini uwepo muda ambao hakimu na jaji ni lazima watoe hukumu, mimi naifuatilia kesi moja ya Ndugu yangu Kiongozi nimeandika barua mpaka kwa msajili, mpaka kwa jaji mkuu, mpaka leo hakimu alishamaliza kesi lakini hajatoa zaidi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dhamana, polisi hajamaliza upelelezi hivi ni hakimu gani huyu anakaa anakuja askari anasema Mheshimiwa Hakimu naomba huyu apelekwe rumande kwa wiki mbili kwa sababu sijamaliza upelelezi na wewe hakimu unacheka tu khe! utakwenda rumande. Huoni kwamba yule raia ananyimwa haki yake pale? Hivi wewe askari ulimkamatia nini mtu huyu kama unajua wewe huna ushahidi, ulimkamatia nini sasa? Au ni mchezo tu askari anafika ananikama ananipeleka pale kwanza nasota siku mbili pale au saa 48 ambazo zinaruhusiwa kisheria halafu keshokutwa naingia mahakamani, mahakamani kuna mizengwe lete barua fulani na

utaleta na hati ya nyumba. Mtanzania gani ana hati ya nyumba halafu baada ya kuleta ile hakimu anasema aah! bwana unajua bado utakwenda wiki bili.

Wewe unampotezea mwenzio wiki mbili kwa uzembe wa askari? Hivi huyu hakimu anaogopa nini kumwambia askari kwa sababu umeshindwa kufanya upelelezi huyu mtu anakwenda nyumbani wewe ukimaliza upelelezi utamleta , anashindwa nini kufanya hivyo? Hivi wananchi wanapata nini kwenye haya sijui maboresho, sijui vitu gani, jaji atapewa gari sijui hakimu atapata nini? tunataka nini sisi wananchi dhamana ni kitu ambacho kipo kikatiba na makosa yake yanajulikana ambayo yatakuwa yana dhamana na ambayo hayatakuwa na dhamana. Kwa nini yote yamechanganywa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshaona kesi ambayo ina dhamana mtu hapewi dhamana, wanasema huyu ni mhalifu sugu huyu kwa *proof* ya nani? Katika utaratibu kama huu tulionao Watanzania ambapo askari anaweza akamkamata mtu yeyote akamwambi wewe umezurura, mtu anaweza kukamatwa mara sita bila kosa bila lolote na kila mara akapelekwa polisi na akafunguliwa na kesi na ikafutwa kwa sababu hakuna ushahidi na kwa sababu kulikuwa hakuna msingi wa kumkamata lakini mara ya saba ikifika hakimu analetewa faili anaambiwa alishakamatwa mara sita huyu, huyu ni mhalifu sugu aende tu na hakimu anasema nenda. Hatujali haki za raia, haki za binadamu, hivi huyu Mtanzania amekukosea nini mpaka akakae rumande wiki mbili, wiki nne, mwezi anangoja polisi amalize upelelezi wake. Sasa kama uzembe wewe unautafuta wapi? Si ndiyo uzembe wa polisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema pamoja na yote mimi siungi mkono hoja hii kwa sababu tu naona kwamba *executive* imekuwa na mkono mzito kwenye Mahakama kwa kuwaingiza viongozi wa Serikali moja kwa moja lakini kama kutakuwa na marekebisho kwenye hayo sisi tuko tayari kuunga mkono Muswada huu au sheria hii na kwa kweli wakati umefika sasa kuitambua Mahakama kama ni muhimili husika kabisa katika utawala wa nchi hii na upewe uhuru wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. Dr. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote ningependa kuchukua nafasi hii nitoe rambirambi zangu za dhati kwa wanachi na wapiga kura wa jimbo la Kasulu Mashariki kwa kufiwa na mpendwa wao Hayati Mheshimiwa Frank Mussati. Pia ningependa kuchukua nafasi hii kuwapa Waheshimiwa ambao wamefiwa na wake zao, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Benito Malangalalila naomba kuwapa pole sana. Tatu ningependa kutoa pole kwa wale ambao wamefiwa na ndugu zao, wazazi wao na watoto kwa kipindi hiki naomba kuwapa pole na ninamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema peponi.

Baada ya kutoa rambirambi zangu ningependa nichukue nafasi hii kwa niaba ya wapiga kura wangu wa wanawake wa Morogoro kuwatakia Waheshimiwa Wabunge heri ya mwaka na baraka za Mwenyezi Mungu kwa mwaka huu wa 2005. Napenda sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wao wote na kamati husika kwa kutengeneza huu Muswada ambao

kwa kweli kwangu mimi kama mwanamke na raia ninayetoka kwenye wilaya ambazo ninaona matatizo mengi ya wananchi ni Muswada nyeti kabisa kama kweli hii sheria itapita na itatekelezwa kama ilivyoandikwa humu mimi ninaamini kwamba Watanzania wengi watapata haki za hususani wanawake ambao wengi wamekosa haki zao na walikuwa hawajui wafanye nini ili kutetea haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kabla sijaendelea ningependa tu kuangalia kifungu cha 39 (d) kwa pamoja na kifungu cha 40(d) pale ambapo wanasema kwamba: *"three other members one of them being a minister of religion appointed by the regional commissioner from among prominent persons in the region".* Mimi ningependa tu kutoa tahadhari hapo sisi Watanzania wengi tunaabudu katika dini moja au nyingine, kuna wakristo na hao wakristo wana madhehebu mengi mengi kidogo kuna waislam na ninafikiri waislam wana madhehebu mbalimbali mle ndani sasa pale ambapo mkuu wa mkoa ataamua amchukue mkristo aache waislamu nafikiri kutakuwepo na tatizo kidogo kwa hiyo kutakuwa hakuna *equal representation* kutokana na itikadi za dini.Mimi ningeomba kwamba kifungu kiangaliwe vizuri zaidi na kama inawezekana kuboreshwa kiboreshwe, kikubalike kwamba labda viongozi wa dini kati yao wakae pamoja waamue kumteua mmoja ambaye ataingia katika hii kamati kwa niaba ya viongozi wote wa dini ambao watakuwa kwenye ule mkoa. Hapa tutakuwa tumetoa *democracy of representation* katika hizi kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi nizungumze kidogo kuhusu muundo wa wale ambao watateuliwa na Mheshimiwa Rais na watakaoteuliwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Mimi naomba nitoe rai moja, rai yangu ni kwamba katika uteuzi huu tuangalie basi uwiano wa jinsia. Kwa nini nazungumza hivyo, ni kwamba nimesema humu kote ni kwamba, hata ile *adjective* inayo-*describe* mwanaume, mwanamke huku unakuta ni him, him, him. Kwangu nimeona kila kitu kinaelekea kwenye mfumo dume kwenye hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wanaopata matatizo katika nchi hii ni wanawake hasa kwenye kesi za mirathi, talaka na waume zao wenye pesa, wanawake katika kunyang'anywa hata mali zao baada ya waume zao kufa na pia kunyang'anywa mali zao baada ya wazazi wao kufa ambapo baba alisema mimi namwachia mwanangu Hadija shamba hili. Baba akishafariki wanaume wanaamua kuchukua lile shamba na kwa kuchukua kitu wanachoita *customary law.* Sasa unakuta hawa akinamama kwa sababu wengi wapo Vijijini wanashindwa kujua waende kwa nani. Lakini nimeona kwamba wanawake wengi wanajisikia *more comfortable* kama watajua kwamba kuna mtetezi wao katika ile Kamati ambaye ni mwanamke, ambaye pia wanaweza kumwajibisha kwa kumwuliza wewe mwenzetu mbona unatuacha kwenye mataa. Kila siku, kila mmoja anavutia kamba kwake, sidhani kwamba atakwenda mama pale alalamike kwamba mimi nilikuwa na kesi yangu na mume wangu Mheshimiwa Waziri, halafu wale wanaume kwenye ile Kamati wastuke, hata kidogo. Wataona ni haki kumlinda Waziri, Mkuu wa Polisi, Mkuu wa Mahakama au Mwanasheria mwenzao. Mimi naomba hilo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba pamoja na unyeti wa sheria hii na pamoja na kwamba sheria hii italinda maslahi ya wananchi kwa kuangalia kwamba watendaji wa Mahakama wanafanya kazi kufuatana na maadili yao. Mimi naamini ni maadili makubwa sana lakini kwa sababu binadamu wana hulka zao tofauti na malengo tofauti ndio sababu wanafikia kuwanyima watu haki zao ili mradi waweze kupata maslahi. Nafikiri mengine wanayafanya kwa makusudi kabisa wakijua kwamba huyu mwananchi ninayemkandamiza hajui aende kwa nani akalalamike kwamba nimemnyima sheria. Sasa ni jukumu letu sisi na ni jukumu la Serikali yetu ambayo imeona umuhimu wa kulinda ile *ethical commitment* ya hawa wahudumu wetu wa Mahakama waweze kutengeneza mkakati mahsusi wa makusudi kabisa ambao utahakikisha kwamba kila mwananchi wa nchi hii anaelewa yale yote yaliyoandikwa katika huu Muswada utakapokuwa sheria. Nafikiri tuna Wanasheria wazuri sana katika Idara ya Mahakama ambao wanaweza wakafanya muhtasari wa yale muhimu ambayo mwananchi anatakiwa kujua ili ajue kwamba anamwajibishaje mtu ambaye hampi haki yake pale ambapo anaamini kwamba anaweza kupata haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara ya kwanza kufahamu kwamba kwenye ngazi ya Mkoa kunakuwa na hiyo *Judicial Committee,* ndiyo mara yangu ya kwanza nasikia. Nafahamu kwamba ipo kule kwa *DC* ambako tunalalamika kwa ajili ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na kwenye *District level* lakini kule kwingine hatukujua. Sasa mimi ambaye nimesoma shule, nasoma magazeti na ambaye ni mtunga sheria nilikuwa sijapata ufahamu mzuri. Sasa yule mwananchi ambaye anatoka kule kwetu tuseme Kijijini mbali kule Malinyi, redio haisikiki, televisheni haipo, magazeti hayafiki, huyu mwananchi anaelewaje ile haki yake ambayo tumempa kwenye huo Muswada wa sheria? Mimi naomba vitengenezwe vijarida, Serikali itumie njia yoyote ile ambayo inaweza kumwezesha mwananchi kujua haki yake aliyopewa ya kulalamika na alalamike kwa nani na pia kama kuna muda ambao umewekwa, *time factor* kwamba muda unaopewa kulalamika ni siku thelathini au nini uwekwe bayana, sijauona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naomba nieleze, wananchi wengi wamekosa haki zao kwa sababu hawajui kwamba kuna muda wa kukata rufaa. Hakimu anatoa ile hukumu pale anazungumza kwamba unaweza ukakata rufaa, mambo yamekwisha hasa kama anajua kwamba amekunyima haki, inasemwa *court,* watu wote wanaondoka na yule mwananchi anabaki anazubaa zubaa *by the time* anakuja kuzinduka kwamba kuna kukata rufaa muda umeshapita na hajui sasa afanye nini. Sasa hilo ndilo ninalosema kwamba tunatunga sheria nyingi hapa, tunatumia kodi ya wananchi, halafu hizi sheria zinakwenda kuwekwa kwenye *shelves* haziwafikii wananchi kwa mtindo unaoeleweka. Isingekuwa vibaya hizi zikapelekwa pia kwenye *library* za shule za sekondari, tunajua kwenye Vyuo Vikuu zipo kwa sababu kuna wanafunzi wanaosoma sheria. Lakini ziwekwe basi mle na kwenye lile somo la uraia igusiwe ili wale watoto wajue ili waende wakawaeleze hata wazazi wao nyumbani. Naomba hilo liangaliwe na lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia pamoja na kusema kwamba tunatengeneza vyombo vya kufuatilia na kulinda maadili ya utendaji katika Mahakama, hivi kwa nini tusijiulize pia kwamba kwa nini hawa watu wanavunja

maadili ya kazi yao? Kati ya hawa Mahakimu kuanzia *level* ya *Primary Court* kwenda mpaka Mahakama Kuu ni wangapi wanaapishwa kufanya kazi zao. Sisi Madaktari tunajua kwamba kila Daktari mwenye degree anaapa kufanya kazi kwa maadili anayoyajua yeye na aliyofundishwa. Lakini mimi sijui kama Mahakimu wetu kwenye Mahakama za Mwanzo wanaapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watu kwa kweli jamani hawajui hata maadili yao kwa sababu wakati unakwenda kumwuliza huyu mwananchi amelalamika hili naomba ushauri na mwongozo wako, majibu mengine anayokujibu ni mabaya sana, kama mtu unajua *psychology* unajua kwamba huyu hajui anawajibikaje kwa mwananchi na hajui kwamba maadili yake ni nini. Sasa naomba pamoja na kuwawekea vyombo vya kuwabana na wao wakumbushwe mara kwa mara maadili yao *put it in writing* kuwepo kabisa na kijarida ambacho yeye anakaa nacho siku zote anakisoma soma akijua kwamba mimi maadili yangu ni haya. Tusimwajibishe tu kwa sababu wengine hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine, Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anasaini *eviction order* barabarani bila faili, mwananchi anatupwa nje. Inabidi sisi kama walinzi wao wa amani na haki tulalamike, tunapokwenda kulalamika inakuja kugundulika kwamba hilo faili halipo na ameamua yeye ku-*act* badala ya *Resident Magistrate.* Halafu ukimwuliza *Resident Magistrate* sasa ndugu yangu tunafanyaje? Anasema ahaa, lakini nyie ndio mnaotunga sheria. Tunatunga sheria lakini ndio nyie mje kuzivunja? Sasa unafika mahali unaanza kufikiri kwamba huyu mtu kweli alielewa kwamba anafanya kosa kusaini eviction order barabarani tena kwa niaba ya *Resident Magistrate* ambaye siku hiyo alikuwa kazini. Mimi nimeona kwamba yule haelewi. Kwa hiyo nafikiri pia na Mahakama itafute namna ya kuwakumbusha na kuwaelimisha mara kwa mara, basi wakumbushwe kwa sababu binadamu wanasahau jinsi siku zinavyokwenda na jinsi ambavyo na yeye anakuwa labda hakulelewa kwenye maadili mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalofikiri ni kwa nini Mahakimu wetu wanatunyima haki zetu kama raia. Wengine wanatunyima haki zetu kwa sababu ya maslahi yao ya kazini. Mishahara yao ni midogo, marupurupu mengine wanayoyapata pia sio mazuri na unakuta kwamba kuna ushahidi, mashahidi wanatakiwa walipwe na Mahakama ili waweze kusafiri, lakini shahidi anakuja mara ya kwanza halipwi, hapewi hata posho ya chakula au kulala, mwingine anatoka mbali inabidi asafiri siku moja au mbili afike Mahakamani, lakini unakuta kwamba hakuna pesa ya kumlipa huyu. Inapofika sasa aende kumalizia ushahidi wake hafiki, sasa kwa sababu hafiki, yule mwenye haki anakosa haki. Sasa hapo unajiuliza alaumiwe Hakimu au huyu ambaye hakufika. Mimi nasema tujilaumu sisi kwa sababu hatujawawezesha vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingine unamkuta mtu amepelekwa mbali kule kwetu Malinyi, hakuna anayekumbuka kumpeleka kwenye *refresher course,* hakuna mtu yeyote anayempa *up grading* ya jinsi sheria zinavyokuwa *amended, amendments* hakuna mtu anayempelekea sasa pale ambapo anakosea, yeye anafuata sheria ya miaka ile aliyosoma na ni mzee, kakulia kule, anakwenda kilabuni, anarudi gazeti halioni. Sasa mimi naona kwamba tuwe na mfumo wa kuweza ku-*up grade* ile *skills of knowledge* za

wale watendaji wetu ili na wao wawe *more competent and confidence* anapotoa hukumu yake Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nirudie tu kwamba tusambaze hii Miswada iende mashuleni na pale ambapo tunahitaji kui-*translate* kwa Kiswahili kwenye vijarida vidogo vidogo, tufanye hivyo ili tupeleke basi kwenye vikundi vya akinamama Makanisani, Misikitini ili wananchi waweze kuelewa kwa sababu bila kuelewa haki yake hutaweza kuitafuta na sisi tusipowawezesha kutafuta haki kama ambavyo Serikali yao imeamua kufanya, sasa hivi tutakuwa hatujawatendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAMIS J. NGULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kukushukuru kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada ambao upo mbele yetu. Lakini kabla ya kufanya hivyo naomba kwanza nami niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi zangu kwa familia, jamaa na rafiki wa Mheshimiwa Michael Mussati aliyefariki na naomba familia yake kwa kweli kwa kipindi hiki iweze kuwa na uvumilivu na Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema. Pia naomba nitoe rambirambi zangu kwa Waheshimiwa waliofiwa Mheshimiwa Ntagazwa, na Mheshimiwa Malangalila kwa kufiwa na wake zao na Mheshimiwa Hoogan kwa kufiwa na baba yake mzazi. Mwenyezi Mungu pia awape nguvu na uhimili katika wakati mgumu huu ili waweze kuendelea na maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba nami kuunga mkono Muswada huu uliopo mbele yetu kwa asilimia mia ili niendelee kuchangia. Mahakama katika nchi yoyote ile ndio kioo cha nchi. Mahakama ikifanya kazi yake vizuri ni kwamba utawala unasifika na nchi hiyo inasifika kwamba ina utawala mzuri kumbe tunapokwenda ovyo katika Mahakama basi na utawala wote wa nchi unaonekana kwamba hauendi vizuri. Hii ni kwa sababu ni sehemu muhimu au mahali ambapo haki ya binadamu, haki ya raia au haki ya mtu hutolewa. Sasa haki inapotolewa bila upendeleo wala matatizo basi raia wanaridhika na hapo ndipo wanapoisifu Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria kwa kufikiria kuleta mabadiliko haya ili kuweza kuimarisha sheria zetu na kuweza kuimarisha Mahakama yetu ili iweze kutenda haki kwa raia wetu. Lakini mara nyingi sana tumekuwa tukilalamikia sehemu ya Mahakama au sehemu ya Sheria kwamba Wizara hii haipati fedha za kutosha ili kuweza kuendesha mambo yake na katika kutoa haki mara nyingi sana tumeshaona katika Mahakama zetu vitu vingine hata vitu vidogo vichache vinakosekana. Vinapokosekana Mahakimu wanashindwa kufanya kazi yao. Sasa mimi ningependa kujua tumejipanga vipi katika kuendelea kuboresha Mahakama zetu, kuendelea kuboresha mkono huu wa tatu katika nchi yetu ili nao uweze kufanya kazi vizuri jinsi tunavyotazamia. Maana yake ilikuwa si jambo la ajabu ukakuta Hakimu anakosa hata karatasi za kawaida tu za kuendeshea kesi yake au vitendea kazi vya

kawaida. Sasa, wakati huu tunapokuwa tunajipanga na tunataka turekebishe shughuli hizi ili mambo yaende vizuri tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Mahakama zetu Majaji tunawapangia katika siku tisini aweze kutoa hukumu yake au maamuzi yake, lakini tunajikuta mambo mengi hatujamtekelezea je, tuna uhakika kwamba huyu mtu hatakuwa na sababu za kutueleza kwamba hajafanya hivyo kwa sababu hana hiki wala kile ndio ameshindwa kufanya hili? Ikifika mahali hapo tutamtawala vipi huyu mtu? Akifikishwa katika vikao hivi ambavyo ndio tumempangia katika Kamati hizi au katika Tume na akajitetea namna hiyo je, tutakuwa na lipi la kumwambia? Kwa hiyo, ningeomba basi kabla ya kuanza kumrekebisha huyu bwana na baadaye kuja kuanza kumbana tumrahisishie kazi yake iweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati Waziri wa Elimu alileta marekebisho akitaka *division four* ya Kidato cha nne ifutwe kwa sababu aliona haina kazi. Lakini wakati ule ule alipoleta kwenye Kamati yetu ya huduma za jamii hatukuona mantiki kwa sababu kwanza tukamwuliza hivi katika Wizara hii sasa hivi walimu wameshatosha, vitabu vimetosha, vitu vyote ambavyo vinatakiwa na wakati ule hata madarasa, madawati na kila kitu katika shule kilikuwa kinakwenda shaghalabaghala ili mradi kwamba hakuna vitu vyote ambavyo vinatakiwa kumwezesha huyu mwanafunzi aweze kufaulu. Sasa utakujaje kumfutia *division four* wakati hujampa vitu vyote hivi aweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo nimetoa mfano huo kulingana na hili ambalo tunalieleza hapa. Tutakuja kuwalaumu hawa kwa kazi yao ambayo sasa hivi tunataka tuwabane na tunataka wajirekebishe lakini tuangalie kwamba Mahakama sasa hivi fedha na haitoshi kila wakati tunalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunalalamika, kwa mfano, tukienda kwenye Mahakama za Mwanzo au Wilaya wapo hawa Wazee wa Baraza. Matatizo yao yapo kila wakati ya kutolipwa posho zao kiasi kwamba zinajilimbikiza kwa muda mrefu, wanakata tamaa hata kwenda Mahakamani kuhudhuria zile kesi. Sasa je, pia tumeweza kutengeneza hiyo ili hao wazee waweze kupata fedha zao ili kila wakati waweze kuhudhuria vikao hivi? Kwa sababu hawa wazee walikuwa wanalipwa kila siku waliokuwa wanahudhuria lakini tukafika mahali nafikiri mwaka juzi, tukasema kwamba kwa kila kesi inayokwisha huyu mzee alipwe sh. 1500/=, lakini bado na hiyo ikawa si rahisi kulipwa. Sasa mimi namwomba Mheshimiwa Waziri sambamba na kufanya marekebisho haya, basi Serikali ihakikishe kwamba Mahakama inapewa fedha za kutosha ili kuweza kutoa haki kwa hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tatizo lingine tena katika uteuzi wa Kamati hizi zitakazosimamia Mahakama za Mikoa, Wilaya na Mahakama za Chini kifungu cha 39 na 40. Pale pamoja na kwamba Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya anapewa haki ya kuteua wajumbe wengine pale lakini pia anakuwa Mwenyekiti pale. Tunavyojua ni kwamba wananchi wetu licha ya kufahamu kwamba mkondo wa Mahakama ni kwamba ukishindwa hapa lazima uombe rufaa katika Mahakama inayofuata, lakini unakuta wananchi wetu wa kawaida mambo yao wakati mwingine ni kulalamika kwa Mkuu wa Mkoa au Wilaya. Anaona ameonewa aidha kwenye Mahakama ya Mwanzo au Wilaya

sasa anataka apate maelekezo, anakwenda kwa Mkuu wa Mkoa au Wilaya. Sasa mimi wasiwasi wangu ni kwamba hawa wanapokuwa tena pale kama Wenyeviti wanaweza wakamshauri vipi huyu mwananchi ili aweze kuondokana na yale ambayo ana uhakika kwamba yeye ameonewa wakati Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anarudi tena kwenda kukaa katika vikao hivyo kama Mwenyekiti. Nilikuwa napendekeza kwamba wapo hawa Ma-*RAS* au *DAS* ambao zamani walikuwa wanaitwa Mabwana Shauri, kwa nini wasipewe kuwa Wenyeviti katika vikao au katika Kamati hizo? Nilikuwa nashauri awekwe *RAS* au *DAS* kuwa Mwenyekiti wa Kamati katika Wilaya au Mkoa wake ili angalau kuendelea kumweka Mkuu wa Wilaya au Mkoa awe huru na kwa hiyo aweze kupokea na kushauri wananchi wake lolote lile ambalo atakuwa amekosewa katika Mahakama fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa naliona ni kwamba muda wa siku tisini anazopewa Hakimu pengine awe amekamilisha vitu vyake hivyo, basi kwa sababu hawa watu wakati mwingine huwa wamekaa muda mrefu lionekane hilo linatekelezeka. Kwa sababu kwenye Mahakama, ni kweli Mahakama zinakuwa huru na kwa hili ambalo tunataka tutekeleze angalau uhuru huo wa Mahakama uwe unaulizwa, maana hakuna uhuru usio na mipaka. Mahakama zinakuwa huru kiasi kwamba hata yule wa juu yake au Hakimu wa juu yake anakuwa hana uwezo ule wa kumwuliza lakini sasa tunashukuru kwamba kwa mfano, kama Majaji basi Jaji Mkuu aweze kuwauliza Majaji wenzake labda kesi zinavyokwenda kwa sababu na hiyo inaturahisishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninalosema ni kwamba iwe siku tisini kweli ili watu waweze kupata nafuu ya kuendelea kukaa mahabusu maana ni muda mwingi unakuta na ndio maana tunakuwa na mahabusu wengi kuliko hata wafungwa. Mahabusu wanakuwa wengi kuliko wafungwa kwa sababu kesi haziendi lakini kama kweli tunaamua kuweka siku tisini pamoja na kwamba mimi naziona ni nyingi zingekuwa angalau siku sitini kama ilivyokuwa zamani kwa sababu ukiangalia siku tisini ukajumlisha na zile ambazo pengine huyu mtu tangu ashikwe amekaa muda gani pale kwa kweli tunakuwa tunaendelea kumweka mtu mahabusu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba siku hizo kwanza zipungue angalau zifike sitini ili hawa wafanya kazi na ikiwezekana Polisi ambao kila wakati ndio huwa wanarefusha siku nyingi basi na wao wakabiliwe ili upelelezi uweze kufanyika kwa wakati kwa sababu tukiangalia Hakimu au Jaji anakuwa na sababu za kuendelea kuwa na siku nyingi kwa sababu upelelezi haujamalizika. Siku tisini zimekwisha na unakuta mtu bado hajahukumiwa lakini ukimwuliza Jaji kwa kweli anakuwa na sababu za kufanya hivyo, lakini naomba basi hii iendelee imfuate pamoja na Polisi ili aweze kufahamu kwamba katika siku tisini kama Polisi hajakamilisha upelelezi wake na yeye achukuliwe hatua kwa kurefusha muda huo kwa raia hao. Kwa kweli mimi nilikuwa na haya machache ya kuzungumzia na bila kukawia kwa kweli naomba kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja hii ili tuweze kuboresha Mahakama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Muswada huu na sitachukua muda mrefu kwani yangu ni machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi tumepewa *schedule of amendment* hasa natazama ukurasa wa tatu *amendment (N)* na *(O)* juu ya muda wa kuandika hukumu. Mwanzoni kwenye Muswada muda wa kuandika hukumu ulikuwa siku sitini. Katika Kamati tukakubaliana iwe siku tisini, lakini wakati tunajadili suala hili katika Kamati tuliona kwamba vifungu vyote viwili kifungu cha 27 cha Kanuni za Mwenendo wa Daawa na kifungu cha 311 cha *Criminal Procedure Act,* vyote vimewekwa kwa njia ya kwamba lazima hukumu iwe imeandikwa katika kile kipindi ambacho kimeonyeshwa katika ile sheria. Leo asubuhi msemaji wa Kamati yetu aliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilipendekeza kuwe na *proviso* kwenye hivyo vifungu kwa sababu kiutaalam kama umeweka sharti ni kwamba lazima hukumu itamkwe katika kipindi fulani, lakini sisi wote ni binadamu na tunaishi kwenye dunia na kuna matatizo mengi ya kiutendaji na ya kiafya ya aina aina ambayo yanaweza kuwapata wale watumishi wa Mahakama wakashindwa kuandika zile hukumu kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tulikuwa tumependekeza kwamba kuwe na *proviso* kwamba *judgment* lazima iandikwe katika muda wa siku tisini, lakini kama kuna sababu yoyote ambayo inalazimu kupatikana kwa nyongeza ya muda basi Jaji Kiongozi au *Judge in Charge* apewe mamlaka ya kutoa hiyo nyongeza. Sababu ni kwamba ukisoma hivyo vifungu swali linatokea je, kama Jaji hataandika hukumu kwa siku tisini maana yake nini. Unaweza ukamwadhibu au kumchukulia hatua lakini ile *judgment,* je, nani ataiandika sasa, imeshakuwa time *barred,* kesi itaanza upya au mtu ataachiliwa? Maana yake umesema sharti baada ya siku tisini hakuna mtu mwenye ruhusa ya kuandika ile hukumu, kwa hiyo zile *proceedings* zote ni batili. Kutokana na hilo ndio sababu tukawa tumependekeza kwa sababu wanatumia hilo neno sharti ni lazima kuwe na *proviso* kwamba kuwe na uwezekano wa kuongeza muda kwa sababu ambazo zitatolewa mbele ya mamlaka iliyo juu zaidi ya yule Hakimu au Jaji. Sasa sijui kwa nini Serikali imeamua kuleta *schedule of amendment* bila kuweka hiyo *proviso* kwa sababu huo ni ubishi ambao lazima utatokea Mahakamani, Wakili anayemtetea mshtakiwa anaweza akasimama akasema mshtakiwa wangu aachiwe kwa sababu siku tisini zimepita na hakuna hukumu na mnawajibika kuandika hukumu. Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri asikilize pendekezo lililokuwa kwenye Kamati na alete hiyo *proviso* ili kuruhusu ule muda uweze kuongezwa na mamlaka iliyo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme jambo ambalo, baada ya kusoma huu Muswada kwa kina zaidi nimechanganyikiwa kidogo sababu katika masuala ya *discipline* tunashughulikia *discipline* ya *Judicial Officers.* Katika Muswada huu definition ya *Judicial Officer* imemwondoa Hakimu *Judicial Officer* amekuwa ni Jaji na Wasajili. Mahakimu kwa mujibu wa *definition* iliyo kwenye huu Muswada sio *Judicial Officer.* Hivi ile kazi ambayo Mahakimu wanafanya sio *judicial?* Kama siyo *judicial* ni kazi gani sasa maana wanahukumu na wanasikiliza kesi. Mimi nilikuwa nafikiri nao ni *Judicial Officers.* Sasa hiyo *confusion* iliyotokea ya kuwaondoa wale

kama *Judicial Officers* ndio utaratibu wa kushughulikia discipline yao umekuwa *confused* kwenye huu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye *Judicial Service Commission* wajibu wake, *functions* zake zipo kwenye *part five,* kifungu cha 23. Zile *functions* za hii *Commission* ni pamoja na kuelekeza na kushughulikia masuala ya *discipline* katika Mahakama. Sasa mimi naamini kwamba ile *Judges Ethics Committee* sasa ipo chini ya hii *Commission,* lakini kinachonishangaza ni kwamba ilivyoainishwa katika kifungu cha 23(2), hii *Commission* inayo kazi, naomba nisome: *"Without prejudice to the provisions of the subsection one, the Commission may delegate its functions as follows".* Halafu inataja zile *functions* za ku-*investigate and inquiry into discipline relating to Judicial Officers, investigation and inquiry into discipline relating to Resident and District Magistrate etc, etc.* Ina maana kwamba kazi ya *inquiry* ni kazi ya hii *Commission*. Sasa kama kazi ya *inquiry* ni kazi ya hii *Commission* kwa nini sasa kuanzishwe tena hizi *Judicial Ethics Committees* na kwa nini zianzishwe hizi *Regional Committees* na *District Committees.* Sasa mimi nafikiri kuna mahali ambapo kuna *omission. Spirit* ni nzuri lakini nafikiri kuna *omission* ambayo lazima isawazishwe ili hii sheria ikae vizuri.

Kitu kingine ambacho kilinichanganya kidogo ni kwamba ikiwa tutakubaliana kwamba tunashughulikia *discipline* ya Mahakimu nilikuwa nategemea kwamba hiyo ni *Professional* kwa hiyo ingeshughulikiwa na watu *Professional.* Matatizo ya kikazi ya Kimahakama yanajulikana kwenye hiyo *Profession.* Sasa kuwawekea wanasiasa na watu walioteuliwa na wanasiasa kuwa *disciplinary Board* zao, hatari ni kwamba tutakuwa na umbea mwingi sana katika *level* ya Wilaya na *level* ya Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mtu anaweza akalalamika kwamba ooh Hakimu amechukua wiki mbili kuamua suala la dhamana. Kweli. Mtu anaweza akalalamika Hakimu anasikiliza mno upande wa *prosecution* huenda ikawa ni kwa sababu yule Hakimu ni mkali sana anafunga mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwamba ikiwa tunakubali kwamba hizi Kamati za Wilaya na za Mkoa zinashughulikia *discipline* ya Mahakimu wakiwa kazini, basi tufikirie zaidi kuwaweka watu ambao ni *Professionals* kwenye ile kazi. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea wale Maofisa kwa mfano, kifungu cha *39 composition* ya *"Regional Judicial Committee "*mwisho kabisa kuna *(e) "a judicial officer appointed by the Judge incharge."* Mimi nilikuwa nafikiri huyo ndiye angekuwa Chairman wa hiyo *inquiry siyo Regional Commissioner na Secretary* wake nilikuwa nafikiri angekuwa *State Attonery* ambaye yuko *assigned* kwenye ile zone. *(Makofi)*

Nilikuwa nafikiria pia kwamba kwa sasa hivi tunao Mawakili wa Kujitegemea wamesambaa karibu Tanzania nzima na kwenye *zones* kungekuwa na uwezekano pia kama kulivyo na *disciplinary committee* ya Mawakili na *disciplinary committee* sasa ya Majaji ambayo inahusisha hata *Tanganyika Law Society* pia kuwe na Mjumbe wa *Tanganyika Law Society* kwenye Kamati hizi kwa sababu Mawakili nao wa kujitegemea ni wadau muhimu katika uendeshaji wa kesi katika Wilaya na katika Mikoa na wapo hao Mawakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ombi ambalo nasema tu ikiwa Muswada huu utapita uwe sheria. Ni kweli ni muhimu sana ku-*discipline* Mahakimu wetu na kukiwa na Kamati ambazo zinafanya kazi sawasawa kweli malalamiko mengi sana yatapungua. Lakini malalamiko mengi yaliyoko yanasababishwa na jinsi ambavyo utendaji kazi wa wale Mahakimu unavyozuiwa na nyenzo ambazo wanapewa. Huwezi kumdai Hakimu aandike hukumu haraka wakati anaandikia *proceedings* zake kwenye makaratasi ya mifuko ya *cement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sambamba na kuwataka wafanye kazi vizuri ni lazima tuhakikishe hali yao ya maisha, hali yao ya kikazi inakuwa nzuri la sivyo tutakuwa tunawaadhibu hawa Mahakimu bila makosa yao. Atatakiwa aandike hukumu wakati hana kitabu cha sheria atanukuu wapi? Utasema amelipua hukumu, ameilipua kwa sababu hana vitabu anategemea kichwa chake. Utasema avae vizuri mshahara wake hautoshi kununua nguo. Sasa nafikiri suala la nidhamu ya Mahakimu ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe pia na marupurupu yao na hali yao ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikizingatia kwamba hiyo *proviso* kwenye ile *amendment* ni muhimu. Naomba niseme kwamba naunga mkono hii hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niungane na wenzangu kwa kweli katika kutoa pole sana kwa familia ya mwenzetu Frank Mussati ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu na Mwanakamati mwenzangu kwa kufariki ghafla kwenye ajali ya gari. Niwape pole wananchi wa Kasulu kwenye Jimbo lake na tupeane pole Wabunge. Lakini vilevile wenzangu wengine ambao wamefiwa na ndugu zao wa karibu sana nao naendelea kuwapa pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu katika Muswada huu sina mambo mengi sana ni machache sana sana. Lakini ninavyoona mimi katika Muswada huu kwa kweli unajaribu kujibu matatizo mengi ambayo yalikuwa yanaipata nguzo hii ya dola. Nguzo hii ya dola ilikuwa kama haina mtu wa kuisemea matatizo yake. Lakini nafikiri kwa kuweka sheria hii sasa tutaanzisha Tume na Tume hiyo sasa itajibu masuala yote kama hakuna vitendea kazi au hakuna itaona, kama kuna Mahakimu hawana mishahara mizuri, kama karatasi za kuandikia kesi hakuna, kama hakuna magari, kama hakuna meza na nini. Kwa hiyo, Tume hiyo kwa kiasi kikubwa itajaribu kujibu mambo mengi ambayo yalikuwa yanakosekana. Mimi napongeza na ninaunga mkono kwa kweli sheria hii ipite kwa sababu ndiyo itakayoleta bajeti kwamba kuna kitu gani katika Mahakama ambacho kinawafanya wasitende kazi vizuri, wasisafiri, wasikague, wasilipwe vizuri hata wazee wa Mahakama za Mwanzo hili ndiyo jibu lao. Siyo kuanza kuwauliza Waheshimiwa Wabunge fedha zetu ziko wapi wataiuliza Tume tunayoianzisha hapa. Kwa hiyo mimi nafikiri mambo mengi yatajibiwa baada ya kuanza Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nisemee machache upande wa nidhamu ya Watumishi wa Mahakama kwa kweli mara nyingi watumishi kama walivyosema

wenzangu, mimi ninaelewa watumishi wa Mahakama kwa mujibu wa sheria hii mimi nafikiri ni wote. Lakini kama kuna omission ambayo ameizungumza Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai kwa kweli ni vizuri wakaiongeza, hatuwezi tukapitisha sheria hii ukiwaondoa Mahakimu na Mahakimu ambao mimi nitawazungumza leo hapa hasa ni wa Mahakama za Mwanzo ambao ni kero kubwa sana. Sasa kama tunatunga sheria hatuwazungumzii hao kwa kweli hii sheria sasa ina ubaguzi. Lakini ninavyoliona hili ni lazima watumishi wote wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nidhamu ninayotaka kuizungumzia ni pamoja na maadili ya watumishi hakuna maadili sasa katika Mahakama zetu. Unakuta hata karani naye amekuwa ni Hakimu. Hakimu anatoa dhamana, karani mpaka umpe hela au anaweza kuchelewesha mtu akaenda mahabusu. Sasa hii nidhamu na maadili ya utumishi wa Mahakama iko wapi. Sasa kwa mujibu wa sheria hii mimi nafikiri na lenyewe litatizamwa kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni la Hakimu ambaye anahukumu tu kesi, uki-*appeal* kwenye Mahakama nyingine unaenda kushinda. Sasa huyo Hakimu aliyehukumu kunyonga au kufa au kwenda jela anapewa adhabu gani yeye. Mimi nafikiri katika sheria hii basi tuweke au katika utaratibu watakaojiwekea hii *Commission* namna ya kushughulikia *discipline* na mambo mengine basi waweke na kipengele kwamba Hakimu anayehukumu kesi kushindwa hapa, lakini zikaenda zikashinda huko zikifika tatu huyo Hakimu asimamishwe kazi. Maana yake sasa mtu atahukumu tu watu wanakwenda jela kumbe labda anapata hela au ana matatizo yake mengine. Sasa ni muda gani Hakimu huyu anayehukumu vibaya kesi atachukuliwa hatua na hatua zile ni hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Mahakimu wengi kwa kweli wanaleta kero kabisa na watu wengi wanatumikia vifungo siyo haki kwa hukumu mbaya ya Mahakimu. Lakini Idara hii nayo inasema *my fellow judge, my fellow magistrate was mislead.* Sasa *mislead* unapata adhabu gani kwa ku-*misleading.* Upatikane utaratibu wa kushughulikia huyo anayesema *mislead.* Kama Mkurugenzi wa Halmashauri anakosea mahali fulani tunamwajibisha, huyo Hakimu anayehukumu watu ovyo ovyo wanakwenda kufungwa tunamshughulikiaje? Ni kweli anahukumu mtu labda ana matatizo madogo tu, lakini kwa sababu amepata chochote au ana matatizo fulani, basi anahukumu. Uki-*appeal* unakwenda kushinda na watu wengi wako magerezani wanahangaika kwa tatizo la taaluma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda lingine ambalo nilitaka kulisemea ni la ujumla. Katika vipengele hivi kwa kweli Mheshimiwa Rais tunampa majukumu mengi sana ambayo hayana sababu sana. Sasa mpaka aende kuchagua nani na nani Mheshimiwa Rais ana mambo mengi na makubwa ya kuifanyia nchi hii.

Sasa mpaka aone ni Hakimu gani, Jaji na Mjumbe wa Tume na nani kwa nini mambo yote hayo. Mimi nilikuwa naungana mkono na wenzangu waliosema kwamba Idara hii ijipange yenyewe ijue nani atafaa pale hata ngazi ya Wilaya. Sasa yupo Mkuu wa Wilaya, yuko na *DAS* wake, sasa watu wote unawalundika ofisi moja kwa hiyo

wanaendesha na huyo Mkuu wa Wilaya tena anapewa madaraka ya kuchagua watu wengine anaowaona yeye wanafaa.

Kwa hiyo, *actually hii Committee* ya Wilayani na hata Mkoani ni za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Sasa tumeinyang'anya Mahakama, sasa tuone mahali kama anaweza kuwa Mwenyekiti *DAS* basi ili Mkuu wa Wilaya aweze kukemea basi kitu ambacho atakiona labda katika Wilaya yake vyombo kama hivi vinatenda vibaya au havitendi haki.

Lakini kama ni yeye mwenyewe amekuwa Mwenyekiti sasa atakemewa na nani? Vilevile ngazi ya Mkoa apatikane mtu mwingine basi wa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ili Mkuu wa Mkoa aweze kuwa na madaraka zaidi ya kuweza kukemea au kusahihisha mahali ambapo watu hao wamekosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na mwenzangu kwa kweli kuhusu taarifa ya Tume hata ya Mahakama hii lazima ifike Bungeni tuipate na tuijadili na mienendo ya Mahakimu tuijadili hapa na mienendo ya Majaji tufike mahali Bunge kwa kweli *Okay* Mheshimiwa Rais amemteua mtu fulani kuwa Jaji, lakini tuwe na madaraka na sisi Bunge kwanza kuwapa ridhaa. Lakini vilevile ku-*review performance* yao, kama Jaji anaonekana *bogus* na hakuna chombo cha kumdhibiti, basi sisi Bunge tunaweza kushauri Mamlaka zinazohusika ili aweze kuchukuliwa hatua zaidi. Labda nina mambo mengine mawili ya msingi ya maombi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la dhamana kwa kweli ni haki ya msingi kabisa ya raia wa nchi hii na mambo ya upelelezi yasiyoisha kwa kweli yanaigharimu Serikali. Mtu anakamatwa labda ametishia kuua, kutishia tu kwa maneno au kwa barua anakwenda jela, watu labda wanapigana kwenye klabu cha pombe mmojawapo za kienyeji anaumia kidogo tu, lakini mtu anapelekwa mahabusu kwamba ni jaribio la kuua na upelelezi unachukua miaka kadhaa kabla ya kumalizika.

Sasa hao wapelelezi wako wapi na wana tatizo gani? Kama fedha ya Benki inaibiwa kwa kitaalam kabisa, lakini upelelezi unashughulikiwa miezi mitatu wanapatikana wahalifu na kesi inahukumiwa. Kama waliolipua Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam na Nairobi walishughulikiwa haraka haraka na wakapatikana. Hawa watu wa vijijini wanateseka kwa mambo ya kienyeji kabisa kwa nini tusiwashughulikie, tunawanyima haki. Watu wako Magerezani bila hatia kwa kweli. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nafikiri katika sheria hii tuweke basi tena siku 90 ni nyingi sana mimi nilikuwa nafikiri lakini hizi ni kama za kuandika hukumu. Lakini hukumu haiwezi kuandikwa mpaka upelelezi uishe na kesi isikilizwe. Sasa sijui ndiyo muda wote huo kwamba mtu amekamatwa upelelezi umefanyika, kesi imesikilizwa Mahakamani na hukumu imeandikwa katika siku hizo au maana yake ni nini? Kama katika siku 90 mimi ningefurahi kwamba mtu amekamatwa leo tunahesabu siku 90 hukumu iwe imetoka ningeelewa vizuri sana. Lakini kama ni baada ya kusikiliza kesi sasa Hakimu akae siku 90 anaandika tu hukumu sasa hapo hatuwatendei haki watu.

Kwa hiyo, mimi nafikiri hata Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali na yenyewe ifanye kazi. Sisi kwa upande wa Bariadi kwa kweli tunakwenda mpaka Tabora, tulishaomba *High Court* ifunguliwe Shinyanga na majengo tukatayarisha na kila kitu kipo na Mheshimiwa Waziri analijua hili.

Sasa tatizo liko wapi la kuweka *High Court* Shinyanga. Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou amelalamika watu wanakaa mpaka miaka miwili, mitatu, hakuna Jaji, hakuna fedha za kumpeleka Jaji Kigoma.

Vilevile hata Shinyanga na mimi nilishatoa ombi hapa kama ni matatizo kupeleka *High Court* Shinyanga basi sisi wa Wilaya ya Bariadi angalau tuhamishiwe Kanda ya Mwanza ambapo ni karibu zaidi kuliko kusafiri mpaka Tabora.

Mimi ninashangaa Mwanasheria wa Serikali wa Tabora anafanya kazi gani, kesi ya mtu amekamatwa na mkia wa nyumbu tu, unaupelelezi gani mkia wa nyumbu! Maana yake mambo mengine ni ya kienyeji kabisa. Mpelelezi wa Mkoa ameshakamilisha ametuma faili Tabora, lakini Mwanasheria wa Tabora ana tatizo gani?

Mimi nafikiri Mheshimiwa *Attorney General* huyo Mwanasheria wa Tabora kama kwa kweli ni mzembe basi tummulike tuone uzembe wake uko wapi na achukuliwe hatua. Lakini tunaona kwa kweli *High Court Shinyanga* tunaomba ifunguliwe mara moja ili itupunguzie adha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine labda ni kuweka Mawakili katika Mahakama za Mwanzo. Kwa kweli katika mwenendo wa kesi za siku hizi tukubali tuweke Mawakili katika Mahakama za Mwanzo watu wanashindwa kujitetea, watu wengine hawajui kuzungumza, sheria za Mahakama za Mwanzo zimeandikwa kwa Kiingereza.

Sasa Msukuma wa Meatu kule au wa Mwamapalala pale ataelewa wanazungumza nini? Kwa hiyo, ni vizuri tukaweka Mawakili basi wa kuwatetea. Watu wanahukumiwa bila kujua, hawajui hata kujitetea. Sasa tutahukumu watu kwa kweli tutatenda dhambi kuwapeleka watu jela bila kuwapa haki hata ya kujitetea.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili la Mawakili katika Mahakama za Mwanzo waruhusiwe kuwatetea wananchi ambao wengi wanaonewa lakini wapo na wahalifu, lakini wengi kwa kweli wanaonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Pili, Muswada huu ukikubalika kuwa Sheria naamini kuwa matatizo mengi yaliyopo ndani ya Mamlaka muhimu ya Mahakama yataweza sasa kutatuliwa. Mahakama ni chombo muhimu sana katika nchi yoyote ile. Hivyo unatakiwa kuwe na *efficiency* na pia hadhi yake ipasavyo. Iwe daima ya kiwango cha juu sana.

Hadhi ya Mahakama kwa sasa iko chini sana. Kuna matatizo mengi sana ambayo yako nje ya uwezo wa Mahakama. Lakini kuna matatizo mengi pia ambayo yanatokana na Utendaji mbaya wa baadhi ya Majaji na Mahakimu wa ngazi zote. Matatizo yaliyo mengi ni ya kimaadili hususan rushwa. Inaweza kutoka kuwa Jaji au Hakimu anaandika hukumu mbili tofauti juu ya kesi moja. Hakimu ambayo anaitoa Mahakamani ni ile inayopendelea: *"The highest bidder".* Kwa vile mambo haya ni ya siri inakuwa vigumu sana kudhihirisha kosa hili baya. Watu wanabaki kulalamika na hakuna lolote linaloweza kutokea.

Katika hali hiyo kwa vile Mahakama inalindwa kikatiba na dhana muhimu ya uhuru wa Mahakama basi hali inaishia hapo. Lakini ni wazi dhana ya uhuru wa Mahakama inakuwa *ABUSED* na baadhi ya Majaji na Mahakimu. Hivyo dhana hiyo ya uhuru wa Mahakama inakuwa *ERODED* na kuonekana kwamba haina thamani mbele ya Jamii. Muswada huu unamwongezea Madaraka Mheshimiwa Jaji Mkuu, *Judicial Service Commission,* na kuanzisha Kamati za Maadili ya Majaji na Mahakama. Hivyo sasa Mahakama itakuwa na jukumu na pia uwezo wa kujisafisha. Tunategemea Utendaji mzuri wa Mahakama baada ya kutunga Sheria hii. *"The Judicial Services Act, 2005".* Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mijadala imeishia hapo. Tutakaporudi jioni Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kujibu hoja zenu. Pia ningependa kuwakumbusha ile *Additional Order Paper* ambayo Mheshimiwa Spika aliisema imeshasambazwa na nimeanza kupokea wale ambao wangependa kuchangia Muswada huo wa Sheria ya Uchaguzi. Kwa hiyo, *Order Paper* hiyo ipo na pengine baada ya Muswada huu kukamilishwa basi tutaendelea na huo Muswada mwingine. Baada ya kufika hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06. 48 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudiwa)*

**Muswada ya Sheria ya Serikali, Muswada wa Sheria inayoainisha Masuala ya Kiutawala Kinidhamu ya Majaji, Wasajili na Utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu ya Mahakama wa mwaka 2005**
***(The Judicial Service Bill, 2005)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa fursa hii ili kufanya majumuisho kwa Muswada huu wa *Judicial Service Act, 2005.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja mbalimbali zilijitokeza wakati wa kujadili Muswada huu. Kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja hizo zilizotolewa, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Danhi Makanga. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Mlawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kukubaliana na dhana na malengo ya Muswada huu. Machache nitakayotolea maelezo ni kwanza hoja za Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imependekeza kuwa juhudi za kuandaa sheria ya maslahi ya majaji zisiwe za mdomo bali ziwe za vitendo. Tunakubaliana na hoja hii, ningependa pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa zoezi hili ni sehemu ya maboresho ya sekta ya sheria. Kuhusu Ibara ya 26 (2)(c), kuhusu Ibara hii Kamati haikubaliani na mapendekezo kuwa Jaji Mkuu ateue Majaji watatu wa Mahakama Kuu kwa misingi ya kijiografia na Kanda za Mahakama na kushauri kuwa maneno haya yafutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na hoja hii na maeneo hayo yamefutwa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la mabadiliko. Ibara ya 39 na 40 katika Ibara hizo Kamati imependekeza kuwa wajumbe watatu wanaoteuliwa na Mkuu wa Mkoa wathibitishwe na Waziri na wale wanoateuliwa na Mkuu wa Wilaya wathibitishwe na Mkuu wa Mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraka ya uteuzi ni ya *Judicial Service Commission* kama kuna hoja ya kuthibitishwa basi Tume yenyewe itafanya hivyo hivyo. Kamati pia imependekeza kuwa fungu la kuhudumia Kamati hizi litoke Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba moja kwa moja na iwasialiane na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba iko mbali na kazi hizi ni vyema basi Ofisi za Mikoa zikapewa jukumu hilo.

Aidha, muundo wa Kamati za Maadili zimezingatia mazingira halisi ya udhibiti wa nidhamu ya Mahakimu, uzoefu umeonyesha kwamba kama kusipokuwepo wajumbe kutoka nje ya Mahakama inachukua muda mrefu kukamilisha uchunguzi wa malalamiko ya nidhamu na kwa kweli mara nyingi Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakilalamikia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 45 na 46 Kamati imependekeza Serikali iangalie upya vifungu hivyo na jinsi ya kuviboresha. Kuhusu kifungu cha 28 kimerekebishwa ili utoaji huduma uwe mapema iwezekanavyo lakini usizidi siku 90

isipokuwa kwa kutolewa taarifa kwa pande zote zinazohusika. Kuhusu hoja kwamba sheria zinazohusu jinai na mwenendo wake zifanyiwe mapitio ili zisiwanyime watu haki zao hasa katika ngazi ya kukamatwa na upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zetu za jinai zilifanyiwa mapitio mwaka 1985 ili kukidhi matakwa ya haki za binadamu na baada ya haki hizo kuingizwa katika Katiba. Hii ikiwa ni kwamba mtuhumiwa wa kosa la jinai afunguliwe mashtaka ndani ya saa 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria zitamke wazi kuwa Tume ya Huduma ya Mahakama *(The Judicial Service Commission)* kama chombo kipya cha kusimamia masuala yote ya ajira na nidhamu ya watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama siyo Tume ya Huduma ya Mahakama, Tume hii haishughulikii ajira za Majaji kwa sababu Majaji wanateuliwa kwa mujibu wa Katiba. Tume inashughulikia watumishi wengine wa Mahakama ambao siyo Majaji, pili Majaji wana utaratibu wao wa Kikatiba kuhusu nidhamu. Kazi ya Tume ni kutoa ushauri kuhusiana na masuala ya nidhamu pamoja na kupokea malalamiko ya nidhamu ya Majaji. Muswada huu haupendekezi utaratibu mpya ila unaziba pengo.

Aidha, si kweli kwamba sheria hii imewaacha Mahakimu na tafsiri ya *Judicial Officers* kama ilivyofafanuliwa katika tafsiri ya sheria Ibara ya 3 ambayo ina lengo la kuwatambua Maofisa wengine ambao si Mahakimu au Majaji.

Suala la Mahakama Maalum ya Katiba, kazi ya Mahakama Maalum ya Katiba si kutafsiri masuala yote ya Katiba, bali kazi maalum ya Mahakama hiyo ni kutafsiri Katiba iwapo tafsiri au utekelezaji wa Katiba unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Chombo hiki kwa muundo, wake hakiwezi kumudu matakwa ya wananchi wote kwenda mbele yake. Utaratibu wa sasa ambao Mahakama Kuu husikiliza mashauri ya watu kuhusu Katiba inafaa, kwa sababu Mahakama Kuu ziko karibu zaidi na watu.

Kuhusu hoja kwamba hakuna utaratibu wa wazi unaoruhusu watu kuhoji Muungano ukweli ni kwamba Ibara ya 26(2) ya Katiba inaelekeza kwamba kila mtu ana haki ya kuchukua hatua kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi. Muungano ni suala la Kikatiba, hivyo kila mtu anaweza kutetea Muungano kupitia Mahakama zetu. Mahakama Maalum ya Katiba haijawahi kushindwa kufanya kazi kwa sababu ya mgogoro wa Kikatiba, matangazo yote aliyoyataka Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa ni migongano ya kawaida.

Kuhusu kwamba Serikali haijatekeleza masharti ya Ibara ya 128 (4) ya kutunga sheria ya utaratibu wa uendeshaji wa Mahakama Maalum ya Katiba. Kutotungwa kwa sheria hiyo hakumaanishi kwamba Mahakama Maalum ya Katiba haiwezi kushughulikia matatizo ya Katiba pindi yanapotokea. Ibara hii ya 128 inatoa utaratibu mbadala wa namna ya kushughulikia matatizo hayo pindi yanapotokea. Hoja ya kwamba si vizuri kuendesha nchi kwa muafaka, utawala mzuri ni ule unaoweka misingi imara kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya muafaka kutokuwa na msingi wa sheria ukweli ni kwamba muafaka ulihusu mambo yaliyopo katika Katiba na Sheria zetu. Utekelezaji wa muafaka ulihusu mabadiliko katika Katiba na Sheria hizo na utekelezaji wake, hivyo muafaka una msingi wa kisheria. Aidha, hoja ya kwamba taarifa za utendaji kazi wa Mahakama ziwe zimejadiliwa na Bunge ili kudhibiti udhaifu uliopo Mahakamani kwa mfano rushwa, ucheleweshaji kesi usio na msingi. Ukweli ni kwamba Bunge huhoji utendaji wa Mahakama kupitia Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba lakini vile vile wanafursa ya kuhoji masuala mbalimbali Bungeni. Lakini ikumbukwe kuwa Kanuni za Bunge zinakataza Bunge kuhoji kesi ambazo bado ziko Mahakamani na hazijatolewa maamuzi.

Hoja kwamba Ibara ya 7 (1) inaifanya Mahakama isiwe huru kama Tume ya Huduma za Bunge kwa vile wajumbe watatu wa Tume hiyo wanateuliwa na Rais kwamba Rais ateue Mjumbe mmoja wa Tume na Jaji Mkuu ateuwe wajumbe wengine wa Tume.

Hoja hii haizingatii ukweli kwamba Rais hawateui Wajumbe hao kama Mkuu wa Serikali bali kama Mkuu wa dola *(Head of State).* Rais anapofanya kazi zake kama Mkuu wa dola hazingatii maslahi ya Serikali peke yake bali anazingatia maslahi ya dola kwa ujumla. Katika hili anazingatia zaidi maslahi ya Mhimili wa Mahakama. Kumpa Rais madaraka ya kuteua mjumbe atakayezingatia maslahi ya Serikali ndiko kutakakoathiri uhuru wa Mahakama.

Kuhusu hoja kwamba haitoshi kuweka muda maalum kwa Majaji na Mahakimu kutoa hukumu bila kuwawekea muda wa kuendesha mashtaka na upelelezi, ukweli ni kwamba upo utaratibu katika sheria unaelekeza kwamba kesi zisikilizwe katika muda wa siku 60.

Hoja kwamba sifa za wajumbe wa Tume wanaoteuliwa na Rais zitajwe katika sheria, imezingatiwa katika mabadiliko ya kumi na nne ya Katiba iliyopitishwa jana. Wajumbe hao hawapaswi kuwa wanasiasa, lakini pia hoja kwamba wengi wa wajumbe katika Tume wanateuliwa na Rais imezingatia ukweli kuwa wengi wao wana ofisi zao *(Ex-official)* na ni Majaji ambao wana *security of tenure of office.*

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kuwa mikakati ya Serikali kuboresha Mahakama zetu. Hoja hii ni ya msingi sana. Hadi sasa katika mpango wa kuboresha sekta ya sheria, Serikali inao mkakati wa ujenzi wa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo pale ambapo hazipo na kuzikarabati zile zilizo katika hali mbaya. Mpango huu ni wa muda mrefu hadi pale hali ya Mahakama zetu zitakapokuwa nzuri. Aidha, kuhusu kufunguliwa kwa Kanda za Mahakama Kuu katika kila Mkoa, Serikali inakubaliana na hoja hii. Upo mpango wa muda mrefu wa kuendelea kufungua Kanda za Mahakama Kuu katika kila Mkoa. Zoezi hilo litafanyika kila wakati hali ya uchumi itakapo ruhusu.

Hoja kwamba Rais akitunga Kanuni kwa ajili ya Tume ataingilia uhuru wa Mahakama na kadhalika.

Kuhusu hoja kwamba madaraka ya Rais kufuta au kuanzisha ofisi ya Mahakama katika mabadiliko ya 14 ya Katiba yaliyopitishwa jana Bungeni, hili limeweka masharti ya kuendelea kuwepo Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ambapo Mahakama Kuu inapaswa kuwa na kiwango cha chini cha Majaji 35 wa Mahakama ya Rufani wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hoja mbalimbali zilizohusu Muswada huu sasa naomba nijielekeze kwenye hoja za jumla.

Imetolewa hoja kwamba Mahakama ipewe fedha za kutosha za kununulia vitendea kazi ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Matatizo mbalimbali yanayozikabili Mahakama zetu ikiwemo ufinyu wa Bajeti yanafahamika. Serikali kama ambavyo imekuwa nikizungumza mara kwa mara humu Bungeni inachukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuendelea kuongeza Bajeti ya Mahakama kadri ya hali ya uchumi inavyoruhusu.

Suala la Mawakili waruhusiwe kuwatetea wananchi katika Mahakama za Mwanzo, Serikali kwa sasa ipo katika mpango wa kuboresha Mahakama. Katika mkakati huu sifa za Mahakimu wa Mahakama za mwanzo zimepandishwa ili Mahakimu wenyewe wenye uelewa mkubwa zaidi wa kisheria waweze kuajiriwa. Sifa hizo ni Stashahada ya Sheria badala ya Cheti cha Sheria, hivyo tutakapokamilisha utaratibu wa kuwapata Mahakimu wenye sifa hizo katika Mahakama za Mwanzo kote nchini tutaangalia utaratibu wa kuwaruhusu watetezi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu kuwasilisha jedwali la orodha ya marekebisho mapema, kabla sijamalizia majumuisho ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge napenda kuchukua fursa hii kutoa ufafanuzi kuhusu taratibu za kuwasilisha jedwali la marekebisho katika Bunge. Hili ni suala ambalo limejitokeza mara mbili na amelisemea kwa uchungu Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba upo utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, inaelezea kwamba: “Mara baada ya Waziri au Mbunge mwenye Muswada kuwasilisha hoja ya Muswada kusomwa mara ya pili, Mwenyekiti wa Kamati aliyeteuliwa kwa ajili hiyo, atatoa maoni ya Kamati yake kuhusu Muswada na kama Muswada unaohusika siyo Muswada wa Serikali, msemaji wa Serikali atapewa nafasi hiyo ya kutoa maoni ya Serikali juu ya Muswada huo.”

“Iwapo katika hatua hii Waziri anataka kufanya mabadiliko katika Muswada huo kutokana na ombi lililofanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (6) au kwa sababu nyingine yoyote, basi atamjulisha Mwandishi Mkuu wa Sheria ili atayarishe, na Katibu atamgawia kila Mbunge...”

Kanuni ndogo ya sita ndiyo inayoelezea wakati gani jedwali la orodha ya marekebisho inapotayarishwa, kanuni hiyo ndogo inaeleza kwamba: “Mjadala wakati wa Muswada wa Serikali kusomwa mara ya pili utahusu ubora na misingi ya Muswada huo

tu. Lakini Mbunge yeyote aweza, wakati wa mjadala huo kumuomba Waziri afanye mabadiliko katika Muswada, ama mabadiliko ya jumla au yale atakayotaja Mbunge."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hii haitoi fursa ya kugawa jedwali la orodha ya marekebisho mapema kabla Muswada haujawasilishwa, wakati wote kabla ya muda huo lolote linaweza kubadilika na hakuna anayeweza kuhoji kwa nini jedwali limebadilishwa. Hivyo basi haikuwa sahihi kuhoji utaratibu ambao wote tunaufahamu, nichukue fursa hii kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu wasome na kuzielewa Kanuni hizi kama anavyotuasa Mheshimiwa Spika mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujafikia hatua inayofuata, napenda kuchukua fursa hii kusema ya kuwa kwa sababu wengi mlikuwa kwenye Kamati za Bunge, kumetolewa *Order Paper* ya ziada. Nadhani mmeiona na kuna Muswada ambao utaletwa punde tu baada ya kukamilisha hatua zote a Muswada huu uliopo hivi sasa.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria Inayoainisha Masuala ya Kiutawala na Kinidhamu ya Majaji Wasajili na Utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu ya Mahakama wa Mwaka 2005 *(The Judicial Service Bill, 2005)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pengine kabla Katibu hajaanza Muswada huu una Ibara 46, ni Ibara nyingi kwa hiyo, kutokana na uendeshaji ambao utatupa muda zaidi kwa mambo mengine nakusudia kuwahoji kwa sehemu. Kwa hiyo mtu yeyote ambaye anadhani ana hoja kwa sehemu hiyo na vifungu vyake asimame apate nafasi aweze kuuliza.

Kichwa cha Muswada

*(Kichwa cha Muswada kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 1

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

**MHE. DR. WILLBROD SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi. Katika Ibara ya 4 ningeomba ufafanuzi kidogo kutoka kwa Waziri. Hoja ya Mahakama Maalum ambayo tulitaka iwe sehemu ya Ibara hii ya 4 angalau tuelezwe kwamba utaratibu huo sasa unakuwaje, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa ujumla tu. Lakini sisi tulileta hoja kwamba Muungano sasa umepanuka, hoja zimekuwa nyingi wakati sasa umefika wa kuwa na Mahakama Maalum.

Sasa Waziri amejibu kwa kifupi kwamba hoja hizo zinaweza kujibiwa katika Mahakama ya kawaida. Sasa mimi sijaridhika na hilo ningependa Waziri anieleze vizuri, kwa nini basi katika Katiba tunakuwa na Mahakama Maalum na ni kwa masuala yanayoletwa na Serikali na Serikali tu. Hoja yetu ni kwa nini wananchi wa kawaida, taasisi zisiweze kuhoji maswali juu ya Katiba inapofikia masuala ya Muungano? Hii ndiyo hoja yetu na utaratibu ulioko katika sheria za kawaida za kuhoji kupitia Mahakama ya kawaida utaratibu ulivyo mgumu. Lakini tungekuwa na Mahakama Maalum watu wanajua hivyo, taasisi zinajua hivyo na tuna hakika mambo mengi yangepata ufafanuzi katika Mahakama hiyo. Sasa Waziri anaweza kutuambia kwamba je, suala hilo liko open kwa mjadala au limefungwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante, pengine kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri utanisaidia unaposema hiyo ndiyo hoja yetu, nini maana yake? Niliyekuona ni wewe.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ilitoka kwenye Kambi ya Upinzani na ndiyo ninaiwakilisha sasa katika hii kwa sababu ndiyo hoja ililetwa kama Kambi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu utaratibu maana hapa tunashughulikia Muswada unaohusu uendeshaji wa shughuli za Mahakama. Hoja anayoitoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, haiusiani kabisa na Muswada huu. Hilo ni la Katiba na suala la Katiba, Kamati yako ilihitimisha jana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nakubaliana na *AG* maana ni suala la Katiba na hili halihusu Katiba kwa hiyo, pengine utafute namna nyingine. Waheshimiwa Wabunge nadhani mnataka kusema kwa sababu jana alitoka nje alijinyima nafasi ya kusema haya kule jana. Kwa hiyo, nadhani kama una lingine unaweza kulisema lakini kwa hili tuishie hapa.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana katika marekebisho halikuwepo ndiyo maana katika tafsiri hii tulitaka kuleta hoja kwa maana ya kwamba iingie kwenye kumbukumbu ifanyiwe kazi. Hii ndiyo utaratibu kwamba hoja inapotolewa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge labda hawajui utaratibu. Katika hoja yoyote inayotolewa Serikali hupata nafasi ya kupokea hoja na vinginevyo haina namna ya kupata hoja zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa kama nilivyosema jana hakupata nafasi angeweza kuhoji hili lingejibiwa.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Ni kwenye Ibara ya 17 kama ilivyorekebishwa kuhusu yale marekebisho kipengele (e) naomba ufafanuzi kwenye mstari wa pili kutoka chini kuna faini ambayo haizidi shilingi mia nina fikiri Serikali ilikuwa na maana ya shilingi 100,000/=.

**MWENYEKITI:** Nani anajibu *Attorney General* au Waziri? Mheshimiwa *Attorney General.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwa macho yake makali na mapana, ni kweli inapaswa iwe shilingi 100,000/= nashukuru sana. Tunaiona kwenye *schedule of amendments* inasomeka: *"not exceeding one hundred shillings,* kwa hiyo isomeke: *"not exceeding one hundred thousand shillings. (Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Badala ya shilingi 100/= inakuwa shilingi 100,000.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 45

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu vifungu vyote viwili 45 na 46.

Katika *schedule of amendment* ya kwanza muda ambao Majaji na Mahakimu walikuwa wamepewa kwa kuandika hukumu zao ilikuwa siku 90 na hii ilikuwa kwa makubaliano kati ya Serikali na ile Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala.

Sasa ugomvi ulikuwa tu pale ambapo hakukuwa na uwezekano wa kuongeza huo muda kwa sababu ambazo zinaridhisha. Sasa naishukuru Serikali imesikia kilio changu cha kutoa hiyo nafasi ya kuongeza huo muda. Lakini kwa haya marekebisho yaliyokuja sasa inaonekana kwamba wamepunguza tena muda wa kutoka siku 90 kuja siku 60. Mimi nilikuwa nafikiri hapo ni *oversight* katika kurekebisha, ningeomba maelezo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitafakari suala hili tuliona tuweke ile *proviso* ambayo ilikuwa imeombwa na ambayo na sisi Serikali tulikuwa tumekubali kuifanya. Lakini kwa sababu dhana nzima ni kuwa ndani ya zile siku 90, tukasema tuanze na ile ngazi ya kwanza ambayo 28 (1) ili aweze kuandika hukumu baada ya kusikiliza pande zote aweze akaandika hukumu hiyo ndani ya siku zisizozidi 60.

Sasa kama kutakuwa na tatizo kwamba sitaweza kukamilisha uandishi wa hukumu ndani ya siku 60 ndiyo tunapendekeza sasa katika Ibara ndogo ya (2) kwamba amtaarifu Jaji Mfawidhi wa eneo au kama ni ngazi ya chini, Hakimu Mfawidhi wa Mkoa na hivyo hivyo wa Wilaya kwamba ana tatizo. Sasa akishapata taarifa hiyo atumie ule mwezi mmoja kukamilisha kile ambacho alipaswa akifanye. Kwa hiyo, bado ni zile siku 90 lakini tumefanya iwe ni kwa sababu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, baada ya kuongezewa huo muda akishindwa ndiyo anaangukia katika utaratibu ambao unapendekezwa kwenye Muswada kwamba achukuliwe sasa hatua zingine. Hiyo ndiyo *scheme* ambayo tumeona inaweza ikatusaidia ku-*deal* na hili. Nakushukuru sana.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliokuwa mbele ya Bunge asubuhi ulikuwa unapendekeza Jaji achukue siku 90. Lakini mgogoro ulikuwa kwamba baada ya zile siku 90 hakukuwa na njia ya kuokoa ile hukumu kwamba mtu angeweza akasimama akasema sasa kila kitu ni batili na kutata kuwe na njia ambayo ile hukumu ingeweza ikaokolewa. Sasa hatukuwa na ubishi juu ya zile siku 90 alizopewa, lakini tulikuwa tunasema baada ya zile siku 90 apewe muda kwa maelezo, aandike ile hukumu ndiyo ilikuwa dhana ya asubuhi kwamba *basically* ziwe siku 90 kwanza, baada ya siku 90 ajieleze na apewe muda.

Sasa wameamua kutoa muda wa siku 30, ni sahihi kabisa. Lakini pamoja na hayo sasa ikishakuwa *breach* ya *code of ethics* nini zaidi? Je, kutakuwa na hukumu au tutaanza upya? Sasa kuna masuala hayo mawili ambayo hayajajibiwa kitu tulichopata sasa ni kupunguziwa ule muda na kusema kwamba ni *breach of judicial ethics.* Lakini sasa mimi nilikuwa nafikiria zibaki zile siku 90 apewe siku nyingine 30 kama ni kuadhibiwa sasa aadhibiwe baada ya zile siku 30 halafu itamkwe kwamba ile *record* itapelekwa kwa Jaji au Hakimu mwingine ili iandikiwe hukumu. Mimi nilikuwa nafikiria kungekuja kitu kama hicho.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Watanzania na tuliisikia pia hata kwa viongozi humu ndani ya Bunge ya kusema ni vizuri Mahakimu wetu na Majaji wetu wakimaliza kusikiliza pande zote waandike hukumu, hiyo ndio kauli. *(Makofi)*

Tumejitahidi sana upande wa Serikali kusikia kilio hicho na ndiyo maana tumekuja na hii *scheme* kwamba ni vema hukumu hizi zikaandikwa kwa wakati. Ibara ndogo ya (3) ndiyo inafungua mlango kwa hayo ambayo Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, anasema nini kiwe.

Sasa tunaamini huyu Hakimu ataiandika hii hukumu kama hana tatizo la ugonjwa ambao unamfanya asiandike hukumu, kwa sababu hakuna mtu anayependa kupelekwa kwenye vyombo hivi ukashughulikiwe. Tunaamini ataiandika kwa hiyo, tulikuwa tunafikiria kwamba kwa mapendekezo haya, acha Kamati yako ituruhusu tuone kama itafanya kazi, kama haifanyi kazi tutarudi Bungeni kusema tunataka tuionyeshe tena kwenye eneo hili na matatizo yaliyotusibu ni haya na haya. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mimi nilikuwa naiomba Serikali kwa sababu mimi ndiyo nilikuwa Mwenyekiti wa kikao siku hiyo, tukishakubaliana kwenye Kamati, tena kuja kubadilisha inakuwa ni vigumu sana kwa sababu tulikubaliana siku 90 hiyo *proviso* tulikuwa tumeiomba hizo siku 90 na tuliomba nyongeza ya siku zingine 30. Sasa nilikuwa naishauri sana Serikali kwa kweli tukishakubaliana kwenye Kamati kubadilisha ghafla inatuletea shida sana, maana kazi yetu kuchambua Miswada na inapokuja hapa ni tayari tumeshakubaliana na Serikali kwenye Kamati. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sina uhakika, nitampatia nafasi aweze kujibu. Lakini sina uhakika lazima Kamati zetu ziruhusu nafasi ya mabishano yaani nafasi ya kutokukubaliana. Mnaweza kwenye Kamati mkajadili, mkafikia muafaka lakini pengine mkairuhusu Serikali iende na hicho wanachoamini. Hapa ndiyo waamuzi wa mwisho. Nadhani hilo ni vizuri mulielewe. Sasa hiyo *sympathy* ambayo mngeitaka Kamati hii, ikubali ni hoja mtakazozileta, lakini na Serikali nayo ina haki pamoja na maelekezo ya Kamati yenu, lakini mnayo haki ya kuleta Bungeni wanachotaka kuleta.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, nitawapa wajibu wenyewe. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba nataka kwenda tofauti dhidi ya mawazo ya wengi, lakini kama mtu ambaye niko Mahakamani karibu siku nne, tano kwa wiki naomba ieleweke wazi, ninavyoona kule Mahakamani, Jaji, anakuwa na mafaili 20 kwa siku ya kusikiliza. Hakimu anakuwa na mafaili 30 mpaka 50 ya jinai na ya madai ya kusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yaki-*mature* akatakiwa aandike *judgment,* tutafika hatua ambayo Majaji watakataa kupokea kesi kwa sababu watashtakiwa au wote tutawafukuza kazi. Sasa lazima tuwe *realistic* tukichukua maamuzi ya kisiasa kazi ya Mahakama itaisha, hakuna mtu atakayekuwa tayari kuwa Jaji, hakuna mtu atakayekuwa tayari kuwa Hakimu kwa jinsi ninavyoona kule Mahakamani mimi. Tusiwe *utopian* ni ukweli ulio wa hakika!

Nendeni pale Mahakama ya Kisutu Dar es Salaam, Waheshimiwa Wabunge, muone kazi zilizovyo pale, watu wanapata *stroke* kwa ajili ya kazi ya Ujaji. Sasa tukiamua kuwatungia tu sheria ndiyo sheria itakuweko lakini tutawafukuza kazi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, pamoja na hizo *concerns* zake. Lakini haya ni masuala ambayo tumezungumza na Kamati. Lakini la msingi zaidi ni kwamba mapendekezo hayo yametokana na Kamati ya Jaji Mroso, iliyoteuliwa na Jaji Mkuu mwenyewe na tumewapa fursa Mahakama kuzungumza hoja hizi zote. Kwa hiyo, wenyewe wanaafiki haya. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 46

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali l
Jedwali 2
Jedwali 3
Jedwali 4

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo natoa hoja kwamba Muswada wa *Judicial Service Act 2005* ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Muswada huo umepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya *agenda* inayofuata namwona Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na kitabu chake cha Kanuni.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba kupitia kifungu cha 55(3) naomba mwongozo wa Spika. Alipokuwa ana-*windup* Waziri, alieleza kwamba kugawa *(schedule of amendment)* nakala ya mabadiliko inatolewa wakati wa hotuba yake. Kwa kifungu alichotumia cha 70 (3) na ambayo ndiyo ilikuwa ombi letu kifungu 70(3)(b) kinataja ifuatavyo; “Nakala ya orodha ya mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa. Endapo orodha ya mabadiliko hayo itatayarishwa, basi yaweza kuambatishwa kwenye orodha ya shughuli.”

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu ni kwamba hotuba inagawanywa wakati unakwenda kujiandaa kutoa hotuba yako kama Kambi ya Upinzani, hupati nafasi ya kumsikiliza Waziri, hupati nafasi ya kufanya marekebisho, hupata nafasi ya kuyafanyia mabadiliko yale uliyoandika. Lakini Kanuni inataka yatolewe wakati wa kutoa *Order Paper.*

Sasa ombi letu angalau hilo pamoja na kwamba hata wakati wa *Order Paper* bado ni mfupi, lakini angalau tupewe wakati wa *Order Paper* mtu akiingia ndani ana *Order Paper* anafanya marekebisho. Lakini siyo wakati anangojea kwenda kupanda kwenye *pulpit* na kanuni ndivyo inavyosema. Kwa hiyo, alichosema Waziri si sahihi sana ukifuata Kanuni ya 70(3) (b).

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naona umemaliza na Kanuni iko wazi na watu wa Serikali na Mheshimiwa Waziri wanafahamu, hiyo Kanuni inavyoeleza. Sasa kwa sababu unazungumzia yaliyopita basi tuwatake kwamba baadaye waweze kutoa hiyo *Order Paper* mapema. Lakini kama huu Muswada unaokuja sasa hivi *Order Paper* imetolewa mchana huu huu.

Kwa hiyo, kama kuna *amendments* naona zimeshatolewa mchana huu huu. Kwa hiyo, *Order Paper* na *amendment* zimekuja wakati mmoja. Lakini vizuri kweli kuwakumbusha wenzetu wa Serikali ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge, hiyo haki kujadili basi itolewe wakati wa *Order Paper* na *amendments* zake, *unless* hizo *amendments* zinatokana na mjadala mkali wa humu ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama humu ndani kuna mjadala na mapendekezo mbalimbali Serikali wakikubali mapendekezo wana haki ya kuleta hiyo *amendment.* Kwa hiyo, pande zote mbili ni sahihi. Sasa *agenda* inayofuata, Katibu. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005
### *(The Electoral Laws Miscellenious Amendments Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi wa mwaka 2005 *(The Electoral Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2005)* sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo, sheria ya kwanza ni Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 *(The Elections Act 1985)* na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa *(The Local Authorities Election Act)* sheria namba (4) ya mwaka 1979.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya ni mfululizo wa marekebisho ambayo yanapendekezwa na Serikali ili kuziboresha zaidi Sheria za Uchaguzi kufuatia kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha Tume ya Uchaguzi kuendesha na kusimamia uchaguzi kwa ufanisi zaidi na kwa wakati ili kuondoa kosoro na mapungufu yaliyopo katika Sheria za Uchaguzi.

Aidha, marekebisho haya yanakusudia kuanisha na kuboresha taratibu za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani katika hatua ya kuandikisha wapiga kura ikizingatiwa kuwa uandikishaji wa wapiga kura kwa chaguzi zote unafanyika kwa pamoja na unaendeshwa na kusimamiwa na mamlaka moja yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuondoa pendekezo lililokusudia kubadili muundo wa Tume ya Uchaguzi, ili kuingiza uwakilishi wa vyama vya siasa kupitia mabadiliko ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, marekebisho yaliyokusudiwa kufanywa katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 kwa sababu hiyo hiyo, sasa yameondolewa. Kwa maneno mengine, muundo wa Tume ya Uchaguzi ulioanishwa katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 ambacho msingi wake ni Ibara ya Katiba ya Nchi, utabaki kama ulivyo ili kulinda uhuru wa chombo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 17, 18 na 19 vya Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, inapendekezwa vifanyiwe marekebisho ili kuweka utaratibu unaofaa na usio na usumbufu kwa wapiga kura utakaowawezesha watu wafuatao kupatiwa vitambulisho vingine vya kupigia kura.

Kundi la kwanza, ni wananchi watakaopoteza kadi zao za kupiga kura au ambao kadi zao za kupigia kura zitakuwa zimeharibika.

Kundi la pili, ni wananchi watakaobadilisha makazi kutoka Kata au Jimbo moja la uchaguzi kwenda katika Kata au Jimbo lingine.

Kundi la tatu, ni wananchi watakaolazimika kubadilisha kumbukumbu zao kwa mfano wale watakaobadili majina yao rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kwamba endapo wananchi katika makundi niliyoyataja watawasilisha maombi kwa ajili ya kupewa kadi nyingine kwa sababu hizo maalum, basi Maafisa Waandikishaji baada ya kuridhika kuwa wahusika bado wanazo sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura watakiwe kuandikisha taarifa za watu hao na kuwapatia kadi nyingine za kupigia kura. Hiyo ndiyo shabaha ya msingi ya pendekezo hili.

Aidha, wahusika kabla ya kupatiwa kadi nyingine watalazimika kurejesha kadi zao za awali isipokuwa pale ambapo kadi ya kupigia kura itakuwa imepotea. Marekebisho haya yataiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kubadili na kuwa na kumbukumbu sahihi zilizo kamili za watu ambao watapatiwa kadi nyingine za kupigia kura kutokana na sababu zilizotajwa.

Hivi sasa mtu anayehama kutoka Kata moja kwenda Kata nyingine au kubadili kituo alipojiandikisha kupigia au kubadilisha taarifa zake anaweza kupatiwa kadi nyingine ya kupigia kura baada ya taarifa zake kuwasilishwa kwenye Tume ya Uchaguzi na kadi kuandaliwa na baadaye kutumwa kwa Afisa Mwandikishaji ili ampatie mhusika kadi yake. Huu ndiyo utaratibu wa Sheria wa sasa. Kwa wale ambao watakuwa wamepoteza kadi zao Sheria inataka wapewe nakala ya kadi hizo yaani *duplicate voters card*. Imebainika kuwa utaratibu huu ni mrefu na unaweza kuleta usumbufu na hata kuwakatisha tamaa wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kifungu cha 35(f)(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, kifanyiwe marekebisho ili kuwataka Wasimamizi wa Uchaguzi kuzingatia utaratibu uliopo ndani ya Sheria hiyo unaowataka wayabandike kwanza kwenye ubao (ku-*display*) matokeo ya uchaguzi wa Rais katika Jimbo la Uchaguzi kabla ya kuyatuma matokeo hayo kwenye Tume ya Uchaguzi yaani kuyatuma Makao Makuu. Hiyo ndiyo Sheria inavyotaka.

Inapendekezwa katika marekebisho haya kuweka mkazo huo, *subject to the provisional of that clause.* Mkazo huu unawekwa kupitia marekebisho haya kwa madhumuni ya kuepusha uwezekano wa mgongano wa taarifa za matokeo ya uchaguzi wa Rais yaani zile zilizotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Uchaguzi na zile zinazotumwa kwenye Tume ya Uchaguzi.

Vile vile katika Fungu la 35(f)(7) inapendekezwa lifanyiwe marekebisho ili kuipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, uwezo wa kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa Majimbo ya Uchaguzi ambayo yatakuwa yamekamilisha kuhesabu kura na kuwasilisha taarifa hizo kwa Tume ya Uchaguzi badala ya kusubiri hadi matokeo ya nchi nzima kuwasilishwa kwenye Tume ya Uchaguzi. Kwa sasa Tume inatakiwa kutangaza matokeo baada ya kupokea matokeo ya Majimbo yote ya Uchaguzi. Hali hii huisababishia Tume kuchelewa kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais kwani uzoefu wa chaguzi zilizopita unaonyesha kuwa matokeo ya uchaguzi kutoka baadhi ya Majimbo huchelewa kuifikia Tume kutokana na hali mbaya ya mawasiliano na migogoro inayojitokeza katika kuhesabu na kujumlisha kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini pendekezo hili litaepusha shutuma ambazo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya wadau dhidi ya Tume kuwa inachelewa kwa makusudi kutangaza matokeo kwa nia ya kubadilisha matokeo ya uchaguzi wa Rais na hivyo kutoa upendeleo kwa baadhi ya wagombea yaani *to doctor the results.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 40 cha Sheria ya Uchaguzi kinafanyiwa marekebisho ili Msimamizi wa Uchaguzi alazimike kuwajulisha wagombea wa nafasi ya Ubunge kuhusu pingamizi dhidi ya uteuzi wao ili waweze kutoa maelezo ya utetezi kabla Msimamizi wa Uchaguzi hajatoa uamuzi wake kuhusiana na pingamizi zilizotolewa.

Vile vile marekebisho yanayopendekezwa yanaweka sharti la kumtaka Msimamizi wa Uchaguzi baada ya kutoa uamuzi wake kuwajulisha wahusika yaani yule

aliyetoa pingamizi na yule aliyepingwa yaani anayegombea. Pale ambapo Msimamizi wa Uchaguzi anakubaliana na pingamizi iliyowekwa dhidi ya mgombea, anatakiwa atoe sababu za uamuzi wake. Utaratibu huu unaopendekezwa utawawezesha wahusika kufahamu hatima inayohusiana na pingamizi zilizowekwa dhidi yao.

Kwa sasa Sheria haimlazimishi Msimamizi wa Uchaguzi kupata utetezi wa mgombea aliyewekewa pingamizi katika ngazi ya uteuzi kabla hajafanya uamuzi hali ambayo huko nyuma imesababisha baadhi ya watu kuondolewa katika orodha ya wagombea bila kupewa fursa ya kujitetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza pia kwamba vifungu vya 88 na 89 vya Sheria hii, 89(a), 90, 91, 92, 93, 94, 95, 103, 104, 105 na 106 zifanyiwe marekebisho ili kuhusisha viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Mapendekezo haya yanatokana na marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi yaliyofanywa mwezi Juni, 2004 kupitia Sheria Namba 13 ya mwaka 2004 ambapo Bunge lako Tukufu lilikubali kuhuisha viwango vya adhabu za vifungo na faini kwa watu watakaopatikana na hatia ya kuvuruga uandikishaji wapiga kura kwa makusudi. Kwa sasa viwango vilivyomo katika Sheria hii katika hatua mbalimbali za uchaguzi haviwiani na uzito wa makosa pamoja na viwango vya adhabu vilivyomo kwa mujibu wa Sheria ya 13 ya mwaka 2004. Hiyo ni Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 hayo ndiyo mapendekezo ambayo tunapendekeza Bunge lako Tukufu liyatafakari na hatimaye liweze kuyatolea maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya pili inayofanyiwa marekebisho ni hii Sheria ya Pacha yaani Sheria ya Uchaguzi kwa Serikali za Mitaa, Sheria Na. 4 ya mwaka 1979. Marekebisho yanayorekebishwa katika Sheria hii yanakusudiwa kuianisha marekebisho yaliyofanywa katika Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 ili kuleta uwiano katika taratibu za kuandikisha wapiga kura hususan utoaji wa kadi zingine za kupigia kura kwa wapiga kura ambao watakuwa wamepoteza kadi zao au kadi zao zitakuwa zimeharibika. Kundi la pili watakaobadilisha makazi kutoka Kata moja au kubadili vituo walipojiandikisha kwenda katika Kata au Kata nyingine au kuhamia katika Kituo kingine na tatu watakaolazimika kubadilisha kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine katika Sheria hii ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, yanayopendekezwa yanalenga katika kuondoa kasoro na mapungufu yaliyojitokeza katika Sheria hiyo na hivyo kuiwezesha Tume ya Uchaguzi kuendesha Uchaguzi wa Madiwani kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10 cha Sheria hii, kinapendekeza kufanyiwa marekebisho ili Maafisa Uandikishaji nao watakiwe kula kiapo kabla ya kuanza kufanya kazi yao kuandikisha wapiga kura kama ilivyo chini ya Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985. Kwa sasa Maafisa hawa wa uandikishaji hawahitajiki kula kiapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 40(1), inapendekezwa kukifanyia marekebisho ili wagombea kwa nafasi ya Udiwani kabla ya uteuzi watakiwe kutangaza maslahi walionayo katika mikataba baina yao na Halmashauri husika. Marekebisho yanayopendekezwa yatawezesha kufahamika mapema kwa wasiostahili kuwa wagombea kuteuliwa kwa vile itaepusha uwezekanao kwa wasiokuwa na sifa kuchaguliwa na baadaye matokeo kuhojiwa Mahakamani na kutenguliwa. Imeshawahi kutokea huko nyuma. Kwa sasa Sheria inamtaka Mgombea Udiwani kutangaza maslahi yanayohusika ndani ya siku 30 kabla ya tarehe ya Uchaguzi. Hivyo Msimamizi wa Uchaguzi hana mamlaka ya kukataa kumteua katika siku ya uteuzi kwa vile uteuzi wa wagombea unafanyika zaidi ya siku 30 kabla ya upigaji kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 44 cha Sheria hii inapendekezwa kifanyiwe marekebisho ili kuwawezesha wasimamizi wa Uchaguzi kupinga na ikibidi kubadili maamuzi ya wasimamizi wasaidizi wa Uchaguzi wa Kata kuhusu pingamizi zilizowekwa dhidi ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Udiwani. Mabadiliko haya Serikali inaamini yatasaidia katika kupatikana kwa maamuzi ya usahihi na ya wakati.

Vile vile utaratibu huu utaepusha rufaa zisizo na msingi kuwasilishwa mbele ya Tume ya Uchaguzi ambapo muda mwingi hutumika kusikiliza rufaa hali ambayo husababisha ucheleweshaji wa maandalizi ya karatasi za kura kwa sababu kama tunavyofahamu maandalizi yake yanategemea maamuzi ya Tume kuhusu rufaa na kufahamu wagombea wanaostahili na wale wasiostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jinsi Sheria ilivyo sasa, Msimamizi wa Uchaguzi hana mamlaka ya kupitia au kuhoji uamuzi uliofanywa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata kuhusu uamuzi wa pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea husika. Hali hii haimwezeshi Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ndiye Afisa Mfawadhi wa Uchaguzi katika eneo analolisimamia kusahihisha makosa ya aina hiyo kwa wakati. Uzoefu unaonyesha kuwa hali hiyo imekuwa inaathiri utekelezaji wa hatua za uchaguzi zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa na Muswada huu yanalenga katika kuhuisha viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali ya uchaguzi ili viwango hivyo viwiane na viwango vipya vya adhabu vilivyowekwa kwa wale watakaopatikana na hatia ya kuvuruga kwa makusudi zoezi la uandikishaji wa wapiga kura. Vifungu vifuatavyo vinahusika na marekebisho haya ni Kifungu cha 87, 88, 88(a), 89, 90, 91, 92, 93, 94, 101, 102, 103, 104 na 105.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuchambua Muswada huu. Serikali inathamini na kutambua mchango wa Kamati hiyo, mchango ambao umeiwezesha Serikali kuwasilisha Muswada huu leo hii Bungeni. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Uchaguzi wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Januari, 2005 Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana Mjini Dar es Salaam na kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, juu ya azma ya Serikali ya kuleta marekebisho ya Sheria mbalimbali za Uchaguzi kama ilivyoelezwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusikiliza maelezo ya Serikali na kupitia mapendekezo hayo kifungu kwa kifungu kwa mujibu wa Kanuni ya 72(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, sasa naomba niwasilishe maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukweli kuwa Tume ya Uchaguzi ni chombo kinachotakiwa kiwe huru. Pendekezo la Serikali kukifanyia marekebisho kifungu cha 4 cha Sheria ya Uchaguzi wa mwaka 1985 kama ilivyo katika kifungu cha 3 cha Muswada kutaka kuwe na uteuzi wa Wajumbe wawili kuingia kwenye Tume ya Uchaguzi, mmoja kutoka kambi ya Chama Tawala na mmoja kutoka Kambi ya Vyama vya Upinzani vyenye usajili wa kudumu. Kamati haikukubaliana na pendekezo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kamati ilipendekeza kwamba kifungu hicho kiondolewe. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na kifungu hicho sasa kimeondolewa kupitia Jedwali la marekebisho ambayo tumekabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kamati bado inasisitiza kuwa kifungu hicho kifanyiwe marekebisho ili Tume iweze kuwajibika kwa Bunge kwa kuwasilisha Taarifa zake Bungeni ili zijadiliwe na zitolewe maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho yanayofanyika katika vifungu vya 17, 18, 19 kama ilivyo katika vifungu vya 4, 5 na 6 katika Muswada vinavyohusu utaratibu wa utoaji wa kadi mpya kwa wananchi watakaopoteza kadi za kupigia kura au wale ambao kadi zao zitaharibika. Kimsingi Kamati yangu ilikubali na pendekezo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wapiga kura watakaobadilisha makazi kutoka Jimbo moja hadi lingine au Kata moja hadi nyingine, Kamati yangu haikuona sababu za

kimsingi za kutaka kutolewa kadi nyingine kwa wapiga kura wanaobadilisha makazi ndani ya eneo moja wala siyo kutoka Wilaya moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilitaka kujua utaratibu wa Serikali wa kuwezesha wapiga kura ambao siku ya kupiga kura hawatakuwepo kwenye maeneo yao ya kupiga kura. Kwa mfano, walinzi, askari, watumishi, wasafiri na wasimamizi wa uchaguzi waweze kupiga zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilitoa ufafanuzi wa kutosha na wa kina kuhusu hoja hii na Kamati iliridhia hoja za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa hadi sasa bado kuna maeneo mengi bado wananchi hawajajiandikisha, Kamati yangu pia ilitaka kufahamu hatua na ukomo ambao Serikali imeweka ili wananchi wote wajiandikishe. Hoja hii nayo ilifafanuliwa na Serikali na Kamati yangu iliafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika eneo hili lilihusu haki ya kupiga kura kwa Watanzania ambao wako nje ya nchi. Kamati yangu iliona kuwa kupiga kura ni haki ya kimsingi ya kila Mtanzania. Hivyo pamoja na Serikali kueleza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi kama ilivyo sasa ni vigumu kuhusisha Watanzania walioko nje. Kamati yangu bado inashauri kuwa kwa siku zijazo Serikali iweke utaratibu wa kuzihusisha Balozi zetu ili zitumike kuandikisha raia halali watumie haki yao ya Kikatiba, kwani Kamati inaamini kwamba kutokufanya hivi ni sawa na kuwanyima haki wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo maeneo ambayo Kamati yangu ilijielekeza sana katika kuhoji na kutoa ushauri kwa Serikali. Aidha, maeneo mengine yalieleweka moja kwa moja. Hivyo Kamati yangu inaafikiana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia namshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake kwa maelezo yao mbele ya Kamati kwa ufafanuzi mzuri uliowezesha Kamati hii kuelewa kwa urahisi madhumuni ya mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri ya kuchambua Muswada huu na kufikia hatua ya kuuboresha katika sura inayoonekana. Naomba niwatambue Wanakamati wa Kamati hiyo kuwa ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Huria Kambarage Nyerere, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa

Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawashukuru Makatibu wetu Ndugu Ernest Zulu, Charles Mloka na Aggrey Nzowa, kwa kuihudumia Kamati hii na kufanikisha kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kuunga hoja hii mkono na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuchukua nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(v)(b) na 81(1) kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi yaani *The Electoral Laws Miscellaneous Amendment Act, 2005* uliowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi kimsingi unafanya mabadiliko kadhaa katika vifungu kadhaa vya Sheria Na. 1 ambayo ni Sheria mama ya Uchaguzi ya mwaka 1985 *(The Elections Act, 1985).* Marekebisho yanayokusudiwa yanalenga katika kuifanya Sheria mama hiyo iendane na mabadiliko yaliyofanywa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na marekebisho yake kama yalivyopitishwa jana.

Kabla hatujatoa maoni yetu katika vifungu mbalimbali vinavyofanyiwa marekebisho, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake kwa mambo ya jumla na kuyahuisha na vipengele mbalimbali vinavyofanyiwa mabadiliko hivi sasa. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kupitia maeneo yote yanayofanyiwa marekebisho katika Muswada ulioko mbele yetu, inaamini kuwa kuna maeneo mengine muhimu ambayo pia yalistahili kufanyiwa marekebisho sasa kuendana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yaliyofanyika katika nchi yetu tangu mwaka 1985. Maeneo hayo ni kama haya yafuatayo:-

Kifungu cha 7 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 35(f) cha Sheria mama katika maeneo kadhaa. Kambi ya Upinzani inadhani kuwa kwa vile kifungu cha 6 cha Sheria mama kinatambua haki ya kurudiwa kuhesabiwa kura katika ngazi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, mara baada ya kipengele kipya cha 6(a) kinatakiwa kipengele kipya cha 6(b) ambacho kitatoa pia matokeo hayo kupingwa Mahakamani. Haiingii akilini kuwa kutokee mashaka katika mahesabu na yakarudiwa na kisha majibu yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi yakawa ndiyo yenyewe yenye uamuzi wa mwisho.

Kambi ya Upinzani inaelewa fika kuwa kifungu hiki pia kinataka Ibara ya 41(vii) ya Katiba ya Jamhuri inayotamka kuwa iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa Ibara hii basi hakuna

Mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake. Kwa maoni yetu pamoja na marekebisho haya ya Katiba kupita jana na Ibara hii imepitwa na wakati na inapingana na dhana nzima ya demokrasia. Haiwezekani kifungu cha 6 kitambue uwezekano wa kuwa na mashaka na mgogoro na kisha mgogoro huo ukaishia tu katika ngazi ya Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni haki ya asili iwapo mgombea hata baada ya kuhesabu hajaridhika apate haki ya kupeleka lalamiko lake yaani *petition* Mahakamani kwa uamuzi. Hatua hii pia inaendana na Kanuni za Uchaguzi za *SADC* kama ilivyosainiwa na Wakuu wetu wa nchi, mwezi Agosti, Mauritius 2004. Tanzania hatuwezi kuwa kisiwa ni lazima tuendane na mabadiliko haya iwapo hatutapata maelezo basi tutaendelea kulizungumzia mpaka tutakapofikia muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Kambi ya Upinzani inadhani inatakiwa kuwepo katika mabadiliko haya ni kifungu cha 35(g) cha Sheria mama. Kimsingi Serikali imefanya mabadiliko katika kifungu cha 35. Lakini kwa kuchagua tu vile vipengele ambavyo Serikali inataka vifanyiwe mabadiliko. Serikali kwa sababu inafahamu yenyewe iyazingatie kabisa maeneo mengi ambayo yamepigiwa kelele na wadau mbalimbali wakiwemo wa vyama vya siasa.

Eneo hilo ni kama kifungu cha 35(f)(viii) kinachosema: *"A Presidential Candidate shall be declared to have been elected President, if he receives the greatest number of all the valid votes cast."* Kipengele hiki nacho kimetoholewa kutoka katika Ibara ya 41(vi) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake ambacho nacho kinasomeka ifuatavyo:-

Mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo tu amepata kura nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wengi pamoja na vyama vya siasa vinaamini kifungu hiki kinahatarisha amani na utulivu na hata uhai wa Tanzania kama nchi. Ni jambo la kusikitisha kuwa Katiba ya nchi inatoa kibali kwa mgombea kushinda hata kwa kura mbili au tatu kwani ndiyo maana ya kupata kura nyingi kuliko mwingine. Inawezekana kabisa ikatokea kuwa mgombea anayeshinda kwa kura nyingi kuliko wenzake wote akashindwa na wenzake katika ujumla wao na hivyo tukawa na mgombea ambaye amekataliwa na asilimia 60 au 70 ya wapiga kura lakini kwa kuwa ushindi ni kwa *simple majority* akashinda kutokana na kifungu hiki. Hii ni kukaribisha hatari katika nchi yetu ambayo kwa miaka yote imekuwa na amani na viongozi wake wamependwa na wingi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache sana zinazoruhusu nafasi kubwa kama hiyo kuchukuliwa kwa *simple majority.* Hali ya kawaida ilikuwa mshindi ni lazima ashinde kwa zaidi ya asilimia 51 yaani *absolute majority.* Iwapo hakuna anayepata asilimia 51 basi uchaguzi unarudiwa katika wiki mbili au tatu zinazofuata yaani *election run off.*

Nchi nyingi ndivyo zinavyofanya na hoja ya gharama au nchi kutokuwa na uongozi katika kipindi hicho haina msingi wowote. Sheria inapaswa kutoa nini kinachofanyika katika kipindi hicho, kwani lazima Rais aliyeko madarakani aapishwe siku mbili baadaye? Mbona Namibia wamefanya uchaguzi toka Desemba lakini Rais mpya anachukua nafasi yake mwezi Machi au Aprili. Nchi zingine zinazotumia *simple majority* yaani Rais kushinda kwa kura zaidi tu kuliko wenzake, wana vipengele vingine katika Katiba zao. Mathalani iwapo Rais atashinda kwa kura chache tu na pia kupata Wabunge wengi basi anaunda Serikali ya mseto. Hata hapa Katiba yetu imekuwa bubu, Kambi ya Upinzani inadhani utawala bora tunaozungumza daima ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kisheria. Amani na utulivu havitakuja tu hivi hivi, viliundwa na vinatakiwa kutunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana kabla ya mabadiliko ya 13 ya Katiba ya Tanzania ilizungumzia kuwa ushindi wa mgombea Urais ni kwa asilimia 51. Lakini bila maelezo ya kuridhisha Serikali mwaka 2000 ikabadilisha kifungu hicho, bila shaka kujilinda yenyewe baada ya kuona kuwa mwaka 1995 wapinzani waliweza kupata asilimia 40 katika ujumla wao. Huu si mchezo mzuri wa kupitisha Sheria kwa vile tu Serikali ina wingi wa Wabunge na hivyo kufanya wanavyotaka kwa maslahi ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ndani ya CCM yenyewe kwa nafasi yoyote kubwa ushindi ni kwa zaidi ya asilimia 51 na ndicho kilichotokea mwaka 1995 vinginevyo sio ajabu tungekuwa na Rais tofauti na tuliye naye leo. Iwapo ndani ya Chama kuna masharti magumu ya mtu kuchukua uongozi iweje katika nchi tunajenga mazingira ya hata kichaa kuweza kuwa Rais wa nchi kwa kumwekea mazingira rahisi ya ushindi. Tusipoangalia maslahi ya muda mfupi mtindo wa Serikali na watawala kulinda maslahi yao ya muda mfupi yatatutokea puani. Amani ikisha kutoweka ni vigumu sana kuirudisha. Hivyo ni lazima kuilinda kwa gharama yoyote ile na si kwa hotuba za viongozi majukwaani. Hatua madhubuti za kisheria na zenye muono wa muda mrefu zinatakiwa hasa katika mambo mazito kama mustakabali wa utawala wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si vema Serikali kuleta visingizio visivyo na maana katika maslahi ya nchi, kwani nchi hii ni yetu sote. Tuna uchungu nayo sote na yatakapoharibika mambo tunaumia sote. Siku hiyo hapatakuwepo na ushabiki wa vyama tena na Watanzania wana haki ya kujua ni kwa nini CCM imebakiza kama kigezo ndani ya chama ushindi wa asilimia 51 na kwa uchaguzi wa Rais wanaweka kigezo rahisi tu cha aliyeshinda wenzake hata kama ni kura moja. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani kwa dhati kabisa inaishangaa Serikali kwa kutoleta mabadiliko kuhusu kifungu cha 98(ii) cha Sheria mama ya Uchaguzi ya mwaka 1985, badala ya kushughulikia mzizi wa tatizo Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko kifungu cha 94 na vifungu vyote vile ambavyo vimetajwa vinaweka faini na kuweka au kuongeza adhabu ya faini au muda wa kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukali wa adhabu hauwezi kuleta badiliko katika jamii kama mzizi wenyewe wa tatizo haujaondolewa ambao ni tafsiri ya takrima kama ilivyo kwenye kifungu cha 98(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kuwa kifungu hiki kiliongezwa mwaka 2000 kuhalalisha takrima. Serikali ndiyo inayojifanya iko mstari wa mbele katika kupiga vita rushwa. Serikali hii hii ndiyo iliunda Tume maarufu ya Jaji Warioba, pamoja na wadau kutegemea kuwa wala rushwa wangekamatwa pamoja na taarifa kuwa Tume ya Warioba imepeleka majina ya wahusika kwa Mheshimiwa Rais na yamekaliwa, Serikali ilikuja na mpya baada ya kusema kuwa lengo la Tume hiyo ilikuwa ni kuainisha mianya ya rushwa na namna ya kuizima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Warioba imeainisha kuwa rushwa mbaya zaidi ukiacha Mahakamani na Polisi iko kwa wanasiasa na hasa na hasa wakati wa uchaguzi na hili hatulifanyii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilidhani Serikali bila kulaza damu ingechangamkia nafasi hii kwa kufanya marekebisho kwenye kifungu hiki na kukifuta kabisa ili kuondoa mazingira ya rushwa katika uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wote wanaofuatilia kwenye vyombo vya habari wanafahamu kuwa siku za karibuni vigogo kadhaa wametamkwa kugawa fedha kama njugu katika hatua ya kununua kura za Wajumbe wa vikao mbalimbali vya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Shinyanga hata majina na namba ya vyumba walikolala yametolewa. Wahusika walitajwa kwa majina waliosemekana kuwatuma wala hawakukanusha wala kupinga. Jambo ambalo linaashiria kuna ukweli, nako Morogoro vikao vya kugawa fedha vimeripotiwa kwenye vyombo vya habari. Mtu hahitaji kwenda shule kuelewa kuwa hivi ni vitendo vya rushwa. Kuna taarifa kuwa Zanzibar nako shughuli hiyo hiyo imefanyika. *PCB* nayo imekaa tuli kana kwamba hawasikii, wala hawasomi chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeulizwa mara nyingi na hata Tume ya Jaji Warioba imelisema kwa ukali wote. Haiwezekani mtu aingie kwenye uongozi kwa rushwa na kisha aipige vita rushwa. Angalau basi Serikali ingefafanua hicho walichokiita katika kile kifungu cha 98 *normal all African hospitality* yaani ukarimu wa Kiafrika ni nini.

Kambi ya Upinzani na hata wadau mbalimbali walishapendekeza *PCB* iwe Taasisi huru na kuwajibika kwa Bunge ndipo itakapokuwa na meno ya kudhibiti matendo yote ya rushwa. Lakini Serikali na wanaoendesha gurudumu la Serikali wameweka pamba masikioni Watanzania hawana tena pa kukimbilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 inayobadilishwa na nimepata *schedule* tena sasa hivi. Kwa hiyo, sina cha kusema lakini ninaomba tu kwamba hicho kipengele basi tutalifanyia kazi kwa wakati muafaka. Kwa sababu imekuja wakati tumepewa ingelikuja wakati tunapewa *Order Paper* tungelifanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4 kinarekebisha Kifungu cha 17 cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985. Kifungu hiki kinazungumzia namna mpiga kura aliyepoteza kadi yake ya kudumu au imeharibika kwa sababu yoyote ile au amehama maskani yake anavyotakiwa kupata kadi mpya ili asikose haki yake ya kupiga kura.

Kambi ya Upinzani hatuna tatizo na kipengele hiki. Hata hivyo Kambi ya Upinzani inadhani tatizo la Watumishi kwa mfano Wasimamizi Wasaidizi, Walinzi, Madereva na watu wengine wote ambao kwa uzoefu siku ya Uchaguzi wanakuwa wameacha vituo vyao na kuwa katika vituo tofauti na kule walikojiandikisha kutokana na kazi na hivyo majina yao hayatakuwepo kwenye *register* au daftari ya kudumu la eneo walikopangiwa hawajaelezwa vizuri ya kuwa watapigaje kura. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, kipengele hiki ni lazima kiwe kwenye marekebisho ya Sheria ili Wasimamizi Wasaidizi ambao kwa kawaida wanajichukulia majukumu pale ambapo hakuna maelekezo yaliyo wazi wasije wakajifanyia wanachotaka wao.

Hii ni haki ya watu kwa upande mmoja lakini kwa upande wa pili daftari la kudumu ni namna moja ya uhakika ya kuondoa hisia ya kura kuibiwa. Hivyo tusiache nafasi yoyote ya mtu mmoja kufanya anavyotaka mwenyewe, watu hawa ni wengi sana kwa Wilaya na hata kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8 kinachorekebisha Kifungu cha 40 cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, Kambi ya Upinzani inapendekeza katika Kifungu cha 4 (a) iwekwe wazi kuwa *notify in writing* ili iwe ya uhakika kuliko watu wanakutana tu njiani na baadaye akatumia hoja ya kuwa alimjulisha. Hii ni hatua ya Kisheria na ni lazima pia iwe na Misingi ya Kisheria. Msingi pekee wenye ushahidi wa Kisheria ni kuwa mhusika ajulishwe kwa maandishi. Kambi ya Upinzani ingependa kuwa pia *with the least possible delay* yawekewe muda maalum hasa ikizingatiwa kuwa Kifungu cha 42 kinatamka wazi kuwa: *"No objection to a nomination paper shall be allowed unless it is made to the return officer not later than four o'clock in the afternoon of the day following nomination day."*

Kambi ya Upinzani inadhani kwa vile pingamizi linapelekwa kwa msimamizi msaidizi, hakuna sababu asilitolee jibu mathalani ndani ya saa 48 ili taratibu zilizopo katika Kifungu cha 46 ziweze kuendelea iwapo pingamizi limekubaliwa. Kambi ya Upinzani inapendekeza pia kuwa katika Kifungu cha 4 (b) nafasi anayopewa mtu aliyewekewa pingamizi *to be heard* iwe ni pamoja na kujieleza kwa maandishi ili kuwa na ushahidi kwa hatua itakayofuata iwapo itakuwa lazima. Kifungu kiandikwe vizuri ili iwe ni pamoja na kupata maelezo ya mhusika kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 88, 105 na 106 vyote vina lengo la kuonyesha faini mbalimbali na muda wa kifungu kwa makosa mbalimbali yanayotokana

na makosa yaliyoainishwa katika Muswada. Kimsingi faini zimelinganishwa na thamani leo. Hata hivyo Kambi ya Upinzani inadhani faini na vifungo ni hatua ya mwisho tu. Tume ya Uchaguzi ijenge kwanza uwajibikaji kwa watumishi wote watakaokuwa wanafanya kazi ya Tume na pamoja na kuwa waajiri wa Serikali Kuu. Tume iwe inashirikiana na wadau kutambua watumishi wake wanaolalamikiwa sana mathalani wakurugenzi wengi wamelalamikiwa kwa kuvuruga uchaguzi kwa makusudi kwa kuvuruga uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2004. Ni vema Tume ya Uchaguzi ikachukua hatua ya mapema kuwachunguza kwa kina na bila ya kuona haya wale wote wanaoweza kuiletea Tume aibu na kuiharibia sifa wachujwe mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji wa Vijiji na Kata, nao wengi wanajihusisha na ushabiki wa kisiasa nao wachujwe ipasavyo. Hakuna maana kusubiri adhabu inayotajwa kwenye vifungu vilivyotajwa wakati mhusika amekwishasababisha gharama kubwa iwapo Uchaguzi utabatilishwa na wakati huu huu licha ya gharama, wananchi wanabaki bila ya uwakilishi. Kambi ya Upinzani inaamini ni muhimu zaidi kujenga Utamaduni wa uwajibikaji kuliko kukimbilia kuongeza gharama za faini na kifungu ambayo mara nyingi wananchi hawana hata muda wa kufuatilia Mahakamani kutokana na gharama ya kesi pamoja na umbali kutoka katika Vijiji hadi ziliko Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 23 cha Muswada kinachorekebisha Kifungu cha 10 cha Sheria za Serikali za Mitaa ya mwaka 1979, Kambi ya Upinzani inapendekeza kirekebishwe na kuandikwa upya ili kiuishe pia kiapo cha uaminifu yaani *oath of allegiance* kwa Tume kwa vile hawa ni watumishi wa mamlaka nyingine na pindi kipindi chote wanapofanya kazi ya Tume haitoshi tu kuwa na kiapo cha kutunza siri. Mambo mengi yaliyotokea huko nyuma ni kuwa hawa wasaidizi wasimamizi wanakuwa na uaminifu kwa mamlaka nyingine kuliko wanavyokuwa kwa Tume ya Uchaguzi. Kuhusu yanayohusiana na adhabu na vifungu yanafanana pia kwa uchaguzi wa Madiwani kama ilivyo kwenye vifungu vya 87 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya napenda nirudie kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na timu yao nzima na kwa namna ya pekee, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutumia muda wao kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu nilikuwa namwomba Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kuhusu utaratibu Kanuni ya 50(8)(b).

**NAIBU SPIKA:** Sawa sawa endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Akitoa hotuba yake Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, amesema uko uwezekano wa Rais kichaa kuchaguliwa tu kwa sababu ya utaratibu tulioweka kwenye Katiba jana wa kumwezesha kushinda kwa wingi wa kura. Sasa Katiba yetu inataja sifa

ya mgombea Urais. Moja ya sifa ya mgombea Urais ni lazima mtu kabla hajateuliwa lazima awe ni mtu mwenye akili timamu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatua ya kuchaguliwa inafuata baadaye. Kwa hiyo, anayechaguliwa kutoka katika chama chochote ni yule ambaye ameteuliwa ana akili timamu. Kwa hiyo, hatutarajii kumpata Rais atakayechaguliwa mwenye kichaa. Haya ni malumbano ya kisiasa ambayo ameyaingiza kwa kulinganishwa na CCM akijua kwamba Rais atayechaguliwa kila mara atakuwa wa CCM.

Kwa hiyo, mimi ningeomba aondoe neno kichaa kwa sababu hakuna uwezekano huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwamba katika Katiba yetu sharti mojawapo la mtu kugombea Urais ni kuwa na akili timamu. Kwa hiyo, ni kweli uwezekano wa kichaa kwa maana ya kichaa kugombea Urais au kuchaguliwa kuwa Rais haupo. Sasa Mheshimiwa Mbunge alisema hayo, aliyasema ambao wote tuliyasikia sasa kuna mawili, moja, kuyaondoa hayo maneno na ukakaa ukaendelea na shughuli yako au kusisitiza uliyoyasema na pengine mambo mengine yaendelee. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Katiba yetu inatoa sifa za mgombea. Lakini ukitazama sifa za mgombea zinazotajwa katika Katiba ni zile sifa ambazo mtu huyo si kichaa yule wa Mahakamani. Lugha kichaa inapotumika ina maelezo mengi. Dunia hii imeingizwa kwenye utata mkubwa na Hitler alikuwa na sifa zote Kikatiba kugombea, lakini akaja akatokea kwa batili yake ilikuwa mbele kuliko wengine. Hii ndio maana inayoimanishwa ukitaka nifute kwa maana ya kuisema ninaweza kuifuta lakini bado maana itakuwa imebakia pale pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mbunge, nadhani anakubali kwamba haya maneno mengi mengi haya ni katika kujaribu kuhalalisha. Lakini ombi langu kwa Mheshimiwa Mbunge kwa tafsiri ya moja kwa moja ya Kiswahili tunachokielewa wote ningeshauri ama useme nasisitiza maneno yangu ama uondoe maneno. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Naomba nisema kwamba nilichokisema nimekisema na naomba kabisa tafsiri hiyo niliyosema kwa maana ya lugha ndio lugha inayokubalika. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Inaelekea Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, anataka kuzungusha kwa *semantics.* Sasa mimi ushauri wangu maana haya yote tunayoyasema yanakuwa *recorded.* Sasa ushauri wangu ni nilichoelewa kwamba unasisitiza ulichosema kwamba hayo uliyoyasema Rais kichaa asije akachaguliwa Rais kichaa. Sasa mtoa hoja hii ambayo tunazungumzia anasema uwezekano wa kuchaguliwa Rais kichaa kutokana na masharti na Katiba tuliojiwekea haupo. Maana tumejiwekea Kanuni ya kuhakikisha kichaa hajitokezi katika kuchaguliwa maana ni kinyume cha Katiba yetu. Sasa ombi ambalo hii ni mara ya mwisho nalisema kwako, kwa tafsiri hii ambayo wote tunaijua ulichokuwa unalenga Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ukinisikiliza wote tutanufaika. Ulichokuwa unalenga pengine ni vizuri bila maneno marefu marefu ni kwamba

hukusema kitu sahihi. Sasa ni vizuri sisi tuachie hapo ama tukuachie maneno yake ya mwisho halafu Mheshimiwa Eliachim Simpasa, naona anaangalia angalia. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema na naomba nirudie na niko tayari kwenda kwa Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwamba nilichotoa ni tahadhari kwamba kama ilivyotokea kwa Hilter mtu wa aina hiyo pamoja na sifa, anaweza kutokea. Sasa kama inaenda kwenye Kamati niko tayari kutetea na ikiwa ni lazima kwenda Mahakamani nitakwenda kupata ufafanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Sawa sawa, basi mimi nadhani nimeelewa kwamba yale ambayo tulidhani tumeyasikia anasema hakusema hivyo. Yale ambayo tulidhani tumeyasikia Mheshimiwa Mbunge anasema hakusema hayo. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba amefuta yale, ila ameweka haya mapya anayoyasema.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kikao hiki lazima kiwe *guided,* hatuwezi kwenda tu kienyeji enyeji. Mimi nataka kulifikisha jambo hili mwisho wake. Mheshimiwa Waziri hayo ndiyo aliyoyasema Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Kwa haya aliyomalizia sasa hivi siyo yale, kwa haya aliyomalizia sasa nadhani yanajifuta yale na nadhani tuendelee. Kwa haya, ya pili maadamu yale ameyafuta amesahihisha hapa mwishoni mimi naridhika kwamba alikuwa sahihi kwa haya ya mwisho aliyoyasema. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya maekelezo na maelezo hayo, sasa ningependa kuwaarifu tu kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge watatu walioomba kuchangia. Wameomba kuchangia baada ya yeye Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alikuwa ndiye msemaji wa mwisho.

Kwa hiyo, baada ya yeye sasa atakuja Mheshimiwa Dr. Amani Kaborou, halafu Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Hao ndiyo majina yao nimepata hapa na ndiyo wa mwisho kwa jioni hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupa pole sana kwa tukio lililotokea. Haya ndio matokeo ya siasa. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ndio kazi yangu.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Ndio kazi yako nashukuru sana katika dakika za mwisho mwisho hizi lazima utuvumilie bado miezi minane utautua mzigo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayorekebishwa hapa ni Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Mwaka huu tunafanya uchaguzi, Tanzania nzima kwa ujumla ndani ya Vijiji elfu tisa na kitu, Tarafa na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii tunarekebisha vipengele muhimu kutokana na daftari la kudumu la wapiga kura badala ya kuandikisha kila mwaka wakati wa uchaguzi, tunaandikisha na baadaye tunapiga kura. Ikitokea wakati wa uchaguzi tunaandikisha tunapiga kura. Kwa hiyo, tumeweka daftari la kudumu, ni jibu sahihi kwa ajili ya kuweka takwimu sahihi ambazo zitawaongoza Watanzania . Sheria ya Uchaguzi

inafanyiwa marekebisho katika maeneo kadhaa ili kuoanisha hali halisi ya hivi sasa ya daftari la kudumu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Umuhimu hasa siyo kupunguza gharama wala tija ufanisi, haueni ya aina yoyote ile ambayo inakuwa ya uendeshaji. Lakini vile vile inadhihirisha tabia ya nchi hii yenye mfumo wa demokrasia iliyouzoea na viongozi makini wanaosimamia demokrasia ili kusudi tuweze kwenda sawasawa. Kunatokea mikwaruzo mingi sana ya kushtakiana. Zilitokea kesi karibu nyingi tu mwaka 1995 najua zilianza kupungua mwaka 2000 na 2005 najua zitapungua na hii naweka mapema.

Sasa kuna maoni machache ambayo nitaweza kuyatoa kwamba kwa mfano demokrasia kwa sasa hivi tunasema watu walioko makini wanaongoza. Sasa hivi tumechagua tayari na tayari kwa kweli kama mimi ningekuwa kama mpinzani nilishaona *indicator* tayari ya kwamba CCM inachukua. Kwa sababu kutokana na uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa kwamba tayari tumekwishapita ila hata kama siyo sisi lakini angalau Chama cha Mapinduzi kinapita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa *indicator* tu kwa asilimia 96.5 tumepata katika vitongoji kwa hiyo, inaonyesha *indicator.* Idadi ya uandikishaji unavyokuwa ningeomba Tume ya Uchaguzi iwe makini katika upande wa vifaa. Kuna Majimbo fulani yaliahirishwa kufanyiwa uchaguzi sababu ya vifaa kutopatikana. Kwa mfano, mwaka 1995 katika kura waliyoandikisha katika upande wa Rais ilikuwa 10,088,484 na waliyopiga kura ni 8,517,568 akazidi asilimia 84. Kwa hiyo, hii takwimu ilikuwa inajulikana mapema basi vile vituo vya uchaguzi kwa mfano vingekuwa vimeshapelekewa mapema kwa ajili ya mambo haya. Kwa hiyo, ilibidi watu wengine wasubiri baadhi ya maeneo kadhaa kungojea. Katika maeneo ya hatari kwa mfano maeneo ya mbali kutoka Wilayani kwa mfano maeneo Kidunda uende mpaka sehemu ya Chalinze ndio unapata barabara ya kwenda Seregete A uende Seregete B, unamchukua mtu wa kitongoji kwa mfano wa Kivuma Livumo kilometa 13 halafu aende akapige kura kule Ulilingwa. Kwa hiyo, unakuta kama hao kwa sababu kuna watu waandikishaji wa wapiga kura kule watu kama 800 na kitu kwa hiyo wanaandamana kule. Hivyo utakuta kura nyingi tunazikosa kwa ajili ya hilo kuwa karibu kwa sababu liko daftari la wapiga kura basi vituo viwe karibu na maeneo ambapo wananchi wanaandikishia na vifaa vifike mapema. *(Makofi)*

Halafu semina wakati kama huu kunatokea semina nyingine lazima zidhibitiwe na Tume. Kuna baadhi ya *donors* wataanza kuja kama wanazo fedha za kusaidia kweli mambo ya *civics,* kuwasaidia Watanzania siasa waijue. Basi fedha zile zingekuwa zinasimamiwa, zisije moja kwa moja tunataka kwenda kutoa semina kundi fulani kwamba kuelimisha wananchi zipitie Tume. Kuna semina tunajua kwamba ni muhimu zile za simamizi, vyama vya siasa, wandikishaji, wale ambao ni wasimamizi na wapiga kura mwenyewe wakipata semina hawa tunalenga. Kuliko kuwaelekeza eneo ambalo halistahili kwa watu ambao hawastahili unawakabidhi vitu ambavyo siyo vyao. Sawasawa na mtu ananunua miwani au analeta miwani ya jua wakati ya kwako tuwakabidhi vitu ambavyo vinastahili.

Halafu lingine utoaji wa fedha kutoka Hazina. Uzoefu umeonyesha kabisa kwamba fedha hizi za kwenda kwenye Tume kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Kwa mfano, mwaka 1995 ilitolewa katika awamu nane utakuta mpaka fedha nyingine zilitolewa mwezi Novemba ambapo uchaguzi ulishakwisha tayari katika zile shilingi bilioni 21.5 zilizotolewa kwenda kwenye Tume ya Uchaguzi. Hazikutolewa kwa upande kwa kutegemea kununua vitu ambavyo vilitegemewa.

Kwa hiyo, lazima Tume ya Uchaguzi isaidiwe ili kuletewa fedha mapema. Lingine ni kuhusu masuala ya vituo na fomu zile ambazo zinatakiwa. Kuna mapungufu ya fomu kwa mfano, kuna Fomu *FR(1)* na namba moja na namba sita za kura zile *CF No. 3* mpaka 7 za malalamiko. Unakuta wengine wanalalamika tu.

Pendekezo lingine kuhusu vyama vingine wakati unahesabu kura wanafanya fujo. Kwa hiyo, tumeamua hizi *transparent boxes* tumependekeza yale masunduku ambayo ni *transparent* kila chama kiwe na sanduku lake. Kwa sababu ili akiona sanduku lake hakuna kitu, aondoke mapema pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akiona sanduku la Chama cha Mapinduzi linashindiliwa pale Ngerengere, Kabingu - Ukerewe, Janija - Nzega, Ukangaliaji - Pemba basi anaona chama kingine kinaondoka kama hakuna hata karatasi.

Kwa hiyo, likiwa *transparent* ataona mle ndani hamna kitu wanakata tamaa wanaondoka mapema ili kura zihesabiwe kwa njia ya utulivu. Ndio maana mbuzi alikosa mkia kwa sababu ya kelele. Walipangwa foleni siku moja wanyama ili watofautishwe na binadamu wakaambiwa pangeni foleni Mwenyezi Mungu akawaambia, ninyi mtapata mikia ili kuwatofautisha na binadamu sawa. Wakakaa kwenye foleni sasa mbuzi katika wanyama wote duniani ukikaa sehemu lazima mbuzi utamsikia tu mbuzi na jogoo. Mbuzi akaanza kupiga kelele tatataa! Mungu akauliza nani anapiga kelele, wakasema mbuzi huyo kamsemea sungura. Sasa akawaita wote na kuwaambia mtapata mikia yenu mapema ili muondoke hapa. Ndio maana wakapata mikia mifupi, waliotulia simba walipata mikia mirefu.

Kwa hiyo, Chama cha Mapinduzi kitulie kitapata mkia mrefu na ushindi wa kishindo mwaka huu. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Kwanza niunge mkono kwa asilimia mia moja ila nina sehemu chache tu za kuboresha na kuiomba Serikali kwamba tuweke utaratibu unaoeleweka na ni rahisi kutekelezwa. Kwa watu ambao wamepoteza kadi zao za kupigia kura waweze kupiga kura bila ya matatizo. Utaratibu uwekwe na elimu itolewe wakati wa kupiga kura kusiwe na matatizo. Wengine ambao wako mbali na vituo vyao kwa mfano mtu kaachika karudi kwao kuwekwe utaratibu unaoeleweka na uwe rahisi ili wale watu wasipate usumbufu katika kupiga kura au mtu ameachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mawakala. Kuandaliwe kabisa kama ni malipo kwa sababu wanasumbua kweli Jimboni. Mimi mpaka kesho nasumbuliwa na mawakala, sina raha. Sasa utaratibu uwekwe kabisa hawa mawakala wapewe kabisa, wasisumbue sumbue tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni takrima. Kupiga kura ni karibu kutwa nzima, sasa kama kuna mtu anataka kuwakirimu watu kwa nini watu wasile? Kwa hiyo, suala la takrima nasisitiza ni ruksa. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii. Awali ya yote niseme toka mwanzo kwamba naunga mkono hoja hii na naipongeza tena Serikali kwa kutuletea Muswada makini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia katika hoja iliyotolewa, naomba tu niwaelezeWatanzania wenzetu wanaotusikiliza wakati huu kutoka katika Bunge lako kwamba Wabunge jana wamepitisha Marekebisho ya Katiba na Watanzania wote wanayo haki ya kufurahi hasa wanawake. Wanawake ambao ndiyo asilimia 52 ya Watanzania wafahamu kwamba vyama vingine hawawataki. Maana walitoka nje, hawakuunga mkono ile hoja na wamepinga Katiba. Maana kama wangekuwa wanataka nafasi hizo basi wangebaki wakaunga mkono hoja na kupinga vifungu vingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, natoa wito kwamba akina mama waelewe kwamba Chama cha Mapinduzi kiko na wanawake wote wa nchi hii na ndicho chama chao ambacho kinataka maendeleo yao. Kwa hiyo, natoa wito kwao wawe makini katika uchaguzi. Waangalie wasije wakaingia kwenye kuchagua pumba, wachague mchele safi ambao ni Chama cha Mapinduzi kinachowahakikishia maendeleo ya Kitaifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie katika eneo la zile kadi za kujiandikisha. Napongeza huu utaratibu lakini naomba tuangalie. Kwa sababu katika uandikishaji inawezekana vijana walio vyuoni na mashuleni wanaweza kujiandikisha majumbani mwao au kwenye vituo vya shuleni. Tuangalie utaratibu makini ili vijana wetu ambao wametimiza umri wa kupiga kura haki yao isipotee. Vile vile madereva ambao mara kwa mara wanasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru Bunge lilinipeleka Namibia kwenda kuangalia uchaguzi kule. Wenzetu walikuwa na utaratibu wa kuwawezesha watu ambao wa Majimbo mengine kwenda kupiga kura katika Majimbo ambayo siyo yao ilimradi kuwekwe sanduku maalum kwamba hawa watu hawatokani na eneo husika. Kwa hiyo, tukijiwekea utaratibu ambao unaeleweka utawasaidia hawa ambao wamejiandikisha kwa mfano, Jimbo la Kongwa, lakini bahati mbaya wakakutwa wako Lindi Mjini hawakosi fursa yao ya kupigia kura chama chao na Rais ambaye wanamtaka.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningependa kugusia suala la takrima. Rushwa ni adui wa haki. Lakini unapomsaidia mwenzako baada ya kufanya kazi ngumu aweze kula au kunywa maji hiyo siyo rushwa! Huyu mtu umeshinda naye kutwa kwa mfano, wakati wa

kampeni toka asubuhi na kumaliza kampeni saa kumi na moja jioni mnafanya tathmini, mkae mnatazamana wasile!

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siyo rushwa! Au wakala wa chama chako amekaa kituoni toka asubuhi mpaka jioni anakaa na njaa. Hivi ukienda kumnunulia soda ukampelekea pale anakula ni rushwa? Ama sivyo huyu unataka azimie, kesho asiweze kuendelea na kazi. Kwa hiyo, mimi naomba tuiangalie vizuri maana ya rushwa na takrima ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ningependa kuchangia katika kura za Rais. Kwa kweli mimi nina hakika Serikali ya CCM iliporekebisha Sheria hii wala haikuwa na wasiwasi kwamba itashindwe. Kwa sababu kura zote za Upinzani ukijumlisha hazijawahi hata siku moja kufikia kura za CCM.

Kwa hiyo, kusema kwamba Sheria hii imerekebishwa kwa sababu ya uoga wa CCM wala si kweli, ni katika kupanua demokrasia na kujiwekea utaratibu ambao utatusaidia. Hata mwaka huu wa 2005, katika chaguzi za Serikali za Mitaa tayari *indicator* imeonyesha nyekundu kwa wenzetu tena kwa hatari. Chama ambacho kimepata ushindi katika nchi nzima kwa asilimia 1.4 leo kitambe dhidi ya chama kilichopata asilimia 96 kweli hii ni sahihi! Maana yake sisimizi anataka kujifafanisha na tembo, inawezekana hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hebu naomba Watanzania twende kwenye uchaguzi tukiwa na amani na uhakika wa ushindi wa Chama cha Mapinduzi. Nashukuru. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu-Mashariki na wengine wote waliopata misiba ya wazazi wao, wake zao, watoto wao na ndugu zao wa karibu, Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, naisifu Serikali kwa kubuni na kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daftari hilo la Kudumu ni suluhisho la utata katika upigaji wa kura kwa msingi wa haki kwa sababu udanganyifu katika kura utapungua, uhalali wa upigaji kura kuboreka, kumbukumbu za wapiga kura zinakuwepo, matumizi

mazuri ya muda wa siku ya Uchaguzi (muda mfupi) na ni njia ya kisayansi zaidi na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi waliochelewa kujiandikisha, sababu zake ni Serikali. Ushauri wangu kwa Serikali hususan siku ya kupiga kura kwa wananchi naomba kanuni za upigaji kura kwa wasiojua kusoma na kuandika ni vizuri zibainishwe waziwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mtu asiyejua kusoma na kuandika hutakiwa yeye mwenyewe kutafuta mtu mwingine wa kumwandikia kura yake kwa mujibu wa kanuni zilizopo. Njia hii haina haki hata kidogo kwani anayemsaidia anampigisha pengine tu matakwa yaa Mpiga kura hayatimii. Mchezo huu unachangia sana kuvuruga shughuli za demokrasia na haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia yenye nafuu ni kwamba wasiojua kusoma na kuandika waingiapo chumba cha kura wapate msaada wa kupiga kura kama ifuatavyo, mawakala wa vyama na wasimamizi wa kura wahakikishe Mpiga kura anatimiza matakwa yake, mpiga kura ataje kwa sauti kwa mtu anayemtaka au chama chake na msimamizi atapiga kura hiyo wazi wazi mbele ya mawakala. Kwa utaratibu huu upigaji kura utakuwa kwa kiasi fulani wa haki. Utaratibu ambao utakuwa kinyume cha hapo ni vurugu tupu. Eneo hilo ni nyeti sana kwa hiyo litazamwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya makosa ya Uchaguzi ni kuhusu kujiandikisha na uteuzi wa Wagombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma vizuri Muswada wenyewe ambao umetaja marekebisho ya adhabu hizo na faini zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu ni kwamba nia ya Sheria hizi ni kulinda usalama kwenye mazingira ya chaguzi hizo, kuzuia watu wabaya wanaochafua Uchaguzi, kuwa na shughuli za Uchaguzi zenye amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia nyingine kama vile kuimarisha na kulinda uhuru wa watu, amani ya watu, utulivu wa watu, usalama wa watu, demokrasia na nidhamu katika Uchaguzi wowote. Vile vile adhabu mliyopendekeza ni ndogo mno. Mimi napendekeza iwe maradufu ya ile mliyopendekeza na nia ni kutibu makosa ya kijinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya makosa ya Uchaguzi yaani makosa mengine na marekebisho katika Sheria za Serikali za Mitaa. Adhabu ya makosa katika maeneo yote kama yalivyofanyiwa marekebisho na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri adhabu mliyoipendekeza kwa makosa mbalimbali kwamba adhabu iwe mara mbili hii ni ndogo haitibu chochote. Tusifanye mzaha na masuala ya Uchaguzi. Serikali nayo ipate adhabu kwa makosa ya kusababisha watu wenye haki ya kujiandikisha kupiga kura kushindwa kufanya hivyo. Kwa mfano, uchache wa *film* za picha, madaftari ya kujiandikisha, ubovu wa kamera na umbali wa vituo vya kujiandikishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha Hoja niliyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu adhuhuri hii.

Kwanza nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kusema humu Bungeni au kwa maandishi. Lakini kubwa zaidi kwa dalili ya wazi kabisa kwamba wengi wa Waheshimiwa Wabunge wameelewa Muswada huu na ndio maana pamoja na kwamba hawakuomba wachangie, lakini wameelewa maudhui na shabaha ya Muswada huu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini kama ilivyo kawaida niwataje tu ambao wamechangia kwa kuongea humu Bungeni nikianza na Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Maria Watondoha. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Khalid Suru na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, wote nawashukuru sana.

Katika hoja ambazo zimezunguzwa nitaenda kwa kasi kidogo kwa sababu ya muda. Niseme tu ni kweli siku ya uchaguzi yenyewe patakuwepo na makundi ambayo yatahakikisha kwamba uchaguzi huu unafanikiwa yaani watasimamia watatoka kituo walichojiandikisha na kwenda kituo kingine. Makundi haya kwa sababu Tume ya Uchaguzi ndio imewaweka katika utaratibu huu, itawapatia utambulisho maalum ambao utawawezesha watu wa aina hiyo kupiga kura katika kituo ambacho watakuwa wametumwa kusimamia shughuli hii, huo ndio utaratibu ambao utatumika. Tusisahau Waheshimiwa Wabunge, jana niliuliza swali zuri tu kuhusiana na kwamba kuna wananchi wengi sana ambao kwa bahati au kwa sababu mbali mbali hawakuweza kutumia hii fursa yakujiandikisha na walikuwa wanasema sasa tunafanya nini maana wako wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tusisahau kwamba wakati Serikali inawasilisha Muswada wa Marekebisho Sheria za Uchaguzi si kuweka hili daftari la kudumu tulieleza wazi ili tuweze kufanikisha zoezi hili, tumegawa katika awamu mbili, awamu ya kwanza ni hii inayoendelea sasa hivi. Awamu hiyo ni muhimu sana kwa sababu inataka tupate taarifa zote sasa kwa nchi nzima kwa watu ambao wana haki ya kupiga kura. Zoezi hili sasa linaloendelea litafuatiwa na hatua nyingine muhimu sana ya kurudisha taarifa hizi kwenye maeneo ambayo wananchi wamejiandikishia kupiga kura na taarifa hizi zitawekwa mahali pa wazi. Ili sasa kutoa fursa kwa yule mtu aliyejiandikisha akiona kwamba mbona jina langu taarifa ninazoziona humu si sahihi mimi ni mwanaume lakini

inaonyesha jinsia yangu ni mwanamke na mengine ya namna hiyo yawezekana huyo mtu amejipenyeza, yeye sio raia au hajatimiza miaka kumi na nane yupo kumi na sita na tunaamini ifikapo siku ya tarehe ya uchaguzi hatakuwa amefikisha miaka kumi na nane.

Sasa inatoa fursa ya mwananchi mwadilifu kuweka pingamizi kwa hilo na pingamizi hilo likithibitika Tume itayasahihisha hayo na ndio maana muda wote huu unahitajika sana tutakapokamilisha hiyo sasa mbona *heater* ndio ipo *phase one* sasa inahitimishwa na kipindi cha *objection* kinakamilika na wale wanaotaka kusahihisha taarifa zao wanakamilisha na zinarudishwa Makao Makuu kuingiza taarifa zote hizo katika daftari la kudumu ambalo na taarifa hizo ndiyo zitakazotumika katika uchaguzi huu na katika chaguzi zijazo ambazo zitakuwa zinauhishwa

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tukiomba sana kwamba turuhusu kwa wananchi ambao hawakupata fursa, tufahamu tutakuwa tumevuruga zoezi zima. Hatutaweza kuwahi kwa sababu na yenyewe lazima twende na hiyo *process* ya kwanza, halafu turudi katika hali ya kuhakiki halafu ndio irudishwe tena. Muda wenyewe tunasema haupo na taarifa hizi tunadhani kwa ratiba ambayo Tume imejiwekea kama yapo masahihisho tunajua *the maximum period* ambayo itawezekana haitaenda zaidi ya mwezi wa saba kuweza kufanya masahihisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pale jamani tuombe kabisa kwa wale ambao bahati mbaya hawakuweza kujiandikisha kwa safari hii ya Uchaguzi Mkuu tuwaachie wale ambao wamebahatika kufanya hivyo wawaamlie viongozi kwa niaba yetu. Lakini watakuja waingizwe waandikishwe na kunufaika na haki yao hiyo katika chaguzi zinazokuja na kwa vijana ambao sasa hivi tunaamini ifikapo tarehe ya uchaguzi watakuwa wametimiza miaka kumi na nane Sheria inaruhusu kwamba wajiandikishe mradi athibitishe kwamba hilo ni kweli. Hilo nadhani niliseme ni kweli watanzani wako wengi sana wako nje ya nchi na wangelipenda sana na wao kutumia haki yao ni rai ilitolewa kwenye Kamati, tuliijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uchaguzi hii ya mwaka 1985 na hii Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa. Labda nianze kwa kusema hivi Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuanzia Ibara ya 5 inatoa hii haki yako hii, haki ya mwananchi ya kupiga kura lakini inasema haki hiyo itawekea utaratibu kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Sasa Sheria iliyotungwa na Bunge ni hizi Sheria mbili tunaziongolea kwa ngazi ya uchaguzi wa Rais na Wabunge ni hii Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, Sheria namba moja na kwa uchaguzi wa madiwani ni hii Sheria ya Mitaa namba nne ya mwaka 1979. Sasa hizi zimeweka utaratibu huo kwamba wewe lazima ili utumie haki yako hiyo uende ukajiandikishe katika kituo cha kujiandikisha na utaenda kupiga kura katika kituo cha kupigia kura pale ulipo jiandikishia ndani ya Tanzania ndiyo Sheria inavyosema hivyo. Kwa hiyo, hata tungependa sasa hivi kwanza tuirekebishe Sheria hii ili tuweze kuruhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndio tunasema hoja hii inazungumzika na nadhani mbele ya safari itabidi Serikali iliangalie kwa makini eneo hili na kuona

utaratibu upi unaoweza kuwawezesha Watanzania hawa na wenyewe wakanufaika na haki yao hiyo, kwa hiyo, tugange yajayo.

Ilitolewa hoja hapa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, nadhani umenisaidia kuyajibu mengine, Muswada huu hauhusu Katiba, vifungu alivyovitaja vya 41(7) ni kweli unakiona katika kifungu cha 35 (f) Ibara ya (8) ni kweli kabisa, lakini kifungu hiki kilichomo katika Sheria ya uchaguzi hatukigusi kwa sababu msingi wake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumehitimisha mjadala wa Katiba kwenye maeneo haya, ninavyokumbuka zilikuwepo hoja zimewasilishwa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili na tulitegemea sisi jana kwamba kwa vile walikuwa wametoa taarifa ya kuleta marekebisho katika eneo hilo la Katiba kwamba wenzetu wangekuwa wajasiri wa kusimama na kuwaeleza Watanzania kwa nini wanataka kuwakilisha hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichoshuhudia na Watanzania wote wamekifahamu, sasa wenzetu hawakuwasilisha hoja yao waliondoka kwenye Ukumbi wa Bunge sasa leo ndio naambiwa kwamba kwa nini Serikali inataka iruhusu utaratibu huu. Hapana, utaratibu huu ulikubaliwa na Watanzania wenyewe kupitia ripoti ya Kamati ya Jaji ya Robert Kisanga, walitoa sababu zao kwa nini utaratibu huu uwe hivyo na hivyo hivyo kwa upande wa kwa nini katika ngazi ya uchaguzi wa Rais usihojiwe Mahakamani, wananchi wamelieleza kwa ufasaha sana suala hili. Sasa Katiba hii tunasema msingi wake ni matakwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Sisi kama viongozi tunaweza kuwa na mawazo mazuri, lakini kuwa na mawazo mazuri hakuhalalishi kwamba yale mawazo mazuri ya wengi ya kwako ndio wayachukue, jenga hoja kama watakubaliana na wewe watasema sawa. Kwa sasa hivi wameshasema wao wanataka Rais wetu aweze kuchaguliwa kwa kura zilizo nyingi zaidi ya wengine. Nadhani tutaendelea kuyaheshimu matakwa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Rais kichaa limeelezwa vizuri sana, umelieleza vizuri sana. Katiba hii kwa maana tunayohifahamu sisi kwa sababu Mahakama yenyewe itaelekezwa na Sheria za Tanzania, zinasema nini kuhusu mtu atamkwe kuwa ana matatizo ya akili. Inasema nafasi hiyo haipo kabisa na yawezekana kutokuwa na akili kule Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa ambako anausemea sio huu ambao sisi tunasema kwenye Katiba. Kwa hiyo, nchi hii itaendelea kupata marais wazuri tu na tutaendelea tusiwe na wasi wasi na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda sana nikueleze jambo moja kwamba nchi za Kiafrika ni vizuri tukajenga demokrasia inayoendana na mazingira yetu na utamaduni wetu, ni vizuri hilo tukaliangalia kwa makini, tuangalie yanayoendelea sehemu zingine. Ni vizuri hii hoja kwamba Rais aliyepatikana kwa *simple majority* basi awajibike eti kuwajumuisha na wale wengine iwe Serikali ya mseto, hiyo haina hoja ya msingi. Katiba hii inakupa fursa wewe kama chama uende ukaombe ridhaa ya wananchi kama ukishinda watasema chukua uongozi wa nchi yetu, kama hukushinda, huwezi kuja kwa mlango wa nyuma, hiyo ni kweli. Sasa hii ya kusema mustakabali wa nchi yetu

utaimarika zaidi kama mtatuingiza na sisi katika Serikali ya mseto, mimi nasema hilo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kidogo hili suala la takrima, unafahamu suala hili linapotoshwa kweli kweli na wanaopotosha wana sababu zao. Takrima iliyomo katika Sheria ya Uchaguzi sio ile ya rushwa, imeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na tumelieleza humu Bungeni mara nyingi sana. Haiwezekani kabisa, mimi hainiingi kwenye akili yangu.

Wote tunajua zipo gharama halali za uchaguzi, tunajua kabisa na pia tunajua Mheshimiwa Diwani au Mheshimiwa Mgombea wa Urais au Mgombea wa Ubunge ana timu yake ya mapambano. Sasa hawa ni binadamu kama mgombea yeye mwenyewe, sasa inafika wakati jioni au mchana wanataka wakafungue kinywa au adhuhuri au magharibi. *(Kicheko)*

Sasa wewe unasema jamani mimi naenda, kaeni kidogo hapo pembeni hapo mimi naingia ndani na mke wangu tukale chakula, sawa unaweza ukayafanya hayo, lakini siamini kama kesho utakuwa nao. Watakuuliza sawa mzee endelea na hiyo kitu yako. Lakini la msingi ni kwamba Mahakama ndizo zinazoamua kama imevuka kiwango cha takrima kama inavyosema kwenye Sheria sasa imeingia kwenye rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda sana niwaombe sana Watanzania wenzangu na Waheshimiwa viongozi wa Wabunge kwenye eneo hili, wale wanaopiga kelele waseme kama unajua mtu alivuka mipaka, kwa nini hutaki kwenda Mahakamani? Waulizeni tu kwa nini hamtaki kwenda Mahakamani? Huko ndiyo utapata tafsiri sahihi. Lakini mimi nasema takrima kama ilivyopewa tafsiri katika Sheria ya Uchaguzi tumesema inaendana kabisa na taratibu na mila na desturi za Watanzania na hata kokote ambako jamani chaguzi zinafanyika, tunajua yanafanyika. Marekani jamani angalieni yaliyotokea si mnaona, mbona hamtaki kusema hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inapofika kwetu sisi wenyewe tunaanza kujidhalilisha tu kwamba rushwa katika jina takrima hapana, zipo gharama halali zinazoendana na uchaguzi na moja ni hiyo binadamu tumeumbwa lazima tule kidogo ili tupate nguvu ya kufanya kazi. Sasa wakale wapi, wakale polisi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hatuwezi kuendesha suala la kupambana na rushwa kwa taarifa za magazeti, mimi naomba kabisa tunaendelea kuomba Serikali mtusaidie kama taarifa ambayo inaweza kufuatiliwa mtu unaifahamu tupeleke kwenye vyombo vinavyohusika, vyombo halali, ndiyo tutakuwa tunajenga na kuongeza kasi ya kupambana na tatizo la rushwa hapa nchini. Lakini tukiishia tu taarifa za magazeti hata mimi naweza nikaandika *story* ya kuzusha kuhusiana na mtu ninaye pambana naye ili niweze kumshughulikia kwa namna hiyo. Lakini hiyo naamini ni utaratibu ambao haufai kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda niseme Serikali imesema mara nyingi humu Bungeni, tungependa tuone uchaguzi wa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa amani na utulivu kwa ngazi zote na tutahakikisha kabisa hilo linafanyika

na kwa upande wa Tume tunaamini itajitahidi sana vifaa vya kupigia kura vifike kwa wakati katika vituo vya kupigia kura visiwe mbali sana na wapiga kura kwa sababu inaweza ikawafanya kukatisha tamaa na tutahakikisha kabisa kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vinakuwa macho na wale ambao wanakuwa na *agenda* yao au yakutaka kuvuruga uchaguzi. *(Makofi)*

Mwisho niseme kabisa kwamba hao watakaoteuliwa kufanya kazi ya kusimamia zoezi la uchaguzi tunawaomba kabisa watekeleze majukumu yao kwa uadilifu na wakifahamu kwamba Sheria hii ya uchaguzi ya mwaka 1985 na hii ya mwaka 1979 tumeweka adhabu zinazoweza zikawahangaisha sana iwapo watapatikana na makosa ya kuvuruga uchaguzi au zoezi la uchaguzi kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatakie Watanzania wote na ninyi viongozi Waheshimiwa Wabunge na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa amani na salama, mfanikiwe katika yale yote mnayotafuta katika mwaka huu  na Mwenyenzi Mungu atawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mhehsimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005**
***(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona  muda uliobaki ni mchache, tutakwenda vile vile tulivyofanya kama Muswada uliopita, tutakwenda sehemu kwa sehemu ili tuweze kukamilisha.  Lakini narudia tena hii haimnyimi mtu nafasi kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye angependa kuhoji kifungu chochote, nafasi ipo. Katibu.

Kichwa cha Muswada

*(Kichwa Muswada kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005**
***(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005 yaani *The Electoral Laws Miscellaneous Amendmets) Bill, 2005* pamoja na mabadiliko yaliyofanywa na kuukubali. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005 *(The Electoral Laws Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)* sasa ukubalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kuapitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tumefikia mwisho wa shughuli za leo. Sina tangazo lolote, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.28 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 8 Februari, 2005 saa tatu asubuhi)*